Kikao cha Sita – Tarehe 23 Mei, 2014

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2014/2015. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Saleh Nassor Juma (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2014/2015, sasa naomba kuwasilisha.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 - Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Ahsante sana. Waheshimiwa Wajumbe, tulikubaliana jana kwamba mara tutakapoingia baada ya dua, tunaanza kusikiliza maelezo kuhusu majumuisho. Kwa maana hiyo, nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mola Muumba kwa kutuwezesha kutuamsha salama na kutuwezesha kufika katika Baraza lako hili tukufu na kutupa uwezo wa kufanya shughuli zetu, yeye pekee ndiye mwenye uwezo wa yote tunamuomba atuwezeshe tufanikishe shughuli zetu hizi na aijaalie nchi yetu katika hali ya salama, amani, utulivu na umoja.

Mhe. Spika, baada ya hayo napenda nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Baraza lako hili tukufu, ili na mimi niweze kutoa maelezo kadiri Mwenyezi Mungu atakavyoniwezesha na baadae Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atakuja kufanya majumuisho ya mwisho kwa ajili ya wizara yetu hii ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, aidha, nichukue fursa hii kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa imani yake juu yangu ya kunipa heshima hii kubwa ya Taifa letu ya kuwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Namshukuru sana na namuombea dua yeye na familia yake azidi kupata neema kubwa na afya njema.

Mhe. Spika, aidha, nimshukuru Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais kwa namna anavyoshirikiana na wizara yetu na mashauri yake juu ya wizara hii yanatuwezesha sana katika kufanikisha shughuli zetu. Shukurani maalum ziende kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa namna anavyotusimamia katika wizara yetu, miongozo yake, ushauri wake na namna anavyotuweka karibu katika kutekeleza majukumu yetu. Namshukuru sana Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, pia, niwashukuru mawaziri wenzangu wote kwa mashirikiano yao ambayo ni ya karibu sana na kusaidia katika utendaji wa shughuli zetu. Aidha, niishukuru sana Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa namna ambavyo wanatusaidia katika kutekeleza wajibu wetu na niwashukuru Wajumbe wote wa Baraza hili la Wawakilishi kwa mashirikiano makubwa wanayoipa wizara yetu.

Mhe. Spika, aidha, niwashukuru Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote wa wizara hii pamoja na wafanyakazi wote kwa mashirikiano makubwa wanayonipa katika kutekeleza wajibu wangu.

Mhe. Spika, shukurani za pekee ziende kwa familia yangu kwa ustahamilivu mkubwa wanaonistahamilia na kunipa moyo, ingawa muda mwingi nakuwa nje ya shughuli za kijamii kutokana na majukumu yetu ya Kitaifa. Nawaomba waendelee na moyo huo wa kunisaidia na kunivumilia.

Mhe. Spika, nianze na hali ya siasa. Katika eneo hili lilichangiwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi, ikiwemo Kamati yenyewe ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Mhe. Subeit Khamis Faki, Mhe. Nassor Salim Ali, Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mhe. Asaa Othman Hamad, Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Mussa Ali Hassan, Mhe. Fatma Mbarouk Said, Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa na Mhe. Mahmoud Thabit Kombo.

Mhe. Spika, kwanza nianze tena kwa kumshukuru Rais wetu mpendwa Dr. Ali Mohammed Shein kwa uvumilivu, ustahamilivu na umakini wake katika kuiongoza nchi yetu.

Mhe. Spika, kuongoza Serikali yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa sio kazi rahisi hata kidogo, lakini ni umakini na busara zake zimetuwezesha kutufikisha hapa tulipofika na Mwenyezi Mungu amsaidie ampe uwezo zaidi wa kuendelea kufanya majukumu yake kwa Taifa letu. Aidha, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwamba hata akichokozwa hachokozeki, hakuna jambo gumu kama kuvumilia unapochokozwa na hasa unapochokozwa na mtu unayempenda ni tatizo sana kuvumilia. Kwa hiyo, namshukuru na nampongeza sana Rais kwa msimamo wake huo.

Mhe. Spika, tatizo letu Wazanzibari kadiri tunapoelekea katika Uchaguzi Mkuu, basi tunaanza malumbano ya kisiasa, jambo ambalo kwa njia moja ama nyengine haitusaidii kabisa katika mustakabali wa nchi yetu.

Mhe. Spika, katika nchi ambayo inahitaji kuvumiliana, kusameheana, hakuna kama Zanzibar. Kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe na wananchi wote wa Zanzibar tuvumiliane, tusameheane, tuanze ukurasa mpya tusahau yaliyopita, tushikamane ili kuimarisha umoja, mshikamano na upendo wa nchi yetu. Hii ndio njia pekee ya mafanikio na maendeleo ya Zanzibar, vyenginevyo vyote basi ni kujirudisha nyuma na kupoteza muda.

Mhe. Spika, katika ulimwengu wa leo uchumi ndio siasa na mtu yeyote akidhani kwamba siasa za malumbano ndio kujitengezea umaarufu, ukitaka upate umaarufu wa kisiasa katika ulimwengu tulionao, basi uoneshe ni namna gani utapiga hatua katika suala zima la kujenga uchumi wa nchi yetu. Ulimwengu wa leo unazungumzia kuimarisha masoko, kukuza biashara, kukuza uwekezaji, kuimarisha ajira, kuimarisha elimu na afya, kuimarisha kipato, kuwasaidia wananchi ili waweze kujijenga kiuchumi na kujenga mahusianao ya kikanda na kuhakikisha kwamba nchi ina amani, utulivu na umoja.

Mhe. Spika, huu ndio uvumilivu wa leo ulivyo, vyengine vyovyote ni kwenda nje ya mstari wa mahitaji ya ulimwengu wa leo. Tuache malumbano, tuache kupotosha, tuache kuchonganisha, tuache kufitinisha na sasa tuunganishe wananchi ili tuishi kwa salama na amani katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa upande wa Muungano. Muungano ndio umoja wetu na Muungano unasaidia sana katika kuimarisha shughuli za kiuchumi wa nchi yetu kama tutazitumia vizuri fursa hizo. Katika eneo hili kulichangiwa na Waheshimiwa wafuatao:

Mhe. Spika, kwanza Kamati yenyewe ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ilivyowasilishwa na Mwenyekiti wake Mhe. Hamza Hassan Juma, ilichangiwa pia na Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Ashura Sharif Ali, Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa na Mhe. Mahmoud Thabit Kombo. Waliochangia eneo hili wote walitaka tuendelee kuimarisha Muungano wetu na kuondoa kasoro zinazojitokeza katika Muungano huo. Sisi kwa upande wetu tunauchukua ushauri huo.

Mhe. Spika, lakini nataka niseme tu kwamba hakuna Muungano usio na changamoto, kwa sababu Muungano ni sehemu ya maisha, tutamaliza changamoto zilizopo, lakini bado zitakuja nyengine mbele yetu. Kwa hiyo, ni wajibu wetu katika maisha ya kila siku kutafuta njia moja ama nyengine ya kutatua matatizo yetu na msingi wa matatizo yetu, lazima tuyatatue kwa kutizama chanzo gani cha asili ya tatizo lenyewe, sio hata katika mambo ya msingi

kuchanganya mambo ya siasa wakati yako mambo ya msingi ambayo yanahitaji kushughulikiwa katika kutatua maisha ya kila siku kwa manufaa ya watu wetu.

Mhe. Spika, katika masuala ya Muungano zimezungumzwa kero za Muungano, lakini nataka nikuhakikishie kwamba Kamati yetu ya pamoja tumeyazungumza mambo haya na katika mazungumzo yetu huwa hatuogopani, kila mmoja hujenga hoja hakuna anayemuogopa mwenzake wala hakuna anayemuona mwengine ni bwana wa kumpigia magoti.

Mhe. Spika, wakati mwengine sisi ni watu wazima tunaposema mambo mengine si vizuri kutamka maneno ambayo unavunja heshima ya mwenzako. Sisi ni watu wazima, ni wanaume sawasawa tena vidume vya kweli kweli, sasa tunapokwenda kuzungumza katika mazungumzo yote tunazungumza kwa uwezo wetu, hatumpigii mtu magoti na mtu yeyote anayetaka kunijaribu aje anijaribu kama mimi ni kidume. Kwa hiyo, masuala mengine lazima ufahamu, tunapozungumza hapa lazima tuheshimiane, hakuna mtu wa kumpigia magoti, tunayoyazungumza tunazungumza mambo ya msingi ya kutatua matatizo yaliyo mbele yetu.

Mhe. Spika, matatizo ya Muungano yaliyopo sasa ni mengi yanahitaji ufumbuzi wa Kikatiba. Serikali zetu mbili zimeyazungumza mambo haya mengi na imeona ni muwafaka sasa haya yaliyobaki yanahitaji kupata ufafanuzi wa Kikatiba. Kwa hivyo, ni wajibu wetu sote kushiriki vizuri katika Bunge la Katiba katika kutetea hoja za msingi za maslahi ya Zanzibar. Maslahi ya Zanzibar hayapatikani kwa kusema unatetea Zanzibar, lazima kujenga hoja za msingi zitakazoonesha umetetea Zanzibar katika mambo ya msingi yenye maslahi ya maendeleo na uhai wa Taifa letu.

Mhe. Spika, yako mambo tumeyazungumza sana humu ndani ikiwa ni pamoja na suala la mafuta na gesi asilia, suala la Tume ya Pamoja ya Fedha, suala la misaada na mikopo na suala la kupunguza mambo ya Muungano. Hayo ndio masuala makubwa ambayo sasa yanahitaji utatuzi wa Kikatiba na njia pekee ni kushiriki kikamilifu katika Bunge la Katiba ili kujenga Rasimu itakayohitajika kuwa na Katiba bora tukaipeleka kwa wananchi.

Mhe. Spika, kwa hiyo, nataka nikuhakikishie kwamba serikali zetu zimekubaliana kwa dhati kabisa kupata ufumbuzi wa matatizo haya, lakini msingi wake ni lazima kupata dira ya Kikatiba. Vile vile, suala la Zanzibar kuhusu kushirikiana na Taasisi za Kimataifa nalo halina mjadala.

Mhe. Spika, hata Katiba ya sasa Rasimu iliyoko mbele yetu katika Bunge la Katiba imeliona jambo hilo na limo. Kwa hiyo, jambo la msingi ni kushiriki vizuri, tukajenga hoja na tukatatua matatizo yaliyo mbele yetu. Si kwa kufanya mikutano ya hadhara, si kwa kufanya maandamano, hayo mambo badala ya kupunguza matatizo, yataongeza matatizo, yataongeza malumbano, yataongeza ugomvi, yataongeza kuhasimiana na chuki, hayatusaidii katika mafanikio ya kujenga nchi, lazima tuwe wakweli katika kutetea mambo ya nchi ili tupate ufumbuzi ulio sahihi kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Spika, liliulizwa swali hapa kwa nini Viongozi Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama wanatokea upande wa Tanzania Bara peke yake? Nisingependa kuzungumzia sana jambo hili kwa sababu nimelijibu sana katika maswali mbali mbali na nimeeleza, ni mamlaka ya uteuzi ndiyo yenye mamlaka ya kuteuwa Wakuu wa Vyombo hivyo vya Ulinzi na Usalama. Mahala pekee pa kulizungumza hilo ni kule kule kwenye Bunge la Katiba, tunayo haki ya kulizungumza hili na kuliwekea utatuzi kama tunaona kuna kasoro ya aina yoyote, lakini kwa sasa mamlaka hayo anayo Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mimi sina uwezo wa kumuingilia katika mamlaka hayo.

Mhe. Spika, kuhusu kwa nini Mabalozi wetu walio nje ya nchi wanaoiwakilisha Tanzania kwa Zanzibari ni idadi ndogo. Hili atakuja kulieleza kwa kirefu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa sababu pia aliwahi kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje. Kwa hivyo, ana udhoefu nalo na kwa sababu serikali zetu mbili zinayo maoni kuhusu jambo hili.

Mhe. Spika, kuhusu Mikopo ya Elimu ya Juu kwa Wazanzibari. Nataka niseme katika moja ya fursa ambayo tunaipata katika Jamhuri ya Muungano ni mikopo ya elimu ya juu. Hivi sasa Wazanzibari wana fursa mbili, wana fursa ya kupata elimu ya juu kupitia vyuo vilivyopo Zanzibar na vile vile, wana fursa ya kupata elimu ya juu kupitia vyuo vilivyopo Tanzania Bara. Wanapoomba mikopo kule hawatazamwi kama hawa ni Wazanzibari au Watanzania Bara, wanatizama vigezo vya *qualification* yako unavyofaulu, wanakupa mkopo kutokana na vigezo ulivyonavyo na

kwa taarifa zetu tulizonazo kwamba Wazanzibari wengi wanapata fursa hii licha na wale Wazanzibari wanaotoka huku kwenda kuomba kusoma katika elimu ya Juu, lakini pia, Wazanzibari wanaoishi huko Bara wanapata fursa hiyo sawa sawa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa hivyo, ndugu zangu kuna mambo mengine "hala hala mti na macho" mambo mengine yanatusaidia yanatupa manufaa kwetu, tusitafute namna ya kuyachokoroa na baadae tukakosa haki zetu ambazo tunapaswa tuzipate. Kwa hivyo, mimi ni muumini na nitaendelea kuwaamini kwamba suala la Elimu ya Juu libaki katika mambo ya Muungano. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kuhusu Utumishi katika Taasisi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hili jambo kwenye Kamati yetu ya pamoja limemalizika, tumekubaliana kwamba ugawaji wende kiasilimia, Zanzibar ipate asilimia 21 katika Taasisi za Muungano na kwa upande wa Tanzania Bara ipate asilimia 79 na sasa hivi tunategemea utaratibu kwa namna za utekelezaji wa suala hilo, ndio jambo liliopo. Kwa hiyo, maani jambo hili litatufikisha pahala pazuri. (*Makofi*)

Mhe. Spika, pia, liliulizwa swali hapa kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, alituunganisha vipi Wazanzibari katika Bunge la Katiba. Hilo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais mwenyewe yupo atakuja kulieleza kwa kina.

Mhe. Spika, kuhusu Sherehe za Mapinduzi, Sherehe za Mapinduzi ni zotu sote. Mapinduzi yetu sote nia na dhamira ya Mapinduzi ni kujenga Umoja wa Wazanzibari, Maendeleo ya Nchi hii, kuondosha dhuluma na ubaguzi wa aina zote, ndio ilikuwa nia yake na ndio tunayoitekeleza mpaka leo na sote humu ndani tumekula fadhila za Mapinduzi haya, hata kuwemo kwetu humu kwenye Baraza hili kabla ya Mapinduzi haya tusingekuwemo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa hiyo, sharti tuelewe Mapinduzi haya yamefanyakazi kubwa na tuwashukuru waliofanya kazi hiyo na tuwapongeze na tuwaombee dua waliotangulia mbele ya haki. Kuja ukakejeli, ukafedhuli na ukakebehi ah! tena haya mambo yamezidi.Tutaenzi Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 na kuendeleza kumbukumbu zake na kuheshimu waasisi wetu na kuendeleza Historia yetu, tutaendelea na kuyaheshimu na kuendeleza Historia ya Mapinduzi. Hivi vielelezo tunavyoimarisha ni katika kuenzi na kuendeleza Mapinduzi Matukufu. Kwa hiyo, jamani suala la Mapinduzi ni suala la Kimataifa ambalo linatuhusu sote. Sitegemei kwa kila mara tukayasema mengine. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kuhusu sherehe hasa sherehe za miaka 50, ndugu zangu hakuna sherehe ndongo wala hakuna sherehe ya nchi ndogo na kubwa haina tafauti, maana kama ni gwaride vikosi hivyo hivyo vinavyochezwa Dar-es-Salaam, ndivyo hivyo hivyo vinachezwa Zanzibar na Zanzibar viko vingi zaidi kwa sababu viko na vya SMZ, kama ni shamra shamra inakuwa ni sawa sawa, kama ni ngoma ni sawa sawa, kama halaiki ni sawa sawa na kubwa zaidi, basi Zanzibar katika Sherehe za Mapinduzi tunafungua miradi ya Maendeleo katika maeneo mbali mbali. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa hiyo, tusidhani kabisa kwamba zitakuwa gharama ndogo, gharama zitakuwa kubwa. Nataka niwaambie najua gharama ukubwa wetu hatufiki hata asilimia 10 ya gharama zinazotumiwa na wenzetu kwa upande wa pili. Kwa hiyo, mjue kwamba watendani hawa wanafanya kazi nzuri, wanajibidiisha sana kadiri wanavyoweza kujidibiisha ili kuhakikisha kupunguza gharama za sheria zetu na mambo mengine ambayo kwa Taifa letu.

Mhe. Spika, kiutaratibu tuna Kamati Kuu ya Sherehe na maadhimisho na ndio inayofanya maamuzi ya namna sherehe zenyewe ziwe na maoni yao na mapendekezo yao yote yanakwenda serikalini kwa kupata maamuzi ya mwisho. Kwa hiyo, kila linalotekelezwa huwa tayari limepata baraka za serikali na ndio utekelezaji unaanza na katika utekelezaji huo kuna Kamati 11, kuna Kamati ya Bahari na Uenezi, Kamati ya Afya, Kamati ndogo Pemba kuna Kamati na Nishati, kuna Kamati ya Mapokezi na Ukaribishaji Wageni, Kamati ya Halaiki, Kamati ya Mapambo, Tamasha na Tafrija, Kamati ya Usafiri chakula na Malazi, Kamati ya Gwaride, Kamati ya Uhamasishaji na Maandamano na Kamati ya Sekreterieti, wala isiwepo dhana ukafikiri kwamba hizi fedha zinapokuja zinakuja Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na wao ndio wanatumia kwa matumizi ya hizo Kamati. Fedha zinapokuja zinakwenda moja kwa moja kwenye kamati husika kutokana na makisio ya kamati husika.(*Makofi*)

Mhe. Spika, bajeti yetu inatokana na Kamati makisio ya Kamati na kwa sherehe za mwaka huu. Kwa mujibu wa makisio ya Kamati baada ya kujibana walikuja na makisio ya bilioni 4 na mililioni 695 milioni, ndio ilikuwa tukamilishe sherehe. Kwa hivyo, tunapokuja tukapewa bajeti ya bilioni mbili, maana yake ni asilimia 40 tu ya makisio ya Kamati zenyewe. Kwa hivyo, inapotokeza nyongeza ya milioni mia tatu mia nne ni mambo yatajitokeza katika utekelezaji.

Mhe. Spika, kwa hiyo, ninachotaka kusema matumizi yaliyohitajika kwa Kamati yalikuwa bilioni nne milioni mia sita na tisini na tano. Fedha zilizopatikana ni bilioni mbili na milioni mia nne. Kwa hiyo, mimi kwanza nilikuwa nataka niwapongeze watendaji hawa kwa namna ambavyo walijibana kwenda tena kushauriana na Kamati na Kamati zikatekeleza wajibu wao kwa kiwango cha asilimia 40 tu ya lengo lao. Sasa liliulizwa swala hapa, nani aliruhusu kuhaulisha?

Mhe. Spika, kuhaulisha zipo taratibu zake za kisheria na sisi tunafuata utaratibu wa kisheria. Kwa hivyo, tulihaulisha na tukapata idhini wa Waziri wa Fedha, ndio matumizi mengine yakafanyika na serikali inayatambua matumizi yaliyofanyika. Kwa hivyo, uhaulishaji ulifata utaratibu na idhini kwa Waziri wa Fedha ulitoka na ndio maana mambo yakafanyika na sherehe zikafanyika.(*Makofi*)

Mhe. Spika, sasa wako watu walidhani tutashindwa kufanya sherehe, sherehe tumefanya na tutaendelea kufanya, maana vitisho vingi vilitoka mara hii sijui hivi na hivi, sisi hatuogopi vitisho, nyie endeleeni na sisi tutaendelea kufanya mambo ya msingi ya kujenga nchi yetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kuhusu gharama za ujenzi wa Mnara. Gharama za ujenzi wa Mnara zote jumla ni shilingi bilioni mbili na milioni mia, ndio gharama za ujenzi wa Mnara. Mpaka sasa shilingi bilioni mbili zimetumika. Kwa nini sasa hivi Mnara umesimama kidogo kuendelea kujengwa, si tatizo la mkandarasi hata kidogo, ni tatizo lililojitokeza katika kunawirisha Mnara wenyewe. Wenyewe wenye Mnara wamiliki ni *ZSSF*, baada ya kwenda *Seattle*, wakakuta Mnara wa *Seattle*, ule unazunguka na wakasema na huu nao uzunguke ili ukikaa kule juu unaona yote Zanzibar unapiga *round* pale, rafikiri Mhe. Abdalla Juma ukenda kula *Restaurant* pale utafurahi.(*Makofi*)

Mhe. Spika, sasa kilichotokea ni kwamba kwa sababu ya umuhimu na umakini wa kujenga ili isitokee athari imechukuliwa hatua maalumu na fedha ni zile zile ili utengenezwe utaratibu na mara utakapokamilika huo utaratibu wa hilo dubwana la kuja kuweka pale kwa msingi wa kuwa kule juu kuzunguke kwenye Mkahawa, shughuli itaendelea.

Mhe. Spika, kwa hiyo, hayo ndio yaliyosababisha kucheleweshe na nisema kwamba hizi si fedha za serikali, hizi ni fedha za *ZSSF*, baada ya kufanya tathmini ya kuona kwamba Mnara ule unaweza kujiendesha kibiashara na kifaida kwao, ndio wakachukuwa maamuzi hayo. Kwa hivyo, gharama zinazotumika zitarejesheka kwa *ZSSF* na wao hawaishii kujenga Mnara tu pale, kuna mambo mengi yatafanyika na itakuwa chanzo cha kuifungua Zanzibar kibiashara zaidi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kutoka na Historia ya Michenzani, tumeamua kuendeleza Historia hiyo ili pawe eneo la biashara, eneo la kupumzikia watu jioni, iwe eneo la kupata Historia ya nchi yetu. Kwa hiyo, katika Mnara kutakuwa na Mkahawa, kutakuwa na Maktaba, kutakuwa na kumbukumbu za Viongozi wetu na Historia yetu na kwa ule upande uliojengwa Mnara kutakuwa na bustani mwanana baada ya kusongamana Forodhani na kwengine kama Darajani, tutakaa Michezani tupunge upepo kwa burdani ya hali ya juu na hata Kisonge tushakubaliana tunajenga pale wanatuuzia eneo lao tutalinunua ili tujenge kitu cha maana na tutashirikiana nao hayo ndio matokeo. Kwa hiyo, tunafanya jambo kwa kujua kwa mtizamo mtakaoleta haiba na sura ya Zanzibar mpya. (*Makofi*)

Mhe. Spika, liliuliza swala hapa kuhusu Makusanya na mapato yanayotokana na maduka katika jengo lile la Ghala la Sherehe na Maadhimisho. Naupokea ushauri, nataka niihakikishie Kamati na Wajumbe kwamba tutahakikisha kwamba wale wote wenye maduka kwenye maeneo yale wanalipa kodi stahiki na fedha zinaingia katika mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, kuhusu mkopo wa *Mapinduzi CUP*. Kwanza niipongeza Kamati ya *Mapinduzi CUP*, Kamati hii imefanya kazi nzuri na wamefanyakazi vizuri na hasa kupitia Wizara husika ya Habari na Michezo na wakafanya kazi nzuri ya kuhamasisha michezo mbali mbali hasa hasa mchezo wa mpira ya miguu. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa kazi hiyo. Pia, nimpongeze Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali kwa kuwaamua kuwakopesha fedha ambazo *Mapinduzi CUP* walitaka kutoka kwa Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali.

Mhe. Spika, lakini napenda niseme hivi hii *Mapinduzi CUP* ni taasisi isiyo ya kiserekali. Kwa hiyo, si vyema kuipaka matope kwa jambo lililokuwa si lake. *Mapinduzi CUP* wamekwenda kukopa kwa Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali na mimi nakushukuru kwa kuwakopesha, lakini kidogo limetokea tatizo. Tatizo la msingi

lilikuwa hapa, ulipoona umecheleweshwa kulipwa pesa zako, ulikuwa uwasiliane na Kamati ya *Mapinduzi CUP*, wajue kinachadaiwa na wao wangekubaliana, walipoona kwamba jambo hili limewashinda, wangewasiliana na Wizara husika na wizara husika itakapoona jambo hili limewashinda, basi sisi milango yetu iko wazi na nakuhakikishia hili jambo halitushindi.

Mhe. Spika, tatizo hapa ambalo nafikiri hata Mhe. Waziri wa Bahari limemkera ni Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali kujikurupukia ukenda kwenye vyombo vya Habari kabla ya kupitia kwenye kamati husika, kabla ya kwenda kwenye uongozi wao mkakaa mkazungumza.Nataka nikuhakikishie kwamba hakuna linalotushinda, hili ni jambo dogo sana kwetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa hiyo, ninachokwambieni kwamba madhali sasa mmelileta kwetu, tutachunguza tulimalize na utaona tutalimaliza vipi, maana uwezo wa kulimaliza tunao, lakini si vyema kuipaka matope serikali kwenye mambo ambayo yanatokea kwa nia njema. Kwa hivyo, Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali milango yetu iko wazi na madhali sasa umeleta malalamiko rasmi kwetu nakuhakikishia utaona majibu yetu.

Mhe. Spika, kuhusu Idara ya Maafa, kwanza niseme ushauri tumeupokea na nataka niwahakikishie Wajumbe tutaufanyia kazi. Katika eneo hili limechangiwa kwanza na Kamati yenyewe ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Subeit Khamis Faki, Mhe. Nassor Salim Ali, Mhe. Ali Salim, Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mhe. Fatma Said, Mhe. Mwanaidi Kassim, Mhe. Raya Suleiman Hamad, Mhe. Hamad Masoud, Mhe. Bikame Yussuf, Mhe. Marina Joel Thomas na Mhe. Ashura Sharif Ali. Nataka niwapongeze sana Waheshimiwa kwa michango yenu na miongozo yenu ambayo itaisaidia idara hii kufanya wajibu wake vizuri. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwanza tunakubali umuhimu wa kujitayarisha na kujiandaa kwa maafa, tunajua umuhimu huo na tumefanya kazi kubwa katika eneo hili na tuko njiani ya kufikia muafaka mzuri na hivi sasa tumewashauri wenzetu wa *UNDP* na *UNICEF* ili tushirikiane katika kupata ufumbuzi wa kujitayarisha na kujiandaa kwa kukabiliana na maafa. Kwa mwaka huu wenzetu hawa wamekubali kutusaidia shilingi za kitanzania bilioni moja milioni mia tatu na thalathini na mbili elfu laki nane na thamanini kwa kuanzia. Hata hivyo, kuna nchi nyengine rafiki tunaendelea na mazungumzo nao tuone nao watatusaidia kwa kiasi gani na kwa taarifa za awali mazungumzo yetu yanakwenda vizuri.

Mhe. Spika, nia yetu ni kuwa na vijana wenye taaluma katika eneo hili kuwa na vifaa vya kisasa vya kukabiliana na maafa, kuwa na majengo mazuri ya ghala za kuekea vitu vya maafa na kuwa na vitu vyote muhimu kwa ajili ya kukabiliana na maafa. Hili sio jaribio dogo ni jaribio kubwa na linalihaji mchango wa kila mmoja wetu, lakini pia, linahitaji wenzetu washirika wetu katika maendeleo ili tuweze kufanya kazi hii vizuri.Kwa hivyo, nawahakikishieni Waheshimiwa chungu kinapikwa kama anavyosema Mhe. Hamad Masoud na iko siku Mwenyezi Mungu akitupa uhai na uzima tutakipakua tukiona idara hii imejitayarisha vizuri imejijengea uwezo vizuri kwa sababu niliyoyasema yote ni mambo ya msingi.

Mhe. Spika, kuhusu Sheria ya Mfuko wa Maafa, hii sheria muda mrefu tulikuwa tunamaliza, lakini tulipokwenda kwa wadau ilikuwa na changamoto nyingi mambo mengi yameongeza wametupa utaratibu mzuri zaidi wa kuifanya sheria iwe bora zaidi, ndio maana sheria hii ilichelewa. Sasa sheria imekamilika na wakati wowote, sasa itakwenda kwenye Kamati ya Makatibu wakuu ili iende serikalini kwa maamuzi ya mwisho ya kuileta kwenye Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, hatimae tutakuwa na Mfuko wa Maafa, naamini kwamba mfuko huo utatusaidia sana kwa mambo mengi ambayo yamelalamikiwa.

Mhe. Spika, kwa wakati wa sasa huu, idara hii haina mfuko maalum wa maafa, yanapotokea matatizo tunakwenda serikalini kuomba fedha zitoke mfuko mkuu. Kwa hiyo, wananchi wasitegemee sana kwamba kila watakapopatwa na maafa watapata msaada wa serikali. Watapata msaada wa serikali pale ambapo uwezo upo.Wangependa sana kushughulikia kila tatizo linalojitokeza katika maafa, lakini serikali inajitahidi kadiri inavyowezekana na wale wanaoathirika zaidi, basi serikali hujitahidi kusaidia, lakini kama mnavyojua Waheshimiwa Wajumbe hali yetu ni ngumu ya kiuchumi.

Mhe. Spika: Mheshimiwa alipanga dakika kama 45 kwa ajili ya ufanye majumuisho kwa upande wako, ili Mheshimiwa nae apate kuja kupata muda. Katika dakika 45 zimebakia dakika 10.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ahsante, nitajitahidi, lakini Mheshimiwa mambo ni mengi. Kwa hiyo, nafikiri yale nitakayoyabakisha, basi Waheshimiwa watanivumilia, lakini niseme kwamba tutajitahidi sana kufanya yale ambayo tunayoshauriwa na Baraza hili ili kutekeleza wajibu wetu vizuri.

Mhe. Spika, pia, liliulizwa swali, kwa nini fedha za mchango wa serikali mara hii zilikuwa milioni 40, mwaka jana ilikuwa milioni 70. Hii ndio uhalisia wenyewe wa hali halisi ya bajeti, maana bajeti yetu ya maendeleo niliyopata mwaka huu tumeipata ukilinganisha na mwaka jana, upungufu wa asilimia kama 40 na hiyo ya mwaka jana tulipopanga milioni 70, tulifanikiwa kupata milioni 10 tu. Kwa hiyo, umepanga ya 40, naona ni uhalisia wa hali yenyewe ambazo fedha zitakazoweza kupatikana.

Mhe. Spika, kwa nini bajeti ya wahisani ikawa kubwa, tushukuru bajeti ya wahisani iwe kubwa, mimi naomba iwe kubwa zaidi, maana haitoshelezi, hii niliyopata tunataka tupate zaidi. Kwa hiyo, tuombeane dua tupate nyengine, hii si ya kuiuliza tena.

Mhe. Spika, kuhusu Kiwanda cha Uchapishaji, hivi sasa tumo katika hatua ya awali. Namshukuru Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein kwa msaada mkubwa aliotupa katika kukamilisha kazi hii, lakini niseme kwamba hii ni awamu ya kwanza tu, bado tunayo kazi kubwa mbele yetu kukiimarisha kile kiwanda, maana tulikuwa tunakwenda kwa awamu, hii ni awamu ya kwanza sasa, kuna awamu ya pili na awamu ya tatu, ndio kwanza tuna mashine moja tu ya *digital*. Katika kiwanda chochote kunatakiwa angalau *minimum* uwe na mashine mbili na ikiwezekana zaidi ya hapo. Sasa hivi tuna moja, maana yake ikitokea kasoro yoyote ya kiufundi kazi inalala.

Mhe. Spika, kwa hiyo, tunaanza na nawashukuru watendaji tumeanza vizuri, tunaomba tupewe moyo, kuna mambo mengi yanahitajika pale. Uchapaji sio ile kiwanda cha kuchapishia tu, kuna mambo mengi, kuna visu na mambo mengine. Kwa hiyo, yote hayo tumo katika kutafuta namna nyengine ya kukabili ili tuweze kufanya vizuri.

Mhe. Spika, lakini kubwa zaidi ni mafunzo hatuna wataalamu pale, tuna ufinyu wa wataalamu, wataalamu wetu waliopo wote wa kubahatisha bahatisha. Kwa hiyo, hilo lieleweke. Sasa kazi tuliyonayo kubwa ni kutaalimisha, lakini safari ya kukifanya kiwanda kiweze kujitegemea kifanye shughuli zake nyengine kwa kibiashara na nyengine za serikali tumo njiani na hivi sasa tumeshafanya tathmini na iko tayari ya Mpango wa Mkakati, Mpango wa Kiuchumi kwa ajili ya kiwanda hichi, tutawasilisha serikalini na serikali sasa itaamua ni muundo gani uwe wa kiwanda hichi ili kiweze kujitegemea zaidi na kiweze kutoa huduma bora zaidi.

Mhe. Spika, kuhusu kwa nini malengo ya mwaka jana yalikuwa makubwa na makusanyo yakawa madogo, jibu ni rahisi. Malengo tulitarajia kiwanda kiwe kimeanza kazi, lakini kwa bahati mbaya kutokana na tatizo letu la kifedha tulichelewa kupeleka fedha kwa wakati unaotakiwa. Kwa hiyo, tukachelewa kupata mashine kwa wakati unaotakiwa.

Mhe. Spika, kwa hiyo, ile *projection* yetu haikuweza kutekelezwa, lakini mwaka huu nakuhakikishieni Waheshimiwa Wajumbe tutafikia lile lengo ambalo tumeliweka, Mungu ajaalie twende salama, isitokee misukosuko yoyote na mashine iendelee kufanya kazi kama inavyofanya kazi na watu wetu wajitahidi kufanya kazi vizuri na huku tukiwaelimisha ili waweze kutekeleza wajibu wao.

Mhe. Spika, kuhusu makusanyo ya utafiti malipo yake yanakusanywa na Mtakwimu Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, sisi wizara yetu hatutozi ada za utafiti. Idara ya Faragha ambayo na hii ilichangiwa na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Kamati yenyewe, Mhe. Mahmoud Thabit Kombo na kadhalika. Kuhusu *escort* za viongozi, ni kweli *escort* za viongozi ziko hali mbaya.

Mhe. Spika, mimi niseme tu ushauri tunaupokea na tukaufanyie kazi zaidi ili tuondoe aibu hii, bado ni mtihani kwetu na ule msaada ambao tulitegemea tuupate kwa wenzetu wa Oman, naona mpaka sasa hatujaupata, lakini na hapa kwetu kuna mambo mengi hatujui tunasema vipi pengine tutawakera ndugu zetu, baadhi ya maneno yetu pengine tunarukaruka tukenda tukasema wenzetu wengine wakasema hivi na vile matokeo yake yakatokea maneno ambayo pengine kwa njia moja au nyengine yakasababisha kuchelewa kupata msaada huo. Kwa sasa siwezi kuwa na jibu halisia.

Mhe. Spika, ujenzi wa nyumba za viongozi jambo hili lipo kwenye Mfuko Mkuu wa serikali na naamini kadiri ya uwezo utakavyopatikana, nyumba za viongozi wetu hawa zitashughulikiwa, lakini kwa upande wetu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tayari tunayo michoro, tayari tunavyo viwanja kule Pemba. Kwa hiyo, kazi iliyobaki ni kujengwa kwa nyumba.

Mhe. Spika, kuhusu usafiri, tatizo lipo, sisi katika wizara yetu tumepanga kununua gari moja mwaka huu, Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji akija hapa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais nae ataeleza mipango yao ni vipi kwa ajili ya upande wa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, kuhusu ushauri wa kuwa na *CCTV Camera* wazo tunalipokea tutalifanyia kazi tunategemea sana hali ya uwezo wa kifedha.

Mhe. Spika, kuhusu safari ya Marekani ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Jambo la kusikitisha sana ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija mambo mengine haya tunapoyauliza na tusipofanya utafiti tukapata ukweli halisia saa

nyengine tunaweza kugombanisha viongozi wetu wakubwa, tunaweza kuleta mtafaruku katika nchi yetu kwa mambo ambayo ungekuja mimi ukaniuliza ningekupa taarifa vizuri zaidi.

Mhe. Spika, hakuna hata kiongozi mmoja anayesafiri katika nchi hii ikaletwa taarifa yake hapa Baraza la Wawakilishi, hata sisi Wawakilishi hatuleti taarifa zetu hapa, kwa sababu zipo kwenye bajeti zetu zinajulikana utaratibu wake na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hafanyi safari ambayo haina tija, hafanyi safari kwa kwenda kuharibu fedha, hafanyi safari isipokuwa ina nia ya kujenga.

Mhe. Spika, nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Afya jana alilieleza jambo hili kwa upana wake, lakini lazima tuelewe hakuna serikali inayoendeshwa bila ya gharama. Viongozi wetu wakubwa hawa wanapokwenda safari wanaijenga nchi yetu. Jana alisema pale kuna msaada wa kompyuta wenye thamani ya bilioni 4.

Mhe. Spika, lakini nakwambieni tumekwenda *Microsoft* mambo mangapi tumeahidiwa kufanyiwa na watu wake wamekuja hapa tumeanza mazungumzo nao, tumekwenda kuonana na *Bill Gates Foundation* wanakuja kutusaidia katika mambo mbali mbali ya kilimo na mpaka Chuo chetu cha Kizimbani. Kuna mambo mbali mbali ambayo wenzetu wale wa *COSTECH* wamekusudia kutusaidia. Kuna suala la *Schumer Group* kujenga nyumba za Mbweni na kadhalika.

Mhe. Spika, kwa hiyo, tunapoambiwa lazima tujiambie na ukiambiwa changanya na zako. Kwa hiyo, mimi sitaki niseme fedha ambazo zinatumiwa kwa sababu nitajenga *business* mbaya na ikabidi sasa kila kiongozi hapa tuje tutaje fedha zilizotumiwa, lakini nataka nikuhakikishie sio dola laki tatu na nusu. Kwa hiyo, ili tukitaka jambo, sisi tupo, ni vizuri tuheshimu viongozi wetu wakuu hawa ili mambo yaende vizuri.

Mhe. Spika, kuhusu Tume ya Uchaguzi, niseme ushauri tunaupokea na niliona Tume ya Uchaguzi imechangiwa sana na Kamati yetu hii Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Ali Salum Haji, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mhe. Hamad Masoud Hamad na Waheshimiwa wengine.

Mhe. Spika, kwanza niseme kwamba elimu kuhusu uchaguzi itaendelea kutolewa na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa elimu itaendelea kutolewa kwa wananchi ili waelewe suala zima la haki yao ya kupiga kura.

Mhe. Spika, kuhusu maandalizi ya Kura ya Maoni yanaendelea na tayari bajeti imetengwa kwa ajili ya Zanzibar bilioni 4.3 kwa ajili ya kuendesha Kura ya Maoni Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, nataka niseme jamani watendaji wetu wa Tume waadilifu, wanafanya kazi yao kwa mujibu wa kazi yenyewe kwa kufuata sheria za nchi na kubwa Tume ya Uchaguzi mambo yake mengi yanayoongozwa na Katiba ya nchi yetu, hawa ni wafanyakazi wa serikali, wanafanya kazi kwa taratibu za kiserikali, wala hawampendelei yeyote, wala hawasaidii chama chochote wao wanafanya wajibu wao.

Mhe. Spika, na kama kuna ushahidi wa upendeleo leteni serikalini, tuone ushahidi huu na huu na huu, wamefanya kosa hili na hili, lazima tujenge hoja ya lile kosa analolifanya, tukifanya jumla jumla tu hivi tukawaelekezea vidole kwamba huyu ana gari aah, kwani wenye gari peke yao nchi hii, wafanyakazi wangapi wa serikali wana magari? Sisi viongozi vile vile hatuna magari sisi, hatuna majumba sisi, maana haya mambo ukimuelekezea mwenzako kidole kimoja, kuna vinne vinakuelekezea wewe.

Mhe. Spika, mimi ninachosema kama wana makosa hawa wapo chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma mtu yeyote ana haki ya kulalamika akawalalamikia akaonesha makosa yao moja, mbili, tatu. Wana viongozi wao hawa, kuna Kamishna wa Tume ya Uchaguzi, kuna Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, kuna makosa waandikieni lizungumzwe na wao wanakutana na wadau hawa mara kwa mara mambo yazungumzwe yajulishwe serikali kosa la huyu, kosa la huyu, lakini tukenda ku-*personalize* mambo tukawa-*attack* watu ambao wao hawafiki humu kujitetea, itakuwa kwa kusema kweli hatutendi haki.

Mhe. Spika, kwa hiyo, naomba kabisa kabisa kunapokuwa na jambo tufuate msingi mzuri. Tunapochanganya siasa na kila kitu maisha nawaambieni tena tutaendelea kuharibikiwa na nchi yetu itarudi nyuma badala ya kwenda mbele.

Mhe. Spika, mimi nataka niwahakikishie kwamba hakuna mtu yeyote atakayekosa haki yake ya kupiga kura, mwenye kutimiza vigezo, kafuata sheria za nchi zilizopo atapiga kura na kama kuna jambo lolote la hoja, basi nafasi zipo za kuzungumza kwa sababu inatolewa nafasi kwa wadau, inatolewa nafasi kwa vyama, inatolewa nafasi kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuzungumza na watu wa Tume wakati wowote wanapohitaji kuzungumza nao na utaratibu huo unawekwa wala si tatizo.

Mhe. Spika, na hakuna sheria zilizotungwa za kibaguzi za kumbagua huyu, huyu asipige kura. Sheria jamani tunazitunga sisi hapa hapa kwenye Baraza hili. Hivyo, mimi niulize tunatunga sheria za kibaguzi hapa? Basi hapa kama tunatunga sheria za kibaguzi, aje mtu alete hoja binafsi aseme kuna sheria hii tumeitunga sisi wabaguzi Baraza la Wawakilishi kuanzia sasa, maana hayo mambo mkiyasema, lazima mjue tuliotunga sheria hizi ni sisi hapa na wengine mmo humu toka 1995. Kwa hiyo, maneno mengine ni ya kuchonganisha, kufitinisha na kugombanisha wananchi na serikali yao si jambo zuri hata kidogo.

Mhe. Spika, mimi nakubali kabisa ushauri wa kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake vizuri ili iweze kuweka hizi kumbukumbu vizuri na katika huo mwaka ambao Tume ya Uchaguzi imepewa fedha nyingi ni mwaka huu,

wametengewa na Mfuko Mkuu bilioni 3 kwa ajili ya shughuli za uchaguzi, ili hayo yote mnayoyasema yaweze kufanikishwa vizuri na uchaguzi uende vizuri wa haki na huru.

Mhe. Spika, unajua tatizo jamani hatusemi kweli, mbona kule Pemba tunapopata majimbo hatulalamiki, lakini kwenye mambo haya kuna kukubali, kwenye ushindani lazima ukubali kushindwa wakati mwengine na kushinda, ikiwa kazi yetu tutakuwa tunagombana tu hayaishi mambo, hatuna tutakapofika.Tuache kugombana na kulalamika tuzungumze mambo ya msingi tujenge hoja jambo fulani lina kasoro tulitatue kwa pamoja, tumo pamoja ndani ya serikali lipo jambo lina kasoro lileteni tulitatue tatizo liko wapi?

Mhe. Spika, tunasema mambo kila siku tunagombanishana wenyewe kwa wenyewe, si jambo zuri kabisa. Tunawarudisha nyuma wananchi wetu, tunavunja moyo mafanikio yaliyopatikana, tunataka sasa kupasua na umoja wetu kwa maneno yetu haya madogo madogo. Madogo yanazaa cheche kubwa. Kwa hiyo, lazima tufike mahala mtu ajue anasema nini, anasema na nani na wakati gani.

Mhe. Spika, sasa kuhusu ugawaji wa majimbo. Mimi nastaajabu kuna watu wanasema wameshajua mpaka majimbo yatakuwa mangapi Pemba. Ugawaji wa majimbo unatokana na Katiba yetu kifungu 120 (3), ndio kinatoa muongozo vipi majimbo yagaiwe. Hakuna mtu mwenye uwezo wa kugawa majimbo bila ya muongozo huu na Katiba hiyo hiyo kifungu 120 (4) kinatoa mamlaka kwa Tume kufanya uchunguzi, baada ya uchunguzi inaweza kubadili idadi ya majina na mipaka ya majimbo ya uchaguzi.

Mhe. Spika, ni Katiba sio mtu na hili halifanyiki utekelezaji wake, lazima unakutana na wadau, wadau wakuu ni sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Vyama vya Siasa na wengine. Kwa hiyo, hakuna jambo linalofanyika bila ya mashauriano. Katiba ndio inakupa nafasi ufanye na kuingia kwetu humu kunatokana na Katiba. Huwezi kutaka lile zuri linalokufurahisha wewe tu, ndio liwe zuri, lazima usimame katika mstari wa usawa na haki.

Mhe. Spika, nchi haiendeshwi kwa matakwa binafsi, nchi inaendeshwa kwa Katiba na sheria, ndio utaratibu wa kuendesha nchi na kama mnaanza muendeshe nchi kwa kila mtu anavyotaka, itakuwa kazi kubwa sana, lakini utaratibu wetu ni Katiba na sheria ndio inayoongoza nchi. Kinyume cha hapo itakuwa ni ulimwengu wa papa huo mdogo kumla mkubwa, mkubwa kumla mdogo.Kwa hiyo, mimi nafikiri ni vizuri kuheshimu Katiba yetu na Katiba iheshimiwe, taratibu za nchi ziheshimiwe, sheria ziliopo ziheshimiwe na kushauriana ni jambo la msingi.

Mhe. Spika, kuhusu uhakiki wa daftari la wapiga kura. Vyama vyote vya siasa vinapewa nafasi ya kuuona uhakiki, kushirikishwa kwenye uhakiki na unakwenda kwa mujibu wa sheria na mara nyingi tunafanya wakati wa uchaguzi unapokaribia. Kwa hiyo, hakuna tatizo kwa chama chochote kutaka kujua hali inavyoendelea, ni jambo jepesi tu tunawasiliana na Tume ya Uchaguzi watakubali kushirikiana, watakubali kutupa kila msaada ili nia yetu ni kufanya uchaguzi mzuri utakaotoa nafasi kwa watu wote.

Mhe. Spika, sasa mtu kuvimba, ukawa na nongwa, ukawa na hamaki, huhamaki katika mambo ya kuongoza nchi. Sisi kutwa hapa huwa tunashambuliwa, tunaambiwa hivi, lakini tunajua wajibu, huwezi ukahamaki. Nchi ina taratibu zake, utahamaki, utahamaki mpaka utapasuka haikusaidii chochote. Utavimba ukivumbuka mwishoni utapata *pressure*, utaanguka, aah! basi. Kwa hivyo, mimi ninafikiri ipo nafasi ya kuwasiliana na Tume kwa wadau kupata undani wa jambo wanalolihitaji.(*Makofi*)

Mhe. Spika, kuhusu fedha za marudio ya uandikishaji wa wapiga kura zinatoka SMZ, wale watazitoa wapi? SMZ ndio inayotoa pesa ili kufanya suala letu la uchaguzi liende vizuri. Baada ya kurudiwa uandikishaji, ni kweli watu mia tatu hawakujitokeza, hawajakatazwa wasijitokeze. Nafasi ipo bado ya kwenda kujiandikisha, tutakaporudia tena suala la kujiandikisha daftari waende, huo ndio utaratibu, lakini taratibu zifuatwe.(*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa upande wa Baraza la Wawakilishi. Kwanza kwa niaba ya Baraza la Wawakilishi kwa kuwa wenyewe watendaji hawafiki hapa, tunapokea pongezi zote ambazo wamepewa Baraza na nimpongeze ndugu zangu Katibu na watendaji wote wa Baraza kwa kutoa huduma vizuri kwa Baraza letu hili, pamoja na kukupongeza wewe kwa uongozi wako mzuri wa busara wenye mashirikiano makubwa tunakushukuru sana.

Mhe. Spika, katika eneo hili limechangiwa kwanza na Kamati yenyewe ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Ali Salum, Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Asha Abdu Haji, Mhe. Raya Suleiman Hamad, Mhe. Bikame Yussuf Hamad na Mhe. Ashura Sharif Ali.

Mhe. Spika, kwanza limezungumzwa sana kuhusu wewe kuhamia katika nyumba yako, mimi ninayajua matatizo ya msingi ya wewe kutokuhamia katika nyumba yako, tatizo kubwa ni la maji, tumefanya jitihada nyingi za maji, kisima kilichochimbwa pale kinachanganyika na maji chumvi. Sasa tunamuhurumia Mhe. Spika wetu kumpeleka akanywa maji chumvi.

Mhe. Spika, kwa hivyo, cha msingi, sasa hivi tunashirikiana na watu wa ZAWA kutafuta namna nyengine ya kupata maji, tatizo mtihani mkubwa ni kupatikana kwa maji, ninaamini tutapopata ufumbuzi wa tatizo la maji, basi Mhe. Spika wetu ataondokana na kadhia hii na atakwenda zake kuhamia nyumba kwake, yeye na ahila yake na ile nyumba ina nafasi ya kutosha kwa Mhe. Spika, haina tatizo. Ahila yote inaingia mule ndani na ina pande mbili. Kuna pande ya kukaa familia na pande ya kukaa mwenyewe Mhe. Spika, akitaka kuagiza anaagiza tu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kuhusu kuweka bango maaluma la majina waanzilishi wa Baraza hili, walipoanza kwenye jengo hili jipya. Ushauri tunaupokea, tutaufanyia kazi kwa kushirikiana na Kamati ya Uongozi.Tutahakikisha tunalifanya haraka iwezekanavyo ili tuweze kuripoti mapema.

Mhe. Spika, Sheria ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi imo kwenye mchakato, mambo yanakwenda vizuri, tayari tumeshakaa na Baraza la Wawakilishi na wahusika wa jambo hili. Ninataka niwahakikishieni jambo hili serikalini wana-*first track*, lipo chini ya Makamu wa Pili wa Rais na muda sio mrefu mutaona matokeo, sheria itakuja hapa ili tulimalize tatizo hili.

Mhe. Spika, kuhusu malipo ya watendaji wa Baraza la Wawakilishi. Muundo tayari na malipo yatalingana kutokana na muundo. Kwa hivyo, nalo hili sio tatizo tena. Kuhusu marejesho kwenye mfuko wa jimbo kwamba wale waliofanya marejesho wapewe fedha za *CDF* za majimbo. Hilo jambo tunalipokea, ni ushauri sahihi tutafanya mara ya bajeti hii, kuanzia Jumatatu na kuendelea huko tutasimamia suala zima la wale ambao marejesho yao, tayari tuanze kufanya malipo ya mfuko wa jimbo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kuhusu kuongezwa kwa mfuko wa jimbo. Ushauri umepokewa. Mara hii bajeti inayofuata hii tunayoanza kama nilivyokwisha kusema kutoka milioni kumi na tano, kwenda milioni ishirini. Kadiri ya uwezo wa serikali utakavyokuwepo, ndivyo ambavyo tutajitahidi kufanya hivyo.

Mhe. Spika, kuhusu ushauri uliotolewa na akinamama (wanawake) nao wapate fedha. Sasa hawa hautokuwa mfuko wa jimbo, maana yake hawana jimbo, wao watakuwa na mfuko wa akinamama kusaidia maendeleo yao, maana kwenye sheria inasema ni mfuko wa jimbo. Kwa hivyo, ninaona ushauri ni mzuri, tutaupokea, tuufanyie kazi vizuri na tutashauriana, halafu basi, bahati nzuri karibuni inakuja sheria yetu ya Utumishi wa Baraza, pengine hata hatujawahi kufika mbali, mambo yakija yatakuwa huku huku tena yanajimaliza wenyewe.

Mhe. Spika, ananihimiza hapa, ananiambia tufanye haraka haraka. Kwa hivyo, nikimbilie haya mengine ya haraka haraka. Kwanza kuhusu *parking* za maturubali. Jamani haya maturubali hayachanika, yametoka uzi kwa upepo mkali, lakini hayajachafua hapo ndani, yanasaidia. Kitakachofanywa tutayashona na yatarudi katika hali yake ya mazingira mazuri ili tuweze kufanyia *parking* ya magari yetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kuhusu kufuta fedha za Kamati Teule, kufuta fedha za safari za nje, kupunguza fedha za *PAC*. Sisi tunaona upo umuhimu wa Kamati hizi kupewa fedha, Lakini Wajumbe wenyewe watakapokuja kuona kwamba haupo umuhimu huo, watatwambia, kwa sababu Mjumbe mmoja hawezi kusemea Wajumbe wote, tutasikiliza tutakavyoambiwa hapa.

Mhe. Spika, lakini niseme tu kuwa safari za nje za Waheshimiwa Wajumbe zinakuza mahusiano na Mabunge mengine na zinatoa taaluma kwa Wajumbe wenyewe, lakini kwa wale ambao hawajapata fursa ya kusafiri kwenda nje ya nchi, ninajua Mhe. Spika na uongozi wake wa Baraza utafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba na Waheshimiwa Wajumbe wanapata nafasi hiyo.(*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa upande wa tatizo la *echo*, tumeanza kulishughulikia. Kuna Kampuni mbili za Kichina hapa, tunazungumza nazo na kama mambo yatakwenda vizuri katika kipindi cha miezi baada ya kumaliza Baraza hili, tutaweka muafaka mzuri. Tumo katika mazungumzo.

Mhe. Spika, kwa nini tofauti kubwa ya bajeti ya mwaka jana na mwaka huu, ni suala la mishahara. Sasa tunakwenda kwenye uhalisia wake. Hivyo, uhalisia huo ndio unavyoonesha na kama kutahitaji nyongeza kwenye mishahara, basi serikali itaongeza. Kwa hivyo, sio tatizo.

Mhe. Spika, kuhusu *Hostel*, tuna mradi wa kujenga *Hostels* na maktaba, michoro tayari na mradi upo, tutafanya kazi hiyo kadiri tutakavyofanikiwa katika kuendeleza mradi huo. Kuhusu ofisi za jimbo kwa sasa kwa kuwa hali bado ngumu kidogo tutashirikiane na Waheshimiwa Wabunge kutumia ofisi zao mpaka pale hali itakapokuwa nzuri.

Mhe. Spika, jengo liwe rafiki kwa walemavu la Baraza la Wawakilishi. Mhe. Raya Suleiman Hamad tumeupokea ushauri wako tutaufanyia kazi ili twende vizuri. Kuhusu utaratibu, nianze na hili la kwanza kwamba kulisemwa hapa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Waziri, Katibu Mkuu, Katibu Fedha tumekula pesa za jimbo. Pesa za mfuko wa jimbo wa Wabunge la Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Spika, sijui tuna matumbo makubwa kiasi gani ya kula fedha za mfuko wa jimbo. Tatizo letu tunachanganya kila kitu na siasa, kwa sababu mimi ninasema serikali, basi mwenye serikali tatu anachukia anasema mimi ninakula fedha, ndicho alichokifanya Ahmed Juma Ngwali kule. Ndugu yangu, mtoto wangu, lakini sawa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, lakini mimi ninachosema fedha zile zilikuwa hazijaingia katika akaunti yetu. Mama Asha Bakari Makame kasema hapa, ziliingia tarehe 7 huu mwezi wa Mei. Mimi nipo Abuja kwenye mkutano wa *World Economic Forum*. Nimeingia tarehe 8, Katibu Mkuu wangu akawapigia Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikaletwa *instruction* ile, maana zile fedha zinakuja na *instruction* ya kila jimbo zilipwe kiasi hichi. Kazi yetu sisi ni kuandika barua tu zikenda, hatuzikugusa, zina akaunti maalum, huna namna ya kuzipata. (*Makofi*)

Mhe. Spika, wala hazijajengewa mnara, mnara unajengwa kwa pesa kwa *ZSSF* na wanazo pesa za kutosha. Hivi sasa wana miradi mengine ya kufanya. Hivi sasa wametenga zaidi ya bilioni hamsini kwa miradi mipya *ZSSF*. Kwa

hivyo, jamani kila jambo tunazuliana zuliana, tukigombana, kugombanisha viongozi, sio jambo zuri hata kidogo. Mimi ninasema hala hala mti na macho na Mhe. Raya jana alisema mukivutana ikikatika munaanguka wote. Kwa hivyo, ndugu zangu si vizuri kushutumiana na kuyasema mambo yaliyokuwa hayana ushahidi wa kutosha. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kuhusu vigezo vya kaya maskini. Nalo hili pia tumeambiwa tumekula pesa, hee! jamani ningekula ingekuwa mambo mazuri mimi sasa hivi. Tunaambiwa viongozi na nini wanakula pesa, kama watu wamekula pesa tuleteeni ushahidi tu tuwashughulikie tu, kwani kuna tatizo gani, lakini vigezo vya kaya maskini hivi nitakavyovieleza.

Mhe. Spika, kwanza unafanywa mkutano wa hadhara katika kila Shehia baada ya kupata yale maoni ya jumla, kwa sababu kwa kutumia *House hold budget survey* inaonesha Shehia gani maskini zaidi. Sasa kwa kuanza kwa mradi huu iliamuliwa Shehia 40 kwa Zanzibar; kwa maana ya Unguja na Pemba. Sasa ikatafutwa Shehia maskini zaidi katika nchi yetu.

Mhe. Spika, mukishapata Shehia maskini zaidi, munafanya mkutano wa Shehia wa hadhara, kwa sababu katika Shehia ni wananchi wenyewe wanaojuana, kwamba Shehia hii na Shehia ndio maskini na ikishajulikana ile Shehia maskini kuna vigezo sasa vinavyofuatwa kwa ajili ya utambuzi katika kila kaya sasa. Kwa hivyo, kwanza mumepata Shehia 40 na katika Shehia 40, Shehia 20 Pemba na Shehia 20 Unguja, hakuna kubaguana.

Mhe. Spika, jambo la kubaguana halifai na hizi zilizokwenda Shehia 20 Pemba zimekwenda kutokana na vigezo vya umaskini na hiyo 20 ya Unguja vimekwenda kwa vigezo vya umaskini, lakini ili kutambua vigezo vya umaskini kwa kaya inatazamwa sasa uwezo wa kaya wa mlo wa siku, kipato cha kaya, makaazi anayokaa, ile nyumba inayokaa ya udongo, ya makuti, ya jiwe, ya tofali. Wategemezi wa kaya, raslimali ulizonazo na haya yakishafanyika kunafanywa tena mkutano katika ile Shehia kwamba basi kaya hizi ndizo maskini zaidi.

Mhe. Spika, kwa hivyo, kwa ushauri wa utaalamu pale na wanajamii wenyewe katika Shehia hiyo, ndio wanapata mapendekezo ya kaya ipi, sasa isaidiwe. Huo ndio unakuwa utaratibu wa awali na baada ya utambuzi wa kujua kaya ipi isaidiwe, sasa hiyo kaya inasaidiwa vipi. Kwa hivyo, kuna kaya zenye masharti ya ruzuku na kuna kaya hazina masharti ya ruzuku.

Mhe. Spika, Kaya zilizokuwa hazina masharti ya ruzuku zinapata elfu kumi na saba kila mwezi miwili. Kaya zenye masharti ya ruzuku zinapata elfu thalathini na nne kila miezi miwili. Sasa wanaopata elfu kumi na sana ni wale ambao hawana vigezo vya ziada. Sasa vigezo vya ziada ni vipi? Ili uwe kwenye ruzuku ya masharti ya upate hiyo thalathini na nne kila miezi miwili.

Mhe. Spika, la kwanza katika nyumba kuwe na mama mjamzito, kukiwa na mama mjamzito, hilo ni sharti la kwanza. Sharti la pili, anayehudhuria *clinic.* Sharti la tatu wanaokwenda kuhudhuria skuli. Kwa hivyo, haya ndio yanakuwa ruzuku ya masharti, unapata thalathini na nne kwa kila miezi miwili, kama huna sifa hizi, unakuwa katika ruzuku haina masharti, unakuwa wewe ni maskini na kwa hivyo, huna sifa hizi unapewa elfu kumi na saba kila miezi miwili.

Mhe. Spika, katika hilo kwenye kila Shehia kuna Kamati ya watu 14 inayosimamia kujua kila kaya itapata kiasi gani na fedha zenyewe zinatoka *headquater* na anajulikana nani na nani anapata. Sasa wewe uliyekuwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais utazila saa ngapi? Sasa kama wapo watendaji huko umefanya utaratibu wowote, twambieni, Lakini kinachofanyika pale zinasimamiwa na watu 14 katika kila Shehia.

Mhe. Spika, kwa hivyo, utekelezaji unakuwa namna hiyo. Hivyo, kwa utaratibu huo, sifikiri kama kuna njia hapo ya kuweza kuzila fedha hizo, maana zinakuwa kwenye *system*, inajulikana kaya ipi na zinakwenda wapi.

Mhe. Spika, sasa Mhe. Hija Hassan Hija jana alisema kuna watu katika jimbo lake hawajapata hizo fedha, mimi taarifa nilizonazo kwamba jumla kama kaya 105 fedha hizo zimefika katika wahusika wote na kama ana ushahidi wowote hazijafika, basi milango ipo wazi kuja kwetu tukaenaye atueleze nani hajapokea, kwa sababu utaratibu unaonesha *very clear* kwamba watu wote ambao walikusudiwa kupewa fedha hizi, watapata fedha hizo.

Mhe. Spika: Mhe. malizia, umeshatumia muda wa saa moja na dakika kumi.

Mhe. Waziri wa Nchi wa Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ngoja nimalizie ili nimpitishe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ijapokuwa bado zipo hoja nyingi, lakini kwa ufupi nitasema kwa wale ambao nimeshindwa kutokana na muda kujibu hoja zao, wachukulie kwamba nia yetu ni njema safi na nia yetu ni kumjibu kila mmoja, lakini muda hauruhusu.

Mhe. Spika, niwaombe itoshe haya maelezo ambayo tumetoa na wale ambao walichangia sana kwenye mambo Mtambuka, kama vile suala la uwanja wa ndege wa Pemba, madawa ya kulevya na *Sober house*, suala la uhifadhi wa mazingira, usafi wa miji, uwezeshaji wananchi kiuchumi, Wakfu na mambo ya mirathi, uhakiki wa mashamba na eka, migogoro ya ardhi, miradi ya *TASAF*, kuhusu suala la ulemavu, kuhusu mambo ya umeme, kuhusu magari ya *fires*, haya wizara zinazohusika wameyasikia na watayaletea majibu ya kina kabisa yatakayokidhi haja zenu.

Mhe. Spika, kwa leo basi kwa sababu ya muda, nimalizie hapa na mimi niseme naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100 na niwaombe Wajumbe wenzangu wote tuipitishe bajeti hii ili mutupe nguvu ya kufanya kwa mwaka huu kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Spika, baada ya hayo, nikushukuru wewe, niwashukuru sana sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili, niwashukuru watendaji wa Baraza la Wawakilishi kwa mashirikiano makubwa wanayotupa na wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi.
Mhe. Spika, ninakutakia wewe heri na ninawatakia Wajumbe wote wa Baraza hili heri na mafanikio makubwa katika maisha yetu na kuitakia Zanzibar na wananchi wake amani, salama na umoja wa nchi yetu.
Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*)
Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri kwa majumuisho hayo. Tumalizie basi kwa eneo hilo la majumuisho kwa kumkaribisha Makamu wa Pili wa Rais. (*Makofi*)

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kuja kumalizia majumuisho ya hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Kwanza nimshukuru sana Mhe. Mohammed Aboud kwa kazi nzuri aliyoifanya, mambo mengi ameyajibu. Kwa hivyo, mimi nitakuwa na machache sana na hasa muda wenyewe tuliokuwa nao ni mfupi kabla ya kwenda swala ya Ijumaa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na uzima, tukakutana hapa leo katika Baraza letu hili tukufu, leo tarehe 23/05/2014, lakini pia, niwashukuru sana wajumbe wote waliochangia hotuba hii. Najua michango yao ilikuwa na nia njema ya kutuongoza ili tuweze kufanyakazi zetu vizuri katika kipindi kinachokuja. Nawahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba katika kipindi kinachokuja, maoni yenu yote nitayazingatia na bila shaka nitafanyakazi kwa uadilifu na mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pamoja na kuwashukuru Wajumbe wote waliopata fursa ya kuchangia hotuba hii, nakuomba kwa ruhusa yako niwatambuwe. Kwanza ni;

1. Mhe. Hamza Hassan Juma; akiwa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi wakuu wa Kitaifa na pia akiwa ni Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura na akiwa pia ni Mwenyekiti wa Wenyeviti.
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali
4. Mhe. Subeit Khamis Faki
5. Mhe. Nassor Salim Ali
6. Mhe. Kazija Khamis Kona
7. Mhe. Omar Ali Shehe
8. Mhe. Asha Bakari Makame
9. Mhe. Ali Salimu Haji
10. Mhe. Mohammed Haji Khalid
11. Mhe. Hija Hassan Hija
12. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
13. Mhe. Asaa Othman Hamad
14. Mhe. Saleh Nassor Juma
15. Mhe. Ali Abdalla Ali
16. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
17. Mhe. Salim Abdalla Hamad
18. Mhe. Fatma Mbarouk Said
19. Mhe. Mussa Ali Hassan
20. Mhe. Hamad Masoud Hamad
21. Mhe. Raya Suleiman Hamad
22. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
23. Mhe. Ashura Sharif Ali
24. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
25. Mhe. Salmin Awadh Salmin
26. Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo
27. Mhe. Waziri wa Afya
28. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa na
29. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed

Hawa wamechangia kwa kusema, lakini pia, wapo waliochangia kwa maandishi ambao ni;

30. Mhe. Salma Mussa Bilal
31. Mhe. Marina Joel Thomas na
32. Mhe. Mahmoud Thabiti Kombo

Tunawashukuru wote kwa michango yao ambayo imetupa faraja sana na bila shaka itasaidia sana katika kufanikisha shughuli zetu kwa kipindi kinachokuja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama nilivyosema mambo mengi yamezungumzwa, lakini mimi niseme juu ya hili suala, niwashukuru sana wachangiaji wote ambao wamezungumzia suala la amani na utulivu wa nchi yetu. Ni kweli kama nilivyosema katika hotuba yangu, amani na utulivu kwa kipindi hiki imetawala sana na ni mategemeo yangu kwamba tutaendelea na amani na utulivu tulionao. Amani hii imekuja kwa sababu ya kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Serikalini tuko na amani kubwa, tunafanyakazi zetu vizuri na tunashirikiana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, lakini tatizo kubwa ambalo tunalipata nilisema hapa wakati nafanya majumuisho mwaka jana, tunapata tabu katika majukwaa ya kisiasa ya mikutano yetu ya hadhara, hapa ndipo pana tabu, tunatukanana katika majukwaa yale. Kwa hivyo, kama amani inavunjika basi ni sisi viongozi ndio wanaovunja amani na sio wananchi wa kawaida.*(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi niwaombe sana viongozi, tuhakikishe sana tunakuwa makini tukiwa kwenye majukwaa yetu ya kisiasa. Mimi ni mmoja wa wale ambao tumeathirika sana na majukwaa ya kisiasa. Nimeitwa majina ya kila aina. Hivi nimuulize rafiki yangu Mhe. Hamad Masoud Hamad, hivi mikutano ya *CUF* hainogi mpaka mtaje jina langu? na hamulitaji kwa wema, mnalitaja kwa ubaya. Sasa haya ndio mambo ambayo yanayowaletea wengine kutaka kuleta hoja binafsi wananchi waulizwe, kama kweli Serikali ya Umoja wa Kitaifa bado inahitajika kwa mambo haya. *(Makofi)*

Kwa nini hatukai kwenye majukwaa yetu tukaeleza sera zetu. Lakini kwenye majukwaa ya kisiasa hasa ya *CUF*, kitoweo ni Balozi Seif Ali Iddi. Balozi Seif Ali Iddi mbaya sana, Balozi Seif Ali Iddi ndiye adui wa nchi yetu. Jamani nimekosa nini? hebu niambiwe hicho nilichokikosa mimi? *(Makofi)*

Sasa mimi naomba sana kama tunataka amani na utulivu wa nchi yetu iendelee, basi tuachane na mambo ya kutukanana kwenye majukwaa ya kisiasa, tuachane kujadili watu, tujadili sera zetu na tuwaelimishe wananchi ndio wanayotaka. Mimi najua wafuasi wa *CUF* wanafurai sana linapotajwa jina langu, lakini sio vizuri. Mnanifanya hata na mimi sasa nikose uvumilivu, husema wakati mwengine maneno ambayo mimi sipendi kuyasema, lakini kwa sababu nyinyi *CUF* ndio mmeanza. Sasa tuwache, kama kweli tunataka tuheshimiane, tuachane na kutaja majina ya watu katika majukwaa ya kisiasa na hasa viongozi. Mnakaa katika majukwaa ya kisiasa mnamtukana Makamu wa Pili wa Rais, mnamtukana Rais ni heshima gani hiyo. *(Makofi)*

Sasa wanasema watu, 'ukimtukana baba wa mwenzio na wako atatukanwa'. Kwa hivyo, tuwache. Ni mategemeo yangu kwamba amani na utulivu wetu vitaendelea katika nchi yetu kwa manufaa ya nchi yetu na kwa manufaa ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Suala la Mhe. Raza limejibiwa vizuri, lakini niseme nikiri kwamba kweli Mhe. Raza alikopesha na mimi nampongeza sana kwa uzalendo wake wa kutaka kuendeleza michezo. Alisema mbele yangu kwamba yuko tayari kukopesha zile pesa 71 milioni kwa ajili ya kulipia gharama za hoteli ambazo walikaa wageni wetu wa michezo kutoka nje. Kwa hivyo, mimi nampongeza sana Mhe. Raza na mimi nakubali kwamba tufanye kila njia Mhe. Raza arudishiwe pesa zake ambazo amezitowa kwa nia safi. Niseme pesa zile hakuniletea mimi kama rafiki yake. Nasikia kuna kauli hii ya kwamba pesa si umekwenda kumpelekea rafiki yako Balozi huko. Mimi hata senti sikuiona ya pesa zile. Kwa hivyo, na kauli hizo za kejeli sio nzuri. *(Makofi)*

Vile vile, yamezungumzwa hapa masuala ya nafasi za Ubalozi kwa Wazanzibari. Kuna wafanyakazi 17 walikwenda kufanya mafunzo katika Chuo cha Kidiplomasia. Nathibitisha kwamba vijana hawa bado watapatiwa ajira katika *Foreign Affairs*. Hivi juzi nilipokuwa Dodoma kwenye Bunge la Katiba nilizungumza na Waziri wa Mambo ya Nje

na amenihakikishia kwamba tatizo hapa ni fedha, nafikiri baada ya kupita bajeti hii vijana hawa nao watachukuliwa kuwa ni sehemu ya *Foreign Affairs*. *(Makofi)*

Mabalozi wa Zanzibar katika balozi zetu, kweli nakubali wako wachache. Lakini haya ndio mambo tunayazungumza kuirekebisha hali hii na nafikiri mambo haya yatatengemaa sana kwa kupitia kwenye Katiba mpya hii ambayo tunaitengeneza. *(Makofi)*

Lakini niseme tu kwamba kila Balozi anapelekwa nchi yoyote, wala hakuna Balozi fulani zimetengwa kwa ajili ya Mabalozi wa Zanzibar, sio kweli. Kila Ubalozi unapokuwa mtupu hauna balozi basi Rais anateuwa Balozi yeyote kumpeleka kwenye kituo kile. Mimi nilikaa Balozi China, lakini nilipoondoka mimi hakupelekwa Mzanzibari, kapelekwa Balozi kutoka Tanzania Bara na baadaye akapelekwa Balozi kutoka Zanzibar, Mhe. Mapuri. Hivyo hivyo na Sweden, alikaa Balozi Ramia pale, lakini baada ya kuondoka yeye hakupelekwa Mzanzibari, kapelekwa mtu mwengine na hivi juzi kapelekwa Mzanzibari tena Mhe. Mzale na hivyo hivyo, hakuna Balozi zilizotengwa kwa ajili ya Wazanzibari, Rais ndiye anapanga Mabalozi katika Balozi zake, lakini idadi ya Mabalozi kutoka Zanzibar sasa tunayazungumza na tutayapatia ufumbuzi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Wajumbe wengi walizungumzia suala la migogoro ya ardhi. Kweli, bado inaendelea kuwepo na tunaosababisha ni baadhi yetu viongozi, tuwache. Mhe. Rais alilizungumzia hili kwamba viongozi tuwache kuingilia masuala haya ya ardhi ambayo yanasababisha migogoro, tuwache sisi viongozi kuwachochea wananchi na kuendeleza migogoro hii sio vizuri. Tuwache kuwachochea wananchi kuwa na migogoro na wawekezaji.

Sisi tunatoka nje kuwatafuta wawekezaji, ili waje kuwekeza nchini mwetu kwa manufaa yetu na kwa manufaa ya wananchi wetu, hawa ni wageni wetu sote wanapokuja hapa na sisi tunafanya kazi hii ya kutafuta wawekezaji, kwa sababu hakuna nchi hata moja ulimwenguni ambayo haina wawekezaji. China inawawekezaji, Marekani ina wawekezaji, kila nchi ina wawekezeaji na ndio maana na sisi tumejitahidi kuleta wawekezaji, ili serikali iongeze pato na vile vile wananchi wetu wapate ajira. *(Makofi)*

Lakini tukianza kuendeleza migogoro hii kati ya wananchi na wawekezaji basi haituletei tija hata kidogo na tunawanyima haki zao wananchi kupata maendeleo na hili nalo ningependa viongozi tujitenge katika kuwachochea wananchi, kwa sababu tu ya tamaa za kisiasa, sio vizuri. Migogoro hii tukiingilia sisi wanasiasa na tukiingilia sisi viongozi basi itaendelea kuwepo na haitamalizika, kwa sababu ni sisi wenyewe tunaichochea. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala la *CDF* alilizungumza Mhe. Mohammed Aboud sina haja ya kulisema tena. Lakini limetupa masikitiko makubwa sana, kwamba watu wanazungumzia kitu hawakielewi, hata ule utaratibu wake hawauelewi. Wamekuja na maneno, pesa hizi zimeliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimejenga mnara, wengine wanasema zimetumiwa katika Sherehe za Mapinduzi na kadhalika. Lakini namshukuru Mhe. Mohammed Aboud amelitolea ufafanuzi vizuri.

Vile vile, kuna suala la kuwa limewaunganisha vipi Wazanzibari katika Bunge la Katiba. Hasa wa kuwaunganisha ni akina nani, wepi wa kuwaunganisha. Tumetoka hapa kama Baraza la Wawakilishi, tunajua maslahi ya Zanzibar kwa kila mmoja muono wake. Humu ndani mimi niliombwa nitowe muongozo wa serikali kuhusu tunapokwenda Bungeni kwenda kutetea maslahi ya Zanzibar. Nilisema wazi kwamba serikali haina muongozo, muongozo ni kwenda kujadili maoni ya wananchi. Kitakachotokea kule ndicho hicho kitakuwa chetu. Lakini kwa upande mwengine usingekuwepo muunganisho huo, kwa sababu hapa tumeondoka vibaya, hapa tumeondoka kila mmoja na msimamo wake.

Kuna watu wameondoka hapa na serikali tatu, wengine wameondoka hapa na serikali mbili, wengine serikali moja na wengine serikali nne, tutawaunganisha vipi watu hao. Ndio tukasema twende tukajadili maoni ya wananchi, kitakachoamuliwe kule ndicho kitakuwa chetu. Sasa leo watu wanasimama hapa wanasema ooh! Mmewaunganisha vipi Wazanzibari kutetea maslahi ya Zanzibar, kwani wewe mwenyewe huyajui? Wewe mwenyewe unayajua kama unaomba serikali tatu unajua maslahi ya Zanzibar yako wapi, kama unaunga mkono serikali mbili unajua maslahi ya Zanzibar yako wapi, twende tukatetee hayo, kila mmoja na muono wake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa turudi mwezi wa nane tukatetee maslahi ya Zanzibar. Maana yake tusikae hapa tukauliza maswali, halafu Bungeni kwenyewe tunakotetea maslahi yenyewe hatuendi, sasa unauliza maswali yatasaidia nini? *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusu masuala ya kukata majimbo. Nafikiri Mhe. Mohammed Aboud amelieleza vizuri. Vile vile, suala la mnara wa Michenzani, Mhe. Mohammed Aboud amelieleza vizuri sina haja ya kulirudia.

Mhe. Spika, pia, nimeulizwa hapa mambo yaliyotekelezwa na ambayo hayajatekelezwa kutokana na maagizo ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kumbukumbu zangu mimi maagizo yote ya Baraza tumeyatekeleza. Kama yapo hayajatekelezwa, basi serikali iandikiwe tuone maagizo gani hayo ambayo hayakutekelezwa na serikali kutoka Baraza la Wawakilishi na sisi tuko tayari kuyafanyia kazi.

Mhe. Spika, sisi utaratibu wetu tunapopata maagizo ya Baraza kwa kupitia Kamati teule, halikaliwi na mtu mmoja tu. Tunakaa kama serikali, kwa sababu ya umuhimu wake tunakaa kama serikali tunachambua, tunasema hili sawa na hili hapana, maana yake sio yote yanayoletwa basi ni sawa tu, serikali itekeleze tu haiwezekani. Kila upande una taratibu zake. Kwa hivyo, yanapokuja maagizo ya Baraza la Wawakilishi kwa kupitia Kamati teule tunayakalia kitako, tunakaa kitako tunayajadili, tunayachambua na baadaye tunaleta majibu. Sasa kama kuna maagizo mengine hayajatekelezwa basi tusingojee Baraza na hii taratibu ya kungojea mpaka Baraza la Wawakilishi ndio tunakuja kuulizwa sio vizuri. Kama kuna maagizo yamechelewa kuletwa basi serikali iandikiwe, ili tusicheleweshe mambo. Lakini kama nilivyosema sikumbuki kama kuna agizo lolote ambalo bado halijatekelezwa na serikali. Inawezekana maagizo hayo hayajatekelezwa kwa mujibu wa Baraza au Kamati teule ilivyotaka, lakini serikali nayo ina muono wake.

Mhe. Spika, jengine lililojitokeza ni suala la wajumbe wa *PAC* kwenda mafunzoni, kweli mimi niliahidi kuwatafutia fursa Wajumbe wa *PAC* kwenda mafunzoni na mimi niliwaandikia Serikali ya India itupatie nafasi hizi, mpaka sasa hivi sijapata jibu, lakini hatua zimechukuliwa na ishaalla baada ya muda si mrefu Wajumbe hawa watakwenda India kwa ajili ya Mafunzo.

Mhe. Spika, leo Ijumaa na wengi wetu wanakwenda Msikitini, tuwahi msikitini kwa sababu leo ni siku tukufu, nimeshukuru kwamba Bajeti yangu inapita kwa siku ya leo Ijumaa. Kwa hivyo, niwaombe Wajumbe wote waipitishe Bajeti hii ili tupate nguvu za kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya wananchi wetu. Kwa sababu muda ni mfupi ni mategemeo yangu kwamba mtaipitisha haraka haraka.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo niwashukuru tena Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa michanganuo mizuri ambayo imetusaidia sana katika utekelezaji wa majukumu yetu katika Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni kwa makofi mengi mliyompigia Makamu wa Pili wa Rais, baada ya kumaliza kufanya majumuisho ambayo yalitanguliwa na majumuisho yaliyosaidiwa na Mheshimiwa Waziri wake wa Nchi. Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa mwaka 2014/2015.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali Hotuba ya Bajeti ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya matumizi, ili kupitisha vifungu vya matumizi vya Wizara ya Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais naomba kutoa hoja

Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, naafiki.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 05 AFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS

Kifungu 0501 Idara ya Uendeshaji na Utumishi - 500,000,000

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mheshimiwa Mwenyekiti sikusudii kuzuia bajeti yangu mwenyewe ambayo nilishirikiana na Mhe. Waziri kuipitisha lakini nilikuwa tu nataka kumuliza Mheshimiwa Waziri, kwa sababu tulikubaliana kwamba kuna mali ya Serikali ambayo ipo chini ya Sherehe na Mapambo na mali ile kuna kodi ambayo inakusanya, lakini kodi ile haingii Serikalini inaingia kwenye mifuko ya watu, sasa tulimpa kazi Mheshimiwa Waziri lakini safari hii bajeti kama ulivyoona kwamba tumechelewa sana kutokana na kuchelewa kwenye Bunge la Katiba.

Kwa hivyo, Kamati yangu haikurudi tena ikaa na Mhe. Waziri Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa sababu katika lile fungu kuna milango ya maduka pale kuna ziro, tukasema inakuwaje hii milango ya maduka inakuwa ziro.

Sasa Mhe. Waziri alituahidi kwamba atawaita wale wahusika ambao wanaoitumia ile milango ili kujua kwamba kwa nini ile kodi wanaichukua wao hawaipeleki Serikalini, sasa ili tuweze kupitisha vizuri fungu hili basi tujiridhishe tu kwamba je, zile fedha kwa mwaka huu zitapatikana na kama hazipatikani Afisi yake itachukua hatua gani ili kuhakikisha kwamba hakuna hata senti moja ya Serikali kuanzia bajeti ya mwaka huu itakayoingia mfukoni kwa mtu? Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti kama nilivyoeleza katika majumuisho yangu lakini kwa bahati mbaya Mheshimiwa Hamza nafikiri alikuwa hayupo, ni kwamba tumewaita wale watu na tumezungumza nao na tukawataka wale wenye vielelezo vya ithibati ya kwamba wao wana uhalali wa kukodisha na kama hawana ithibati hizo basi tukawaambia moja kwa moja kwamba sasa malipo yote ya milango hii yatalipwa serikalini, kwa sababu vielelezo vilivyokuja mpaka sasa havikuturidhisha baada ya kuwaita na kukutana nao kwa hivyo uamuzi wetu ni kwamba wale sasa moja kwa moja wawe na mkataba na Idara hii ya sherehe na maadhimisho na fedha hizo basi zilipwe ili ziweze kutumika katika mfuko mkuu wa Serikali.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri lile agizo la Kamati hakulipuuza na wameweza kulifanyia kazi, sasa lakini bado nilipoangalia hizi kasma fungu kuna ile ile ziro kwa mwaka huu sasa je fedha hizo kama wameambiwa waje wafunge mikataba na Idara fedha zile wakizilipa zitaingia katika kasma gani, kwa sababu ile kasma bado kuna ziro, labda atusaidie maelezo kwa sababu hapa ndipo tunapopitisha fungu makusanyo ambayo hatukuyapitisha hapa na hasa ile kasma wakati kuna ziro maana yake angalau kungekuwa kuna amount fulani mwakani tukaja tukaambiwa imezidi kwa sababu yale malipo pengine yalikuwa zaidi ya yale yaliyokusudiwa.

Sasa kwenye kasma kule mbele bado iko ziro, sasa hili ndio nilikuwa nataka maelezo, kwa sababu kule nikija nikizuia kwenye uendeshaji lile litakuwa katika suala la uendeshaji lakini katika suala la mapato ndio maana nikajaribu kuzuia hapa, sasa nilikuwa nataka tu nijue kwamba je, zile fedha safari hii kama hatujafunga mikataba zitaingia katika kasma gani ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, hebu hiyo kasma unayoizungumzia ni ipi hiyo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, samahani kidogo nipo katika Idara ya maadhimisho wajumbe naomba tusaidiane kidogo, naambiwa kasma 141500.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kwenye kodi hapo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ukurasa wa pili Mhe. Mwenyekiti, Idara ya uendeshaji na utumishi, Idara ya sherehe na Maazimisho kasma 0601 Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya kitaifa itakuwa Mhe. Mwenyekiti hizi kasma sijui tulianza vipi sababu naona tumekwenda mbele lakini kasma ziko nyuma hizi, lakini kasma ambayo niliyokusudia kuiulizia ni kasma 0601, kasma ya 141500 kwenye kodi yaani rate kwamba huku kuna 0 ukodishwaji wa milango ya maduka. Sasa labda Katibu utuongoze kama hii kasma hatujaifikia lakini madhumuni yangu hasa yalikuwepo hapo.

Mhe. Mwenyekiti: Kimsingi ilikuwa hatujafika lakini wacha tumalize maelezo ili tukienda twende moja kwa moja.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hii kasma ipo hapa 141511 ukodishaji wa milango fungu linaonyesha ziro, kitu tunachokifanya tunatoa risiti wakati tukipokea tutawasilisha Wizara ya Fedha halafu tutatizama utaratibu gani unaturuhusu ili sisi kwenye hotuba yetu ya Bajeti ya mwakani tutaripoti tumekusanya kitu hiki. Kwa sababu sasa hivi hatuwezi kubadilisha buku hili tulilokuwa nalo hapa, lakini tunamuhakikishia kwamba tunachokifanya tutatoa risiti na tutawasilisha Wizara ya Fedha na utaratibu utakuja kuwasilishwa wakati tunawasilisha hotuba yetu ya bajeti tulichokifanya.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nadhani wajumbe wangu wa Kamati wanamsikia Mhe. Waziri, kwa sababu hii kasma tulikubaliana kwa pamoja na kama tulivyosema Wizara haikupuuza imelifanyia kazi, kwa hivyo naomba tu watendaji wa Idara hii katika bajeti inayokuja tuje tuone fungu hili ni namna gani limeondoka katika ziro likaja katika kile ambacho chochote kitakachopatikana. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 0501 Idara ya Uendeshaji na Utumishi - 5,000,000
Kifungu 0601 Idara ya Sherehe na maadhimisho ya Kitaifa-3,000,000

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedaly: Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii katika kasma hii ya 611 Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kushukuru na kupata afueni kubwa kifungu hichi baada ya majibu ya kwanza aliyotoa Mhe. Waziri ambayo kidogo mimi na familia yangu yalinipa tabu, lakini nichukue nafasi hii kumshukuru Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kiongozi wa Serikali kwa kuthibitisha kwamba deni hili Serikali ilikopa na ilikubali na italipa, nachukua nafasi hii kupitisha hoja zote na kumshukuru kwa dhati kabisa Makamo wa Pili wa Rais kunisafisha mimi jina langu na familia yangu katika mgongo huu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili ya Rais: Mhe. Mwenyekiti, ningependa kidogo kurekebisha maneno ya ndugu yangu Mheshimiwa Raza, sio Serikali italipa Mheshimiwa Raza, anajua aliowakopesha sisi tutakachokifanya kama ni Serikali nimemuahidi hapa na nasema kwa mara ya pili, tutalisimamia hili jambo kwa

utaratibu ule ule wa wale waliokopeshwa kwa utaratibu ule ule basi hizi fedha zitalipwa kwa utaratibu ule. Serikali hapa utamlipa kwa pesa za nani katika serikali kwa idhini ipi maana lazima aelewe Serikali haiwezi kutoa deni hili lakini utaratibu utafanyika na fedha zake kama alivyoahidiwa atalipwa ndio zitakavyofanywa zilipwe sharti aelewe hapo Mhe. Raza, akisema Serikali kuna tatizo lake Serikali utatoa kwenye fungu lipi.

Kifungu 0601Idara ya Sherehe na maadhimisho ya Kitaifa - 3,000,000
Kifungu 0801 Idara ya Upigaji Chapa na Mpigaji Chapa Mkuu wa Serikali- 600,000,000
Jumla ya Fungu - 608,000,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 05 AFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Kifungu 003 Afisi Kuu Pemba - 388,964,000
Kifungu 0401 Idara ya Mipango Sheria na Utafiti-

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nazungumzia kasma 220302 safari za nje, naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais pale alipojibu hoja yangu ya safari za nje na kimsingi sikukusudia kwamba kuhoji safari ya Mhe. Makamu wa pili, nimekuja kuhoji utaratibu wa safari za Serikali na kwa vile Serikali walikiri tokea bajeti kuu kwamba matumizi ya gharama za Serikali kwa safari yanakuwa makubwa, nikahoji kwamba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alienda nje hoja ambayo sina wasi wasi nayo, lakini nilichotaka kujua kulikuwa na uhalali gani safari ile kwenda zaidi ya watu 20 au 30 na vipi walitumia fedha kwa kiasi gani?

Lakini Mhe. Waziri alipojibu alionyesha kama kwamba sisi Wawakilishi hatuna haja ya kuomba mchanganuo na akatoa mfano kwamba hata wawakilishi wanasafiri.

Mimi nasema kwamba wawakilishi kama wanasafiri na hakuna mchanganuo ni kosa vile vile, kama Waziri anasafiri na mchanganuo hakuna ni kosa, kama Serikali inasafiri na hakuna mchanganuo ni kosa, sisi kazi yetu hapa ni kusimamia matumizi ya fedha za umma ikiwa ni pamoja na safari za Wawakilishi, Mawaziri na Wabunge na watu wengine. Kwa hivyo, si sahihi majibu ya Mhe. Waziri, kuonesha kwamba kwa vile hawatoi mchanganuo mimi mwaka jana nilikwenda Mauritius kama Afisi yangu haikutoa mchanganuo ni kosa.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba unijibu suala langu kulikuwa na uhalali gani wa kuwachukua safari ile zaidi ya wajumbe 25 na kutumia gharama ile ambayo anayotaja, mimi sikwenda safari ile lakini waliokwenda ndio walitwambia kwamba walitumia fedha zile, mimi sikwenda wala sikuwa na haja ya kutia wasiwasi wa safari ya Makamu wa Pili, sina wasiwasi nayo ninachohoji kama mwakilishi, kulikuwa kuna haja gani ya kusafiri watu kiasi kile na matunda yake ni yepi?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, sasa Mhe. Hija ameuliza swali lake vizuri na kwa msingi huo hapo nimemuelewa. Waliokwenda katika ziara ile Mheshimiwa ni pamoja na wafanyabiashara. Wale Watendaji wa Serikali walilipiwa na Serikali. Lakini wale wafanyabiashara 16 walijitolea wenyewe, walijilipia wenyewe, tiketi zao wenyewe, gharama zao wenyewe wao walitaka fursa ya kufuatana na Makamu wa Pili wa Rais, ili kupata namna ya kuwasiliana na wafanyabiashara wenzao wa Marekani, kwa nia ya kuanzisha biashara wao na Marekani. Na walifikia makubaliano kwamba *chamber* ya Zanzibar na *chamber* ya Siato ziwe na ushirikiano kuanzia hapo waweze kuendeleza mahusiano ya kibiashara katika pande mbili hizo na ndio maana wakaja huku.

Kwa hivyo, wale wafanyakazi wa serikali walikwenda kwa mujibu wa taratibu zote za kiserikali.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, ninafikiri hayo ndio majibu ya serikali sio kuwazuia Wawakilishi wasihoji fedha za umma, hayo ndio majibu sahihi ya Mhe. Waziri na naunga mkono majibu hayo.

Kifungu 0401

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Spika, Ahsante sana katika mchango wangu wa maandishi pia niligusia kwa Mhe. Waziri hii safari sasa ninachokiomba kwa Mhe. Waziri kama ataweza kutoa maelezo kwamba ikihojiwa kama hivi isiwe ndio mwisho wa kufuatana na wafanyabiashara. Hao wafanyabiashara Mhe. Makamu wa Rais alifatana nao na Mawaziri pia wanapokwenda kwenye ziara kama hizo wafatane na wafanyabiashara hao ili iweze kuleta maendeleo ya biashara kwa biashara huko wanakokwenda wakakutana na kuweza kutuletea maendeleo katika nchi yetu. Kwa sababu ziara zile huwa na tija na manufaa ya kuongeza hata kipato na kodi katika nchi yetu kwa kuleta wawekezaji kutoka nje.

Kwa hivyo, suala kama hili lisiwatie hofu, ninaomba Mhe. Waziri atoe kauli kwamba hilo jambo litaendelea. Ahsante Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru Mhe. Mahmoud lakini nataka nimuhakikishie kuwa huo ndio utaratibu wa serikali. Nia yetu si tu kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, lakini hata ziara za Mawaziri zinapogusa masuala ya shughuli za kibiashara na shughuli za kuendeleza Zanzibar kwa maana ya miradi mbali mbali, ikiwemo shughuli za kilimo, uwekezaji na kadhalika, basi nataka nimuhakikishie kwamba tutaendelea kufanya hivyo na hatuvunjiki moyo ni wajibu wetu akiuliza swali Mhe. Hija alitaka ufafanuzi na ninamshukuru kwa namna alivyolipokea na kulikubalia.

Pale mwanzo niseme nilimuelewa vyengine lakini baada ya maelezo yake nimeelewa sawasawa na ndio maana nikajibu sawasawa. Sisi ni binaadamu unaweza kupitikiwa. Lakini nataka nimuhakikishie kwamba tunakubaliana na maelezo ya Mhe. Mahmoud na nataka kumuhakikishia kwamba hakuna sababu ya serikali kurudi nyuma, ni utaratibu wa kawaida uliomo ndani ya serikali. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti-	184,007,400
Kifungu 0501	Idara ya Uendeshaji na Utumishi-	704,166,316
Kifungu 0601	Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa-	871,615,500
Kifungu 0701	Idara ya Huduma za Makamu wa Pili wa Rais-	483,116,224
Kifungu 0801	Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali-	482,000,600
Kifungu 0901	Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ-	348,638,000
Kifungu 2001	Idara ya Maafa-	

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilisema kwamba nielezwe kwa nini katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014 Serikali ilitakiwa kuchangia jumla ya shilingi milioni 70 katika shughuli za maendeleo na kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Serikali imetakiwa kuchangia jumla shilingi za Tanzania milioni arubaini ambayo ni asilimia iliyokuwa haizidi 54 ya awamu iliyopita. Wakati shughuli zinaendelea na Idara ya Maafa ina kazi kubwa sana, ni vigezo vilivyotumika mpaka katika awamu iliyopita ikawa ni milioni sabini halafu na awamu hii ni milioni arubaini.

Hiyo ni (a) na (b), nilitaka kujua kwa upande wa washirika wa maendeleo walitakiwa kuchangia shilingi milioni mia mbili na sabini katika kipindi cha 2013/14 lakini 2014/2015 ni bilioni moja milioni mia mbili na thamanini na mbili elfu mia nane na thamanini ambao ni asilimia 475. Hivi kwa Idara kama hii muhimu na mambo ya maafa kutegemea wafadhili kwa kiasi kikubwa chote hicho na ukiacha serikali kuchangia ni kwa sababu Idara haina umuhimu au vipi?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Salim Abdalla Hamad kwa mapenzi yake makubwa kwa Idara hii ya Maafa na ninajua kwa nini anafanya hivyo kwa sababu anaona namna ya watendaji wanavyotekeleza wajibu wao. Nilieleza hapa nilipofanya majumuisho lakini napenda nirudie tena. Vigezo tulofanya mara hii tupate milioni arubaini ni uwezo halisi wa bajeti yetu. Hata hiyo mwaka jana tulipoweka milioni 70 nilisema tulipata milioni kumi tu. Sasa tumeweka arubaini Mungu ajaalie tuzipate hizo arubaini. Kwa hivyo hii ilitokana na hali halisi ya uwezo wetu wa kibajeti ndio maana tukenda pale, tungependa ziwe nyingi zaidi hali hairuhusu.

Kuhusu washirika wa maendeleo tunashukuru kwamba sasa wameongeza msaada wao kwetu baada ya kujenga hoja kufanya nao kazi pamoja tukafanya tathmini ya mahitaji yetu, wameona katika suala zima la kukabiliana na maafa na kujitayarisha kwa maafa basi waanze kutusaidia hii 1.3 *billion*, mimi nataka niwashukuru sana *UNDP* na *UNICEF* na napenda wajumbe wenzangu waendelee kuwashukuru wafadhili hawa waliokusudia kutusaidia kwa ajili ya kujitayarisha kupambana na maafa katika nchi yetu.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 2001	Idara ya Maafa-	298,447,800
Kifungu 2003	Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ , Dar-es-Salaam-	

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, Ahsante, nilipokuwa nikichangia jana nilimuomba Mhe. Waziri atusaidie mambo mawili. Kwanza Idara hii kuangaliwa katika suala la usafiri. Halafu pili, bajeti iliyokuwa imepangwa kwenye Wizara hii ilikuwa ni ndogo sana na pafanyike utaratibu wa namna yoyote ile ili fungu hili liweze kuongezeka kwa mujibu wa taratibu ya Kiwizara na sikupata jawabu ambalo lilikuwa limeniridhisha katika hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti hata mimi naona kwamba bajeti hii ni ndogo. Kwanza anisamehe kwamba sikuweza kumjibu kutokana na muda Mheshimiwa na naelewa. Lakini hata mimi mwenyewe na Wizara tungependa wapate zaidi, lakini tatizo la *ceiling* yetu tuliyopata hiyo ndio hali halisi. Ni kweli kuna tatizo la usafiri na sisi tungependa usafiri uwepo hata mimi napata shida sana ya kupanda gari taxi ama kutafuta gari za *private* si jambo zuri hata kidogo tungepanda hizo gari, gari hizo hizo tuzitumie. Tutakachokifanya tutajitahidi katika hivyo hivyo vifungu vyetu vidogo vidogo kuzitengeneza zile gari ambazo zipo ziweze kusaidia Ofisi yetu ya Dar-es-Salaam.

Ni kweli bajeti ndogo lakini sasa ndio *ceiling* yenyewe tuliyopata, nimesema bajeti ya mara hii tumepata upungufu wa asilimia 40 ukilinganisha na bajeti ya mwaka jana katika ofisi yetu. Tatizo liko hapa. Naomba Mhe. Mahmoud anivumilie na tutajitahidi, maana utakapopunguza pengine ndio utaua zaidi. Hii ni baada yakuangalia uwezekano.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, lakini waliangalie kwa umakini zaidi.

Kifungu 2013 Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dar-es-Salaam- 353,178,160

Jumla ya Fungu - 4,110,200,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 16 BARAZA LA WAWAKILISHI

Kifungu 0201 Utawala Unguja-

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia jana nilizungumza kwamba katika Baraza la Wawakilishi, bajeti ya mwaka 2013/14 ilikuwa bilioni 14,852,000,000. Lakini 2014/15 ni bilioni 14,564,000,000 hapa kuna tofauti ya milioni 288,000,000 na nikamuomba Waziri atakapokuja hapa atuambie kwa sababu shughuli za Baraza kila mwaka ni zile zile. Lakini kuna tofauti kubwa hii ya mwaka jana na mwaka unaokuja, atufafanulie tu ni kitu gani kinapunguzwa, kitu gani kimetolewa hadi kufikia tofauti hii.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nilisema lakini nafikiri Mhe. Hamad hakunielewa vizuri, lakini naomba nitoe ufafanuzi, ili rafiki yangu, ndugu yangu, Hamad Masoud aweze kuelewa. Kilichotokea Mheshimiwa ni kwamba mwaka jana kweli fungu hilo lilikuwa kubwa limetokana na mishahara. Lakini fedha hizo hazikutumika kwa sababu tulikuwa bado hatujakamilisha utaratibu wa muundo na muundo ndio utaonekana kufanya yale matumizi ya mishahara.

Sasa kutokana na hali hiyo fedha zile za ziada zilitakiwa kwa ajili ya kulipa watendaji wetu haikuwezekana na zikabidi zirudi. Mara hii baada ya kupata muundo tumefanya hesabu halisia, kutokana na hesabu halisia tukapata kiwango hiki. *In case* ikitokea hazikutosha kwa masuala ya mishahara, basi tutakwenda Wizara ya Fedha tuwaambie kwamba hazikutosha, lakini kwa sasa kwa mujibu wa ule muundo uhalisia wake ni ule na fedha hizo zinaonekana zitatosha tuweze kufanya shughuli zetu. Ni kwa sababu ya mshahara si kwa sababu ya fungu jengine lolote Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Mwenyekiti, waziri anapoeleza hivyo kwamba bajeti ya 2013/2014 haiwezekani kama kulikuwa na makisio ilikuwa tu tuweke hizi, walipofanya uhalisi 2014/15 wakakuta ni hii, sasa mimi ninapojiuliza hivyo kweli Baraza la Wawakilishi wataalam wote watu wa bajeti wote hawa, mwaka jana unatupa kitu ambacho huna hakika nacho na sisi tukakubali hapa kwamba tukipitishe kwa kukuamini, inakuwaje ni umakini au kutokuwa makini katika hili. Labda Waziri angenambia tu ilikuwaje mwaka jana akatutaka tutoe pesa ambazo hana hakika nazo kumbe bajeti yenyewe haina uhakika. Je, mwaka huu tuna uhakika gani kama mwaka jana hakuwa na uhakika mpaka kukawa na *difference* hii ya milioni 288,000,000.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ninamshukuru kwanza Mhe. Hamad ni kwamba mwaka jana tulidhani kile tulichokifikiria ndani ya Baraza, mishahara hii ingekuja na kiwango hiki. Lakini baada ya mazungumzo na wenzetu huko Utumishi wakaukubali ule muundo baada ya kwisha kushauriana muundo wenyewe sasa ndio ukatupa *reflection* hii. Tuliyoyataka sisi ilikuwa tupate mapato yale, mishahara ile, lakini baada ya taratibu zilizopo za kisheria na kitaalam na mazungumzo ndio tukaja na muundo ambao umekubalika.

Sasa muundo uliokubalika uhalisia wake ni kiwango hiki na siku hizi tunatumia kutokana na *activity* yenyewe, sasa huo ndio uhalisia. Mwaka jana tulidhani hiyo mishahara niliyokadiria ingekuwa mikubwa kuliko hata kupita kile kiwango cha muundo ambacho sasa kimekubalika. Huo ndio ukweli halisi.

Sasa pengine tungekubalika kwenye kiwango kile na tusingeomba fedha maana yake tusingekuwa na cha kulipa, lakini tuliweka akiba hiyo kwa kudhani mazungumzo yanaendelea kungekubalika kwa vile tulivyotarajia.Lakini hatukupata vile, tumepata tulichopata na sisi wenyewe tunaamini kwamba kilichopatikana ni sahihi na kitaleta ufanisi mzuri katika Baraza kwa hivyo tunashukuru yaliyotokea. Ni hayo tu hakuna zaidi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninafikiri Waziri angekiri tu kwamba mwaka jana walituletea jambo la kukisia ambalo hawakuwa na hakika nalo kakiri hivyo. Na kwa hivyo Baraza hili lilipitisha bajeti ile kwa makisio ya mambo ambayo Waziri wenyewe hakuwa na hakika nayo.

Mhe. Spika: Labda kuna jambo moja dogo unajua unapokuwa jambo linakuhusu inakuwa tabu sana sasa lakini kimsingi ni kwamba fedha hii hiyo iliyopungua hiyo ni fedha ambayo ilikuwa imewekwa pale muundo uliopitishwa na Kamisheni ya Utumishi wa Umma fedha ile ilikuwa imewekwa ili iweze kukidhi mahitaji ya malipo kwa ajili ya watumishi. Kilichopo ni kwamba miundo ndani ya serikali imepitishwa mingi lakini amri ya malipo kwa miundo hiyo bado.

Sasa fedha hii kwa kuwa miundo hiyo bado itakuwa ipo katika Kamisheni ya Utumishi miundo itakapokuwa tayari na hizo zitakuja kuingia moja kwa moja, ndio namna yenyewe, bahati nzuri jambo hili na mimi nilishiriki kikamilifu na nilihoji sana kwa nini pesa hizo zitoke. Ikawa kwa sababu ndani ya serikali nzima amri ya kulipa miundo mipya bado. Kwa hivyo, ile pesa ikabidi uhalisia wake sasa isitumike mpaka pale amri itakapotoka kwa miundo yote.

Kifungu 0201

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia Baraza la Wawakilishi niliwaomba Wawakilishi wenzangu wanistahmilie na nilitoa hoja ambayo Mhe. Waziri ametetea, lakini sijakubaliana nayo. Nimeomba kwamba fedha zote za safari za nje za Wawakilishi, fedha zote za Kamati Teule za Baraza hili na fedha za ziada za *PAC* ziondoshwe. Nilikuwa na maana ifuatayo:-

Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, pamoja na sababu zote ambazo umeziaeleza, fedha hizi milioni 288,000,000 ambazo ziliachwa mwaka jana Kamati yetu ya Bajeti ilitenga kwa ajili ya nyongeza za wafanyakazi wa Baraza la Wawakilishi na sisi Wawakilishi pamoja na Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi kuidhinisha matumizi haya, lakini tulishindwa kuwatetea wafanyakazi wetu nyongeza haikuongezwa. Lakini safari za nje Wawakilishi walitetea na tukenda wengi sana. Niliomba hapa orodha ya Wawakilishi waliosafiri, ikiwa ni pamoja na Hija Hassan Hija nilienda Mauritius.

Mhe. Spika, safari hizi hazina tija, leo waambie Wawakilishi wetu watuletee ripoti moja tu ya safari waliyokwenda kwa matumizi ya fedha za umma inashindikana, lakini kwa safari Kamati Teule na *PAC* kumalizwa fedha hiyo Wawakilishi wanatetea, lakini shilingi milioni 284 za wafanyakazi wetu ambazo ndizo zitawafanya waongeze ujuzi wa maslahi zilishindikana kwa sababu ya vikwazo vya Tume ya Utumishi Serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima zote naomba Kasma 211110 shilingi 3.3 bilioni posho maalum liangaliwe liwahusu wale tu viongozi wa Baraza na wale tu watendaji wa Baraza ambao ni wataalamu wetu wapewe. Kasma ya posho maalum kwa ajili ya viongozi wa Baraza kwa maana ya Kamati za Baraza, Kamati Teule na wengine ziondoshwe.

Kasma ya pili 211116 Posho ya Kamati, shilingi 4.5 bilioni, ikiwa kuna pesa kwa ajili ya Kamati Teule ziondoshwe. Safari za nje Kasma 220302 shilingi 155 milioni ziondoshwe, pamoja na matumizi ya hoteli kwa safari hizo za nje.

Kwa nini, kwa sababu bajeti yoyote lazima tuangalie *value for money*, *efficiency* na *assertiveness* ya bajeti. Hapa haipo na ipunguzwe badala yake fedha hizi ziende kwenye utawala kwa maana ya kutengeneza majengo ya Baraza tuondoshe *echo*, jengo litengenezwe na tuwe na Baraza ambalo *echo* hamna, jengo zuri ili watumishi wetu waweze kufanya ufanisi mzuri. Hiyo ndio hoja yangu Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kama maelezo yangu ya awali nilivyosema kumjibu Mhe. Hija Hassan Hija ni kwamba, sisi katika serikali tunaona umuhimu wa fungu hilo kwa maana ya fedha za safari za nje, fedha za Kamati Teule, fedha za *PAC* tunaziona zina umuhimu, lakini ikiwa wenyewe Wajumbe wa Baraza hili wanaona hazina umuhimu sisi tunasikiliza maamuzi tu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, wenyewe fedha hizi ni nani? Hizi fedha si za Wajumbe, fedha hizi ni za umma hazina wenyewe, wenyewe ni wananchi. Hoja zangu hazikuleta ufanisi, *value for money* haipo, niambiwe leo ripoti moja tu ya Kamati za safari ya nje, mnatupeleka nje kujifunza nini? Sasa wenyewe nani, wenyewe sio Wawakilishi 50 wenyewe Wazanzibari kutoka Unguja mpaka Pemba. Hoja yangu tupunguze badala yake majengo ya Baraza na *echo* iondoshwe na wafanyakazi wetu wapate maslahi.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo letu wafanyakazi wetu tunashindwa kuwatetea kwa sababu sisi hatuna wasiwasi, laiti Wawakilishi wangenyimwa haki zao wangetetea, sasa zipunguzwe haki hizi ili kesho kutwa tuwatetee wafanyakazi wetu wapate maslahi yao. Wafanyakazi waliyoongezwa 20,000 tu zikashindikana Wawakilishi wanatanua nje, haiwezekani tupunguze fedha hizi kama kweli tuko tayari kuwatetea Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti: Kuna Mheshimiwa anataka kuongeza maneno hapo?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake ambayo yalikuwa *very clear* katika kutoa ufafanuzi wa jambo hili. Lakini la pili, ni kweli kabisa kifungu hiki anachokisema yeye cha safari za nje na kamati mbali mbali za Baraza ni tofauti kabisa na kifungu cha mshahara. Nimemuelewa ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija, kwamba anachotaka kifungu hiki pengine kihaulishwe. Sasa utaratibu wa kuondosha fungu hapa ni jukumu letu sisi kama Baraza la Wawakilishi kwa utaratibu wa sheria na kanuni ziliopo. Kama tunahisi kwamba tuliondoshe turudi kwenye utaratibu wa kawaida wa Baraza tuamue, la kwanza.

Lakini la pili, ni Baraza la Wawakilishi hili hili ambalo lilifanya safari India, Ghana na Uganda na wakarudi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tukenda mpaka shambani kujadili taarifa zile, na hii ndio iliyozaa suala la kuwa na Mswada wa Sheria ya Utawala wa Baraza la Wawakilishi. Sheria hiyo hiyo tunahimizwa sisi serikali tuhakikishe hiyo sheria inakuja Barazani na inapitishwa ili shughuli za utawala wa Baraza zitekelezeke. Sasa Mheshimiwa Mwakilishi, anaposema kwamba safari za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hazina faida yoyote labda Mhe. Hija Hassan Hija akumbuke hata maneno yake ambayo amesema kwenye vikao vilivyopita.

Mhe. Mwenyekiti, sisi kama serikali na kama alivyosema Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tunahisi safari za kikazi za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Kamati za Baraza la Wawakilishi kufanya kazi zake na wakaja na ripoti wakatushauri serikali, huo ndio utaratibu wa kawaida wa kuendesha dola. Sasa kama yeye anaona kwamba halina maana ni jukumu lako turudi katika utaratibu sisi Baraza tuamue kama hizi hazina maana basi tutaamua na kama zina maana tutaamua. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hija Hassan Hija, hebu tukae, tukae maana sasa mnanipa shida. Kuna Waheshimiwa Wajumbe kuhusiana na safari za nje wananiambia basi Mzee hebu hii *passport* yangu angalau kaipige muhuri tu ionekane kwamba imetumika. Kwa maana Waheshimiwa Wajumbe wengine hawajapata nafasi za safari. Ninadaiwa hivyo na ninazingatia safari hizo zifanyike ili iwe na faida na kupata ile tunayoiita *exposure* ya Wajumbe kwa kushirikiana na Mabunge mengine. Leo ukiniambia hizi tuziondoe sasa hata huo muhuri labda tukusanye *passport* turejeshe kule. Hilo moja.

La pili, masuala ya Kamati Teule inaweza kuibuka kwa mujibu wa haja na hoja, tukiziondoa sasa haja na hoja hiyo tutaifanyaje? Mimi nadhani tuzingatie haya mambo kwa sababu mambo haya yote yamo ndani ya kanuni, yamo ndani ya taratibu zetu kwamba lazima tuyafanye. Hivyo, Waheshimiwa Wajumbe, itapokuja wakati fulani kuna hoja ya kuunda Kamati Teule pesa nizitoe wapi? Katibu utapata wapi pesa, Waheshimiwa tuendelee.

Suala la wafanyakazi linazingatiwa sana, tulichokubaliana na serikali na mimi nilikuwepo bahati nzuri na Makamu wa Pili tulikuwa pamoja, Waziri wa Fedha pamoja na Katibu ni kwamba muundo utapokubalika sasa ulipe kwa serikali nzima, Mfuko Mkuu utafanya kazi hiyo. Sasa hilo jambo linazingatiwa.

Hata Kamati ya *PAC* ambayo kazi zake zimezidi Mhe. Omar Ali Shehe naye anadai na kweli kazi zipo nyingi, tukakubaliana kwamba pale itapofikia pahala kwamba kamati hiyo sasa ile shughuli yenyewe inakuja basi tuzungumze na Waziri wa Fedha ili atupatie pesa. Si hilo tu, lakini hata ule mradi ambao *UNDP* wanatusaidia kwa kawaida wanatupa pesa kidogo sana, kuna pesa nyengine Katibu huwa tunamwambia hebu ongeza kidogo hapa, tukaambiwa inapotokea haja kwamba kuna semina ambayo ina umuhimu mkubwa sana basi tuione serikali ili jambo hilo litendeke. Haya tuliyafanya hivyo ili kwa ufanisi wa shuguli zetu zote, *PAC*, Kamati Teule na nyenginezo.

Mhe. Hija Hassan Hija nakuomba sasa ubaki hivyo hivyo tuendelee.

Kifungu 0201 Utawala Unguja-		11,916,708,000
Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba	-	2,647,292,000
Jumla ya Fungu-		**14,564,000,000**

(Vifungu vilivyotaja hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 30 - TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Mwenyekiti, wasiwasi unaanza kutuingia, mimi nilikuwa sijamaliza, sijaridhika ukanambia nikae, Mhe. Hija Hassan Hija, hajaridhika umemwambia akae. Sasa kama ni hivyo bora tusichangie tena sisi, kwa sababu hapa ni kuridhishana, Mjumbe ana hoja aridhike sasa unapommaliza kabla yeye hajamaliza inakuwa ni mtihani.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kama una hoja tuletee.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Hoja yangu ni hiyo. Mimi nilipokuwa nachangia Tume ya Uchaguzi nilizungumza mengi na wenzangu wakazungumza mengi, lakini katika hili nataka yafuatayo waziri atufafanulie. Nilizungumzia marejeo…

Mhe. Mwenyekiti: Samahani kidogo, makatibu hapa wanasema hatujaingia kwenye fungu lolote la kasma yoyote. Kwa hivyo, katibu tuendelee halafu tena nitakuita.

Kifungu 0201 Utawala Unguja-		1,129,800,000

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nilizungumzia kuhusu marejeo ya majimbo matano katika uandikishaji na nikahoji ni kiasi gani kilitumika kwa marejeo yale na fedha hizi zilipatikana wapi, kwa sababu hazikuwemo kwenye bajeti. Lakini vile vile, nikasema huu ni uzembe wa seketarieti, haiwezekani data hizo kwa sababu umeme umezimwa kwa hivyo ikawa ni sababu tena hizo *data* kwamba nazo zimekwenda. Hivyo, kweli hakuna vitu vya ku-*save* vitu muhimu kama hivyo?

Kwa hivyo, nikasema kwamba uzembe huu ambao hauvumiliki uliogharimu fedha, uliogharimu muda wa watu wengine, uliokosesha hata watu wengine kuandikishwa, hawa waliofanya uzembe huu ni hatua gani imechukuliwa? Waziri hajajibu amesifu tu Tume ya Uchaguzi nzuri wapongezwe, hayo mimi hayakuniridhisha nataka aniridhishe katika hili.

Lakini la pili, nikasema uhakiki wa daftari amenyamaza kimya. Wadau wa uchaguzi wana haki ya kujiridhisha vyama vyote vitakavyoshiriki. Tunataka uhakiki wa daftari sisi wengine tunaliona daftari ni chafu, mna *double registration*, mna mambo chungu nzima. Sasa hili kama hatukuridhika huo uchaguzi wa haki na huru uko wapi, waziri hili vile vile nalo alijibu. Kwa leo ni hayo mawili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru ndugu yangu Mhe. Hamad Masoud Hamad kwa maelezo yake ya ziada nakumbuka nilieleza wakati nafanya majumuisho, lakini napenda nirudie tena.

Aliniuliza jana, alitaka kujua marudio ya uandikishaji fedha zimelipwa na nani? Nikamwambia fedha zimelipwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, sikumbuki kabisa kama jana aliniuliza ni kiasi gani cha fedha zilitakiwa. Lakini sasa hivi ananiuliza na kiasi cha fedha. Sasa kiasi cha fedha kwa hapa sina nitamletea kwa maandishi sina hiyo idadi ya kiasi gani cha fedha.

Mhe. Mwenyekiti, tunapofanya kazi sisi ni binadamu wakati mwengine yanatokea mapungufu ya kibinadamu, wakati mwengine yanatokea mapungufu ya kimashine, kompyuta na kadhalika, wakati mwengine yanatokea matatizo ya umeme katika utendaji wa kazi ukasababisha kasoro kwenye hiyo mitambo ya kufanyia kazi. Kwa hivyo, hapo yanapotokea shughuli hazikwenda vizuri huwezi tu kulaumu moja kwa moja, matatizo yanatokea ya kibinadamu, yametokea, utaratibu ukafanywa wa kurudia uandikishaji, waliokuja wamekuja, waliokuwa hawakujitokeza ndio hawakujitokeza tuliporudia maana ni hiari ya mtu. Sasa tunasema bado uandikishaji utarudiwa tena utakaporudiwa wende wakajiandikishe ni haki yao hakuna tatizo, watakaotimiza sifa kwa mujibu wa sheria.

Lakini la pili, uhakiki wa daftari nililieleza sana Mheshimiwa, ni kweli wadau wana haki ya kujiridhisha na kila linapofanyika wadau huulizwa na kukaribishwa. Hata hivi sasa wadau wakitaka ni kuiandikia tu Tume watawaambia muda muwafaka wa kuonana nao wakafanya uhakiki. Ni kweli umuhimu wa kuhakikiwa na kujiridhisha wadau upo na Tume haikatai kufanya jambo hilo. Kwa hivyo, wakati wowote Mhe. Hamad Masoud Hamad au vyama vyengine vinataka kujiridhisha ni kuwaandikia Tume watawaambia muda wao, lakini itakapofika karibu na uchaguzi kazi hiyo itafanywa na wakitaka hivi sasa ifanyike wawaandikie Tume watakuwa tayari kuwasikiliza hawana matatizo nao, muhimu waifuate taratibu na maamuzi ya Tume ndio yenye maelekezo ya mwisho kuhusu jambo hili.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Mwenyekiti, wakati waziri alipokuwa anajibu aliyaacha mengi na sasa hivi ananambia nimemuuliza hili sikumuuliza hili. Mimi niko pale pale na *hansard* zipo ni kiasi gani kilitumika anasema atanipa kwa maandishi, basi hiki kifungu tusubiri mpaka maandishi yaje, ndio maana yake.

Lakini kama hilo halitoshi, kuhusu uhakiki wa daftari sisi tushawaandikia Tume na mpaka leo hakuna jawabu. Tume hii iko chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, waziri atuthibitishie hapa kwamba uhakiki utafanyika wa daftari. Tume hawajatujibu mpaka leo, azungumze vitu ambavyo viko hewani, waziri atuthibitishie kwamba uhakiki wa daftari utafanyika kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 na wadau wote wanaotaka kushiriki watashiriki.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni utaratibu kwa mujibu wa sheria daftari huhakikiwa na wadau na namhakikishia hilo litafanyika wala halina pingamizi yoyote. Hata hivi sasa kama wamewaandikia Tume basi Tume kwa mujibu wa sheria watatafakari kama wanaona umuhimu wa kuonana hivi sasa, Tume watalitafakari hilo jambo, watakapoona inafaa kwa mujibu wa sheria watawakaribisha, lakini namhakikishia kwamba daftari litafanyiwa uhakiki na wadau wote husika ili tufanye uchaguzi wetu ukiwa huru na wa haki hauna matatizo yoyote.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri anasema kwamba uhakiki utafanyika, tunataka tuendelee.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Mwenyekiti, hizi fedha hazikuidhinishwa na Baraza hili yeye anasema zimepatikana serikalini, hivi ni kiasi gani? Na huko serikalini zilitoka wapi? Kwa sababu serikali nayo ina bajeti ati, si ndio sisi tunaopitisha, haikuwa shilingi 2,000 zile kama mtu ametoa mfukoni au shilingi 71 milioni kama alivyotoa Mhe. Mohamedraza Hassanali, ni bajeti ya majimbo matano na kila jimbo siku tatu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, Bajeti ya Tume ya Uchaguzi tumepitisha hapa na huko nyuma ilipitishwa. Na zile zinazotoka Mfuko Mkuu vile vile zimetangazwa rasmi, hata mara hii tumeseme ziko shilingi bilioni tatu zitatumika kwa ajili ya uchaguzi. Nasema tena kwamba nilikuwa sina ile *figure* kamili lakini bahati nzuri imefika hapa ni milioni kumi na nne na laki tatu zilizotumika kwa kazi hiyo kutoka hii bajeti iliyomalizika.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, katika kuchangia nilichangia kuhusu Tume hii ya Uchaguzi na nilichangia kwa vifungu vya Katiba vilivyopo, katika Katiba hii vifungu 119 kifungu kidogo cha 12,13 na 14 ili nifahamike naomba kusoma hiki kifungu kidogo cha 14 kama ifuatavyo kwa ruhusa yako.

Mhe. Mwenyekiti: Naomba usome kwa kifupi sana muda hatuna.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Katika utekelezaji wa madaraka yake kwa mujibu wa Katiba hii Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar itashauriana mara kwa mara na Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano. Sasa Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano inapofanya *Registration* ya wapiga kura Wazanzibari takribani wote wenye sifa kwa umri ukiacha sifa nyengine wanachukuwa mbali na wale ambao si wapiga kura ya Zanzibar.

Lakini Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ina kundi kubwa la watu liliwaacha wenye umri mkubwa na waliokwisha piga kura huko nyuma kwa sababu tu ya kukosa vyeti vya kuzaliwa. Nilimuomba Mhe. Waziri hili suala atupe ufafanuzi kwa sababu siku za nyuma alisema kuwa suala hili litatafutiwa ufumbuzi. Je, msimamo ni upi kama wanashauri na Tume ya Uchaguzi wa Muungano mbona wao wanafanya vizuri wala hakuna malalamiko, lakini sisi tunawaachia watu bila ya kupata haki yao?

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Tume ya Uchaguzi wa Taifa ina Sheria yake inaongoza, Tume ya Uchaguzi Zanzibar ina Sheria inaongozwa na Katiba imefafanua namna ya utaratibu wa kufanya shughuli zake za Tume ya Uchaguzi Zanzibar. Sasa utaratibu wetu upo *very clear* kwenye masuala ya Uchaguzi. Kama nilivyosema Mhe. Mwenyekiti, hakuna nchi inayoongozwa bila ya Katiba na Sheria, cha msingi ni kuheshimu Sheria yenyewe. Kama kunaonekana kuna upungufu wa Sheria basi ni kuyaonesha hayo mapungufu yako wapi na hata hoja binafsi inakubalika kuletwa kuonesha mapungu yako wapi ya Sheria.

Lakini hivi sasa tuulize hapa walio wengi Sheria hii mapungufu yake yako wapi? Tupige kura hapa tuulize. Kwa sababu wengine wanasema ina mapungufu, wengine wanasema haina mapungufu. Sasa kama kuna mapungufu tuko tayari kuyarejebisha. Lakini Sheria Mhe. Mwenyekiti, iko *very clear* na lazima tuheshimu na si nchi yetu inayoongozwa kwa mujibu wa Sheria sio mtu kwa matakwa ya mtu binafsi anavyotaka yeye, hilo ni tatizo Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hiyo, mimi naona kwamba utaratibu upo wa kisheria na watu hakuna wanaokatazwa kupiga kura, Sheria inaruhusu kupiga kura watu hawakatazwi kupata vitambulisho vya Mzanzibari. Sheria inaruhusu kupata kitambulisho cha Mtanzania na kama mtu hajapata haki yake uko utaratibu wa Kimahakama wa kwenda Mahakamani kudai haki yake ya msingi mtu kupata haki zao.

Sioni sababu kukaa tu na kushindana mambo madogo madogo bure kuchanganya wananchi wetu kusema maneno mengine yaliokuwa si sahihi halafu ndio kama hivyo mtu anaambiwa twende ukajiandikishe hajitokezi na kadhalika. Kwa sababu mambo mengine nafikiri Mhe. Mwenyekiti, tufate taratibu tuheshimu Sheria nchi yetu itulie na tusibadilishe maneno.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na maelezo mazuri ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Lakini Mhe. Mwenyekiti, Katiba inasema kuwa kila Mzanzibari aliefikia umri wa miaka 18 na kuendelea anayo haki ya kupiga kura na kuna mambo ambayo yanamsitisha kupiga kura na moja katika hiyo ni kushindwa kutoa kitambulisho kuhusu umri wake au kitambulisho cha kupiga kura na mambo mengine. Siwezi kuyajua yote kwa moyo wale watu tayari wanavyo vipande vya kupigia kura ambavyo Katiba hii ilikuwa iko na ni Serikali hii hii ikatokezea hivi juu juu kwa kila aliekuwa hana cheti za kuzaliwa asipige kura.

Sasa kulikuwa na sababu gani mwanzo wakapiga kura halafu tena wakazuiliwa wakati katika Katiba haikuelezwa kuwa ni lazima awe na cheti cha kuzaliwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Salim Abdalla Hamad, hizi hoja unapandishia hizi. Hoja ya kwanza ilikuwa umenukuu kitabu hapo cha Hotuba kwamba kutakuwa na mashirikiano ya mara kwa mara na ukataka kujua kwa nini kwa upande wa Tume ya Jamhuri kumekuwa hakuna malalamiko na kwa upande wa Zanzibari kuna malalamiko. Ukatoa maelezo Mheshimiwa ambayo umesema unakubaliana nae ndio neno uliotoa.

Sasa umekuja na hoja nyengine juu ya hoja hii wakati Mhe. Hamad Masoud tayari ameshakula hoja mbili. Utaratibu wetu kila kifungu ni hoja tatu, sasa nadhani hiyo sasa kama alivyosamehe Mhe. Hamad Masoud pale na wewe usamehe.

Jumla ya Kifungu 002001 Utawala Unguja - 1,129,800,000

Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba- 184,300,000

Jumla ya Fungu **1,314,100,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 05 - OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Kifungu 1901 Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ- 2,560,000,000
Kifungu 2001 Idara ya Maafa 1,322,880,000
Jumla ya Fungu- **3,882,880,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 16 - BARAZA LA WAWAKILISHI

Kifungu 0201 Utawala Unguja 710,615,000

Jumla ya Fungu **710,615,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 30- TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR

Kifungu 0201 Utawala Unguja- 1,750,000,000

Jumla ya Fungu- **1,750,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

BARAZA LILIRUDIA

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko yoyote sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu liyakubali makadirio hayo. Naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wale waliokataa, waliokubali wameshida. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nikushukuruni tena kwa mashirikiano ambayo tumeonesha katika shughuli zetu na hatimae tukaweza kupitisha Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Niwaombe tu kwamba kuhoji mafungu ni jambo na utaratibu wa kawaida na Waheshimiwa wana haki ya kupata majibu kutokana na hoja hizo.

Nashukuru Waheshimiwa Mawaziri wamejitahidi hivyo, maelezo wamejitahidi mapema pengine mengine yalikuwa ni kwa sababu ya muda ambao kwa makubaliano katika vikao vyetu vya awali tulisema kwamba tujitahidi kubana muda kwa sababu muda wa mkutano huu mzima kwa kiasi fulani umepungua.

Kwa hiyo, kwanza niombe radhi kwa sababu inabidi tuchunge muda kiasi hicho lakini hatimae tuone kwamba shughuli zetu tunazifanya kwa ufanisi kwa muda huu huu ambao tumejipangia.

Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni kwa mashirikiano makubwa na sasa tusitishe shughuli zetu hadi saa 11:00 jioni ambapo Mhe. Naibu Spika, atakuwa anaendelea na shughuli ambayo itakuwepo kwa wakati huo. Ahsanteni sana.

(Saa 5:52 Mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015- Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa likae kama Kamati ya matumizi ili liweze kupokea, kuzingatia, kujadili, kuchangia na hatimae liweze kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima wa afya na kutuwezesha kukutana katika Baraza hili kwa lengo la kujadili mambo muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, napenda kutoa shukurani za dhati kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa hekima na busara zake za kuiongoza nchi yetu katika hali ya usalama na amani. Napenda pia kutoa shukurani zangu za dhati kwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad, kwa kuweza kusimamia vyema majukumu yake. Aidha, napenda kumshukuru Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa usimamizi na maelekezo yake ya kiutendaji wa shughuli za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, nachukua fursa hii pia kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe binafsi na wasaidizi wako kwa kuliongoza Baraza hili kwa umakini mkubwa, jambo ambalo linapelekea utulivu na ufanisi wa Baraza hili katika kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Naibu Spika, napenda pia kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inayoongozwa na Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, kwa mashirikiano na miongozo wanayotupatia. Pia, naishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Hesabu za Serikali chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Omar Ali Shehe, Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Chake Chake kwa mashirikiano mema na Ofisi yetu.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi, kwa kunipa ushirikiano na ushauri tukiwa ndani na nje ya Baraza. Ushirikiano wao huo umechangia kwa kiasi kikubwa kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa uadilifu na ufanisi kadri Mwenyezi Mungu alivyonijaalia.

MALENGO MAKUU YA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ina jukumu la kuratibu masuala ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi, Watu wenye Ulemavu, Udhibiti wa Dawa za Kulevya na muitiko wa kitaifa wa kupambana na janga la UKIMWI. Katika kutimiza jukumu hili, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imekuwa na malengo makuu yafuatayo:-

1. Kuratibu na kusimamia shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais.
2. Kuratibu Sera na Utafiti unaohusiana na maeneo ya majukumu ya OMKR.
3. Kuimarisha mazingira ya kazi na maslahi ya wafanyakazi.
4. Kusimamia mabadiliko ya tabianchi.
5. Kuimarisha usimamizi wa mazingira na matumizi endelevu ya maliasili.
6. Kuimarisha na kutetea uzingatiaji wa haki na fursa sawa kwa Watu wenye Ulemavu ndani ya jamii.
7. Kuratibu na kudhibiti usafirishaji, uingizwaji, matumizi na biashara haramu ya dawa za kulevya.
8. Kuratibu muitiko wa kitaifa wa kupambana na UKIMWI.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inatekeleza majukumu yake kupitia Taasisi zifuatazo:-

1. Ofisi ya Faragha
2. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
3. Idara ya Uendeshaji na Utumishi

4. Idara ya Mazingira
5. Idara ya Watu wenye Ulemavu
6. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba
7. Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya
8. Tume ya UKIMWI.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA 2013/14

OFISI YA FARAGHA

Mhe. Spika, Ofisi ya Faragha ina jukumu la kutoa huduma na kuratibu shughuli zote zinazofanywa na Makamu wa Kwanza wa Rais.

Kwa mwaka wa fedha 2013/14 Ofisi ya Faragha ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kusimamia na kuratibu shughuli zote za Makamu wa Kwanza wa Rais.
2. Kuimarisha utoaji wa huduma kwa Makamu wa Kwanza wa Rais.
3. Kuimarisha mazingira ya kazi katika kuleta ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2014, Ofisi ya Faragha imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyojipangia:-

Mhe. Naibu Spika, shughuli mbalimbali za Makamu wa Kwanza wa Rais zimeratibiwa ikiwa ni pamoja na kuwasaidia fedha taslim wananchi, jumuiya na vikundi 25, madrasa na misikiti 13 na wananchi 62 (Wanawake 28, Wanaume 34). Vile vile wageni kutoka nje ya nchi na wananchi kadhaa wa Unguja na Pemba walipata fursa ya kuonana na Makamu wa Kwanza kwa lengo la kupatiwa ushauri na maelekezo juu ya mambo mbalimbali yanayowakabili.

Mhe. Naibu Spika, jumla ya kalenda 800 za mwaka 2014 zimechapishwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali. Mkutano mmoja wa mahojiano na waandishi wa habari umefanyika na kuelezea utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na kuzungumzia maendeleo ya ujumla ya Zanzibar.

Aidha, vipindi maalum 5 vya Makamu wa Kwanza wa Rais vimetayarishwa, kati ya hivyo 1 ni maalumu kwa ajili ya maadhimisho ya miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar, vile vile makala 6 zinazohusiana na masuala ya mazingira, siasa na uchumi zimetayarishwa na kuchapishwa katika gazeti la Zanzibar Leo. Ziara mbalimbali za kikazi ndani ya nchi zilifanyika na ripoti za ziara hizo zimewasilishwa sehemu husika kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Faragha kwa mwaka wa Fedha 2013/14 imekadiria kutumia TZS 515,150,000/= kwa kuendeshea kazi. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2014 ilikwishaingiziwa TZS 133,846,075/= sawa na asilimia 26. (Angalia kiambatanisho namba 1)

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Naibu Spika, Idara hii ina jukumu la kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera na mipango ya maendeleo, kutunza takwimu, kuratibu shughuli za utafiti pamoja na kufuatilia na kutathmini utekelezaji kwa taasisi zote zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kujenga uwezo wa watendaji na kufanya tafiti mbili kwa mujibu wa mpango mkuu wa utafiti wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais unavyoelekeza.
2. Kusimamia na kutekeleza mambo mtambuka yanayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.
3. Kuratibu, kusimamia na kutekeleza mipango ya kazi na ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.
4. Kuimarisha mazingira ya kazi na kuwajengea uwezo wafanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2014 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyojipangia:-

Mhe. Naibu Spika, utafiti wa kubaini upatikanaji wa huduma kwa Watu wenye Ulemavu zikiwemo huduma za Afya, sheria na elimu umefanyika. Vile vile, utafiti uliangalia miundombinu iliopo kwa watu wenye ulemavu na masuala ya fursa za uwezeshaji na ajira. Matokeo ya utafiti huo yametumika katika kuandaa Sera ya Maendeleo ya Watu wenye Ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imekamilisha rasimu ya kwanza ya Sera ya Maendeleo ya Watu wenye Ulemavu. Rasimu hiyo iliandaliwa kwa kuwashirikisha wadau kutoka sekta za binafsi, za Serikali na watu mbali mbali miongoni mwao wakiwemo watu wenye ulemavu kutoka Unguja na Pemba. Kukamilika kwa Sera

hii kutaiwezesha Ofisi yetu pamoja na wadau wengine kusimamia vyema na kutetea haki na fursa kwa watu wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, taarifa mbali mbali za utekelezaji za robo mwaka na za mwaka zimeandaliwa na kuwasilishwa sehemu husika ikiwemo Tume ya Mipango, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Wizara ya Fedha na taasisi nyengine kila inapohitajika.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iliratibu na kutekeleza miradi 2 ya maendeleo kwa fedha za Serikali na miradi 2 kwa fedha za Wadau wa Maendeleo kama ifuatavyo:-

Mradi wa Elimu ya Mazingira

Mhe. Naibu Spika**,** Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za SMZ. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14 mradi huu umetekeleza yafuatayo:-

- Semina 2 kwa shehia 10 (6 Unguja na 4 Pemba) na vikundi 10 vya polisi jamii kutoka kila shehia zimefanyika.
- Vipindi vinne vya Redio vya Maliasili zisizorejesheka, mifuko ya plastiki, mabadiliko ya tabianchi na usimamizi wa taka viliandaliwa na kurushwa hewani kupitia *ZBC* na *Zenji FM Radio.*
- *Slogan* mbili za *TV* za Maliasili zisizorejesheka na mifuko ya plastiki zimerushwa hewani pamoja na kununua vifaa vya usafi kwa ajili ya kampeni za usafi.

Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia kwa Watumiaji wa Dawa za Kulevya

Mhe. Naibu Spika, mradi huu nao unatekelezwa kwa fedha za SMZ. Katika kipindi cha utekelezaji cha 2013/14, mradi huu ulipangiwa kujenga uzio ili kulizuia eneo hilo na uvamizi. Kazi ya ujenzi wa uzio kwa ajili ya kituo hicho umeanza huko katika eneo la Kidimni. Kabla ya kuanza kwa kazi hiyo, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilifanya hatua zote za taratibu za manunuzi kama sheria inavyoelekeza.

Mradi wa Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

Mhe. Naibu Spika, mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Wadau wa Maendeleo *(UNDP)* kupitia program ya *UNDAP*. Mradi huu unatekelezwa kupitia malengo saba ambapo malengo manne kati ya hayo yanatekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Malengo hayo ni kama ifuatavyo:-

i. Kuhakikisha masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi yanaingizwa katika mipango ya maendeleo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa MKUZA II.
ii. Kutayarisha Mkakati wa Zanzibar wa Kukabiliana na Mabadiliko ya tabianchi na kusaidia utekelezaji wake.
iii. Kuimarisha muundo wa kitaasisi kwa ajili ya kusimamia masuala ya mabadiliko ya tabianchi.
iv. Kukuza kiwango cha upatikanaji wa taarifa na uelewa juu ya athari za mabadiliko na mikakati ya kukabiliana nayo miongoni mwa jamii na taasisi za Serikali.

Malengo mengine matatu ya mradi huu yanatekelezwa kupitia Wizara ya Fedha, Wizara ya Kilimo na Maliasili na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Aidha, jumuiya ya *CODECOZ* nayo inashiriki katika kutekeleza mradi huu kupitia lengo moja la kukuza kiwango cha upatikanaji wa taarifa na uelewa juu ya athari za mabadiliko na mikakati ya kukabiliana nayo miongoni mwa jamii na Taasisi za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, kupitia malengo manne ya mradi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imetekeleza yafuatayo:-

- Nakala 500 za muongozo wa uzingatiaji wa masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi zimeandaliwa na kuchapishwa pamoja na kuwafundisha Wakurugenzi wa Mipango, Sera na Utafiti, Maofisa Wakuu wa Mipango wa Wizara zote pamoja na Wawakilishi kutoka Jumuiya za Kiraia.
- Nakala 500 za muongozo wa kufanyia upembuzi (*screening*) miradi na mipango ya sekta zimechapishwa. Muongozo huo utatumika ili kuhakikisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi yanazingatiwa kwenye mipango na miradi mbali mbali ya maendeleo.
- Mkakati wa Mabadiliko ya tabianchi umeandaliwa na tayari umepitishwa na Baraza la Mapinduzi. Mkakati huo unatoa miongozo ya namna ya kuweza kuhimili na kujikinga na athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo mbali mbali.
- Muongozo wa kutoa mafunzo/elimu juu ya mabadiliko ya tabianchi umetayarishwa; muongozo huo utatumika katika kuwafundishia jamii na kuhakikisha kwamba wamepata taarifa sahihi zinazohusiana na mabadiliko ya tabianchi.
- Mkakati wa Mawasiliano na Utetezi wa mabadiliko ya tabianchi umeandaliwa, mkakati huu umetoa muelekeo wa taarifa zinazohitajika na wadau mbali mbali na namna ya kuziwasilisha taarifa hizo kwa wadau katika ngazi tofauti.

Mradi wa kujenga uwezo

Mhe. Naibu Spika, mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Wadau wa Maendeleo na unaratibiwa na Tume ya Mipango. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia mradi huu kwa mwaka wa fedha 2013/14 ilipanga kutayarisha Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini. Kutokana na kuchelewa kuingia kwa fedha za utekelezaji, hadi kufikia Machi, Ofisi ilianza taratibu za manunuzi ili kuweza kumpata mtaalamu wa kufanya kazi hiyo kama inavyoelekezwa katika sheria ya manunuzi. Mtaalamu huyo tayari amepatikana na ameanza kazi katika awamu ya kwanza ambayo inatarajiwa kukamilika mwezi wa Agosti.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ilikadiriwa kutumia TZS 160,065,000/= kwa kuendeshea kazi na TZS 150,000,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa fedha za Serikali. Hadi kufikia Machi, 2014 Idara ilikwishaingiziwa TZS 43,587,483/= sawa na asilimia 27 kwa kuendeshea kazi na TZS 120,000,000/= sawa na asilimia 80 kwa kazi za maendeleo. (Tafadhali Rejea Kiambatanisho namba 1)

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Naibu Spika, Idara hii ina jukumu la kusimamia shughuli za kila siku za uendeshaji na utumishi zikiwemo sheria na kanuni za utumishi, mafunzo, maslahi na maendeleo ya wafanyakazi.

Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ilipanga kutekeleza yafuatayo:-

1. Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi.
2. Kukuza na kuimarisha mawasiliano ya habari.
3. Kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuwapatia maslahi.
4. Kusimamia utaratibu wa matumizi ya fedha kwa mujibu wa sheria na kanuni za fedha zilizopo.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2014 Idara imeweza kutekeleza yafuatayo katika mambo iliyojipangia:-

Mhe. Naibu Spika, vifaa mbali mbali kwa matumizi ya Ofisi na vitendea kazi, kama vile vifaa vya kuandikia, vifaa vya usafi na kompyuta, mafuta na vilainishi, malipo ya umeme, mtandao na huduma nyenginezo kwa kuimarisha mazingira ya utendaji kazi zimefanyika. Safari 18 za ndani (PBA, DAR, DOM) za kikazi na 7 za nje (Marekani, Poland, Mauritius, Sychelles, Afrika ya Kusini, Malawi na Austria) zimegharamiwa. Safari hizi zimeongeza mahusiano mema na washirika wa maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, programu 5 na makala 2 zenye maudhui mbali mbali ziliandaliwa na kutolewa kupitia vyombo mbali mbali vya habari. Lengo la programu hizi ni kutoa taarifa kwa wananchi kuhusiana na mambo yanayotekelezwa kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Miongoni mwa programu zilizorushwa hewani ni filamu ya maadhimisho ya miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar inayohusu majukumu, mafanikio, changamoto na muelekeo wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. (Angalia Kiambatanisho namba 2)

Aidha, kupitia fedha za misaada ya kijamii zinazotolewa na Mhe. Waziri, Skuli ya Sekondari ya Biashara - Mombasa, Kikundi cha Kipwida cha Maungani na Skuli ya Maandalizi ya Kiislam ya Magomeni vimepatiwa msaada wa fedha taslim ili kuvisaidia katika shughuli zao za kujiendeleza.

Mhe. Naibu Spika, wafanyakazi wawili walinzi wamelipwa posho la baada ya saa za kazi, huduma za viburudishaji kwa wageni na vikao rasmi zimetolewa. Wafanyakazi wanane (wanawake 2 na wanaume 6) waajiriwa wapya wamepatiwa mafunzo ya *Orientation* katika Chuo Cha Utumishi wa Umma. Wafanyakazi 7 (mwanamke 1 na wanaume 6) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na 20 (wanawake 10 na wanaume 10) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya cheti, diploma, shahada ya kwanza na ya pili katika fani mbali mbali. (Angalia Kiambatanisho namba 3)

Mhe. Naibu Spika, mpango wa manunuzi (*Procurement Plan*) wa vifaa mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais umetayarishwa na kuratibiwa ipasavyo kwa kufuata taratibu za manunuzi. Vikao vya Kamati Tendaji vimefanyika na viwili vya Kamati ya Uongozi vilifanyika na kujadili mambo mbali mbali kama miongozo ya kazi inavyoelekeza. Kupitia vikao hivyo, watendaji wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais walipata nafasi ya kupeana maelekezo na kubadilishana uzoefu wa majukumu yao.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 imekadiria kutumia jumla ya TZS 292,827,000/= kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2014, Idara ilikwishaingiziwa TZS 157,648,182/= sawa na asilimia 54. (Rejea Kiambatanisho namba 1)

IDARA YA MAZINGIRA

Mhe. Naibu Spika, Idara hii ina jukumu la kukusanya na kuhifadhi taarifa za kimazingira, kutoa taarifa za kimazingira ili ziweze kusaidia katika kutayarisha na kutekeleza mipango na miradi ya maendeleo, kufuatilia mwenendo wa hali ya kimazingira, kukabiliana na matatizo ya kimazingira, kuhamasisha wadau kuchukua hatua za kuhifadhi mazingira pamoja na kutoa elimu ya mazingira kwa jamii.

Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Mazingira ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuimarisha usimamizi wa udhibiti wa uchafuzi wa mazingira.
2. Kuimarisha usimamizi endelevu wa maliasili.
3. Kuimarisha na kusimamia utekelezaji wa Mikakati, Sera, Sheria na

Kanuni.

4. Kukuza uelewa wa elimu ya mazingira kwa jamii na wadau wengine wa Mazingira.
5. Kusimamia uingizwaji wa masuala ya mazingira katika miradi ya maendeleo.
6. Kuimarisha mazingira ya kazi na maslahi ya wafanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2014 Idara imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyojipangia:-
Mhe. Naibu Spika, operesheni 115 (75 UNG, 40 PBA) za mifuko ya plastiki kwa ajili ya kudhibiti uchafuzi wa mazingira zimefanyika na watu 18 (3 UNG 15 PBA) wamekamatwa na kuhukumiwa kwa faini ya jumla ya shilingi 3,290,000/=. Mifuko yenye uzito wa kilo 978 imekamatwa na imeangamizwa. Vile vile, operesheni 26 zinazohusu uchukuaji ovyo wa maliasili zisizorejesheka zimefanyika. Wahusika wamefikishwa katika vyombo husika na kupigwa faini ya fedha taslim na kuonywa. (Angalia Kiambatanisho namba 4: Operesheni za maliasili zisizorejesheka).
Mhe. Naibu Spika, mapitio ya Sheria ya Mazingira yamefanyika kwa kuwashirikisha wadau mbali mbali. Miongoni mwao ni Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.
Aidha, rasimu ya Mswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira hivi karibuni imewasilishwa kwenye kikao cha Kamati ya Makatibu Wakuu. Michango iliyotolewa na Wajumbe wa kamati hiyo inaendelea kufanyiwa kazi.
Mhe. Naibu Spika, kwa ajili ya kukuza uelewa wa elimu ya mazingira, jumla ya vipindi 6 vya redio na vipindi 6 vya *TV* vimerushwa kupitia *ZBC* redio na *TV*, *slogan* 2 za Redio na *Slogan* 2 za TV zimetayarishwa, semina ya MKUHUMI kwa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Maofisa Tawala wa Mikoa, Wilaya, Madiwani na Masheha wa maeneo yenye misitu ya hifadhi ya jamii imefanyika.
Mhe. Naibu Spika, jumla ya miradi 20 imefanyiwa ufuatiliaji na kutolewa ushauri wa kimazingira na miradi 17 imepewa vyeti vya tathmini ya athari za kimazingira na hivyo kutakiwa kuanza kazi za utekezaji.
Mhe. Naibu Spika, Idara imeshiriki katika mikutano na makongamano katika ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Ushiriki huo umesaidia katika kuleta maelewano zaidi na washirika wa maendeleo na wataalamu mbali mbali pamoja na kuona fursa zilizopo.
Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mazingira kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ilikadiriwa kutumia TZS 127,884,000/kwa kuendeshea kazi, hadi kufikia Machi 2014 ilikwishaingiziwa TZS 55,750,570/= sawa na asilimia 44 (Rejea Kiambatanisho namba 1)
Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi cha mwaka 2013/14 OMKR ilikadiriwa kukusanya TZS 10, 500,000/- kupitia Idara ya Mazingira. Fedha hizi zinatokana na ada ya hifadhi ya mazingira ikiwa ni pamoja na vyeti vya Mazingira. Kazi ambayo inategemea idadi ya miradi inayowasilishwa kutoka *ZIPA* au miradi ya maendeleo ambayo inastahili kufanyiwa tathmini. Hadi kufikia Machi 2014, jumla ya TZS 5, 418,000/= ambazo ni sawa na asilimia 52 ya lengo zilikusanywa.

IDARA YA WATU WENYE ULEMAVU

Mhe. Naibu Spika, Idara hii ina jukumu la kuratibu, kusimamia na kufuatilia masuala mbali mbali yanayohusu Watu wenye Ulemavu ili kuhakikisha ujumuishwaji katika shughuli zote za kimaendeleo zikiwemo za kiuchumi na kijamii.
Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Watu wenye Ulemavu ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi.
2. Kutengeneza mfumo wa takwimu (*data base*) za Watu wenye Ulemavu.
3. Kusimamia haki, fursa sawa na ujumuishwaji wa Watu wenye Ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2014, Idara ya Watu wenye Ulemavu imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyopanga:
Mhe. Naibu Spika, vikao vitatu vya Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu vilifanyika na kujadili taarifa mbali mbali zinazohusiana na maendeleo na changamoto zinazowakabili watu wenye ulemavu. Vile vile, vikao viwili vya Maafisa Waratibu wa masuala ya Watu wenye Ulemavu vilifanyika, kupitia vikao hivi utekelezaji wa masuala ya watu wenye ulemavu wa sekta mbalimbali ulijadiliwa. Jumuiya sita za Watu wenye Ulemavu zimepatiwa Ruzuku ya TZS 1,800,000/= kila mmoja. (JUWAUZA, CHAVIZA, ZACDID, UWZ, ZANAB na SOZ) ili kuzisaidia jumuiya hizo katika kutekeleza majukumu yake. .
Mhe. Naibu Spika, kama inavyoeleweka kwamba, kila mwaka tarehe 3 Disemba huwa ni siku ya Kimataifa ya Watu wenye Ulemavu Duniani. Kwa upande wa Zanzibar, maadhimisho ya siku hiyo yalifanyika Dole, Wilaya ya Magharibi Unguja ambapo ujumbe wa mwaka 2013 ni "*Ondoa vikwazo, weka fursa ili kuwa na jamii jumuishi kwa wote*". Kupitia siku hii, shughuli mbali mbali zikiwemo michezo, ngoma za asili pamoja na shughuli nyengine zinazoonesha maendeleo na changamoto za watu wenye ulemavu zilifanyika.

Mhe. Naibu Spika, Idara imefanya tathmini ya awali ya kutambua mahitaji ya vikundi vya ujasiriamali vya Watu wenye Ulemavu pamoja na matumizi ya ruzuku kwa jumuiya za Watu wenye Ulemavu. Pia kwa kushirikiana na *"SAVE THE CHILDREN INTERNATIONAL"*, Idara ilifanya uhamasishaji juu ya haki na hifadhi ya mtoto mwenye ulemavu katika mabaraza ya watoto, madrasa, nyumba za kulelea watoto pamoja na maskuli Unguja na Pemba. Safari moja ya nje (nchini Marekani) na ziara mbali mbali za ndani zimefanyika. Safari hizi zimepelekea kukuza mashirikiano na nchi nyengine zinazotekeleza programu zinazohusu watu wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Watu wenye Ulemavu kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ilikadiriwa kutumia TZS 396,782,000/= kwa kuendeshea kazi, hadi kufikia Machi 2014 ilikwisha ingiziwa TZS 48,010,267/= sawa na asilimia 12. Kati ya fedha hizo TZS 220,000,000/= sawa na asilimia 56 ya bajeti yote ya Idara ni kwa ajili ya kununua visaidizi ambapo kwa mwaka huu shughuli hiyo haikufanyika. (Rejea Kiambatanisho namba 1)

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Naibu Spika, Ofisi hii ina jukumu la kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli zote za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa upande wa Pemba.

Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi Kuu Pemba ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuwapatia maslahi.
2. Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi.
3. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za OMKR Pemba.
4. Kukuza na kuimarisha mawasiliano ya habari.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2014 Ofisi Kuu Pemba imeweza kutekeleza yafuatayo:

Mhe. Naibu Spika, katika jitihada za kuimarisha ufanisi wa kiutendaji na majukumu, Ofisi imeajiri wafanyakazi 4 (wanawake 3, mwanamme1) kujaza nafasi za msingi katika Ofisi ya Faragha, wafanyakazi hao wote wamepatiwa mafunzo ya awali ili kuhakikisha ufanisi unapatikana. Aidha, mfanyakazi mmoja anayesoma mafunzo ya Rasilimali watu ngazi ya stashahada (Diploma) katika chuo cha Dar-es-salaam *"College of Hostel and Business Studies"* tawi la Pemba amelipiwa ada ya mafunzo.

Mhe. Naibu Spika, katika kuimarisha mazingira ya utendaji kazi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba ilifanikiwa kununua vifaa mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya ofisi. Aidha huduma stahiki kwa wafanyakazi mbali mbali kama vile posho la likizo, malipo baada ya saa za kazi na posho la kujikimu zimetolewa. Aidha, matengenezo madogo madogo ya sehemu za Ofisi yamefanyika.

Mhe. Naibu Spika, katika kuratibu shughuli za Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais Pemba, jumla ya ziara 7 za Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais zimeratibiwa. Huduma ya ulinzi katika nyumba ya Makamu wa Kwanza wa Rais zimeimarishwa.

Mhe. Naibu Spika, katika utekelezaji na ufuatiliaji wa shughuli mbali mbali za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba, elimu na ushauri nasaha kuhusu athari za dawa za kulevya ilitolewa kwa skuli tisa na nyumba 6 za kurekebisha tabia yaani "*Sober house*". Jumla ya wanafunzi 814 (wanawake 441, wanaume 373) na walimu 36 (wanawake 8, wanaume 28) walifaidika na elimu hiyo. Ofisi pia ilifanya uhakiki wa njia za matumizi ya dawa za kulevya. Vikundi 6 vya ushirika na ujasiriamali vya watu wenye ulemavu vilitembelewa ili kuona namna gani vikundi hivyo vinafanya kazi zake. Pia, mikutano 2 ya kuwahamasisha wazazi wenye watoto wenye ulemavu kuwapeleka skuli ilifanyika.

Mhe. Naibu Spika, ili kupunguza athari za uharibifu wa mazingira, usimamizi na ufuatiliaji wa hatua za ufukiaji katika maeneo 8 yalioathirika na uchimbaji wa udongo, mawe na kifusi wakati wa ujenzi wa barabara za Kaskazini Pemba umefanyika. Aidha, ukaguzi wa eneo la uchimbaji matofali uwandani kwa ajili ya kufuatilia maendeleo ya ukuaji wa miti iliyopandwa umefanyika. Maeneo mengine yakiwemo hoteli yamekaguliwa ili kuona kwa namna gani utekelezaji wa masharti ya kimazingira unafuatwa.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi Kuu Pemba kwa mwaka wa fedha 2013/14 ilikadiriwa kutumia TZS 167,575,000/= kwa kuendeshea kazi, hadi kufikia Machi 2014 ilikwishaingiziwa TZS 72,500,000/= sawa na asilimia 43. (Rejea Kiambatanisho namba 1)

TUME YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

Mhe. Naibu Spika, Tume hii ina jukumu la kuratibu mapambano dhidi ya biashara, matumizi, uingizwaji na usafirishaji wa dawa za kulevya Zanzibar. Tume pia ina jukumu la kutoa taaluma kwa jamii pamoja na kutoa huduma za tiba na ushauri nasaha kwa watumiaji wa dawa za kulevya.

Kwa mwaka wa Fedha 2013/2014, Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kupunguza matumizi ya Dawa za Kulevya.
2. Kupunguza usafirishaji, uzalishaji na usambazaji wa Dawa za Kulevya
3. Kuweka mazingira bora ya kazi na kuleta ufanisi katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2014 Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya imeweza kutekeleza yafuatayo:

Mhe. Naibu Spika, ili kuhakikisha Sheria ya Dawa ya Kulevya inatekelezeka "*Road Map*" ya utekelezaji wa sheria hiyo imeandaliwa na kuekewa makisio ya fedha zinazohitajika ili kuwarahisishia wadau wanaohusika katika utekelezaji. Aidha, vikao vitatu; viwili vya Tume ya Taifa ya Dawa za Kulevya na kimoja cha kamati ya kitaalamu cha dawa za kulevya vimefanyika. Kupitia vikao hivyo, mambo mbali mbali yenye lengo la kuendeleza mbele vita dhidi ya dawa za kulevya yalijadiliwa.

Mhe. Naibu Spika, katika kuona kwamba Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya inatekelezwa ipasavyo, rasimu ya kanuni ya sheria hiyo tayari imeshaandaliwa. Vile vile, juhudi za taasisi zinazohusika na mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya pamoja na mashirikiano kutoka kwa raia wema zinaendelea vizuri. Jumla ya watu 23 wamekamatwa kwa makosa ya dawa za Kulevya kati yao (wanaume 22 na mwanamke 1) na kesi 21 ziko mahakamani na upelelezi unaendelea.

Mhe. Naibu Spika, katika kuhakikisha jamii inapata taarifa sahihi juu ya athari na udhibiti wa dawa za kulevya, vipindi 10 vimerushwa hewani kupitia vyombo mbali mbali vya habari vikiwemo *Zenji FM, ZBC, Hits FM* na *Bomba FM*. Aidha filamu fundishi kuhusiana na athari za dawa za kulevya imetayarishwa na inatumika katika programu na vipindi vya kuhamasisha jamii.

Mhe. Naibu Spika, Tume pia iliandaa ziara katika skuli za Serikali, Binafsi na sehemu za kazi ili kutoa taaluma juu ya dawa za kulevya. Jumla ya wanafunzi 2,857 (wanawake 1,690 na wanaume1,167) kutoka skuli 31 za Unguja wamepatiwa elimu juu ya athari za Dawa za Kulevya na maambukizi ya virusi vya UKIMWI. (Angalia Kiambatanisho namba 5).

Ziara za utoaji wa elimu katika shehia mbalimbali za Unguja zimefanyika. Lengo la ziara hizo ilikuwa ni kuonana na kamati za ulinzi shirikishi na Polisi jamii za shehia. Jumla ya shehia 13 za Mkoa wa Mjini Magharibi ambazo zinaonekana kuathirika zaidi na biashara na matumizi ya Dawa za Kulevya pamoja na kuwa na maongezeko ya uhalifu katika jamii zilifikiwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kutambua na kuthamini mchango wa taasisi zisizo za kiserikali katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya, Tume inaendelea kuzipatia ruzuku nyumba za makaazi ya vijana wanaoacha matumizi ya dawa za kulevya yaani "*Sober Houses*" ili kusaidia mahitaji mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ilikadiriwa kutumia TZS 160,117,000/= kwa kuendeshea kazi, hadi kufikia Machi 2014 ilikwishaingiziwa TZS 40,657,333/= sawa na asilimia 25 (Rejea Kiambatanisho namba 1)

TUME YA UKIMWI

Mhe. Naibu Spika, majukumu makuu ya Tume ya UKIMWI ni kuhakikisha kwamba sera na mikakati ya taifa ya kupiga vita UKIMWI zinaandaliwa na kutekelezwa, kutafuta rasilimali zitakazotumika katika utekelezaji wa muitiko wa kitaifa wa kupambana na UKIMWI, kuimarisha uwezo wa wadau katika kufanyia kazi programu za UKIMWI na kuratibu shughuli zao, kushajihisha utoaji wa huduma za tiba na matunzo kwa watu walioathirika na kuathiriwa, kufuatilia na kutathmini umakini na ufanisi wa utekelezaji wa mikakati, sera na muitiko wa kitaifa na kutoa taarifa zote zinazohusiana na UKIMWI.

Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Tume ya UKIMWI ilipanga malengo yafuatayo:

1. Kuimarisha mazingira mazuri ya wafanyakazi wa Tume kwa ajili ya kuleta ufanisi katika shughuli za uratibu wa masuala ya UKIMWI.
2. Kuongeza uwezo wa programu za habari, utetezi na mawasiliano ili kuchochea mabadiliko ya tabia katika jamii na makundi maalum.
3. Kuimarisha Uratibu na Utekelezaji wa Sera, Sheria na Mkakati wa Taifa wa Pili wa kupambana na UKIMWI.
4. Kuongeza utumiaji wa taarifa zinazotokana na Ufuatiliaji, Tathmini na Utafiti katika programu za UKIMWI.
5. Kusimamia utaratibu wa udhibiti wa matumizi ya fedha.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2014 Tume ya UKIMWI imeweza kutekeleza yafuatayo:

Mhe. Naibu Spika, katika kuimarisha mazingira mazuri ya kazi na wafanyakazi wa Tume ili kuleta ufanisi katika shughuli za uratibu wa masuala ya UKIMWI, wafanyakazi 6 (4, UNG na 2, PBA) wamelipwa stahiki zao ikiwemo

likizo, malimbikizo ya mishahara na posho ya kufanya kazi katika mazingira magumu. Wafanyakazi 4 wamelipiwa gharama za masomo.
Vile vile, kumalizika kwa ujenzi wa sehemu ya juu ya Jengo la Tume imewezesha kuongezeka kwa nafasi za watendaji. Aidha, vikao vya Bodi ya Tume vimeweza kuimarisha usimamizi na uwajibikaji wa Tume. Sambamba na hayo, huduma mbalimbali zikiwemo unununzi wa mafuta, ulinzi, umeme na mtandao zimelipiwa kwa kurahisisha ufuatiliaji wa kazi.
Mhe. Naibu Spika, ili kuhakikisha ufanisi katika kuongeza uwezo wa programu za habari, utetezi na mawasiliano kwa kuchochea mabadiliko ya tabia katika masuala ya UKIMWI, Tume iliendelea kusambaza taarifa za UKIMWI kwa kuchapisha na kusambaza Jarida la Jihadhari nakala 10,000, kalenda 3,000 na pia kurikodi vielelezo vya kufundishia kwa watu wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, kama tunavyofahamu kwamba, kila mwaka ifikapo tarehe 1 Disemba duniani kote huwa tunaadhimisha siku ya UKIMWI duniani. Hapa Zanzibar, maadhimisho ya siku ya UKIMWI duniani yalifanyika, ambapo shughuli za kilele cha maadhimisho hayo zilifanyika katika kijiji cha Paje Wilaya ya Kusini Unguja. Pia, katika mwezi wa Disemba 2013, Sheria ya UKIMWI imepitishwa na Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*)
UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO
Mhe. Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014 Tume ya UKIMWI ilitekeleza miradi 2 ya maendeleo kwa fedha za Washirika wa Maendeleo. Fedha hizo ni kutoka *UNDP* na *UNFPA* kupitia programu ya *UNDAP*. Shughulli zilizotekelezwa kupitia fedha hizo ni kama zifuatazo:

1. Mradi wa *UNDAP* kwa ufadhili wa *UNDP*

Mhe. Naibu Spika, shughuli za kuratibu muitiko wa taifa wa kupambana na UKIMWI kupitia mikutano ya uratibu baina ya Tume na wadau mbali mbali zimeimarika. Wadau wanaohusika ni kutoka Sekta binafsi (Jumuiya ya Wafanya Biashara (*ABCZ*), Asasi za Kijamii (*CSOs*), Makundi Maalum, Kamati za Mawizara, Kamati za Wilaya na Jumuiya ya watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI - *ZAPHA+*. Pia, uwezo wa Kamati za UKIMWI wa kuingiza masuala ya UKIMWI umeongezeka kwa Wizara 5 kupatiwa mafunzo hayo.
Mhe. Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa Mkakati wa Pili wa Taifa wa UKIMWI kwa kipindi cha muda wa kati (*Mid Term Review*) yamefanyika kwa lengo la kuimarisha muitiko kwa kipindi kilichobaki cha uhai wa Mkakati (2014 -2016).
Mhe. Naibu Spika, wafanyakazi wanne wa Tume wamewezeshwa kushiriki katika mkutano wa 17 wa UKIMWI uliofanyika Afrika Kusini. Kupitia mkutano huo, Tume iliwasilisha mada mbili kwa njia ya "*Posters*". Mada hizo zinahusiana na changamoto za kuyafikia makundi maalum na namna ya upatikanaji wa huduma kwa makundi maalum.
Mhe. Naibu Spika, mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini umeendelea kutekelezwa kwa kukusanywa taarifa za watekelezaji na hatimae kutolewa ripoti ya mwaka ya ufuatiliaji. Aidha, taratibu za kufanya utafiti unaowalenga wavuvi kujua kiwango cha maambukizi zinaendelea ili kuwezesha kuandaliwa mipango ambayo msingi wake ni taarifa za kisayansi na za uhakika.
Mhe. Naibu Spika, mfumo wa kupashana na kusambaza habari/taarifa umeimarishwa kwa kununua vifaa vya kuiunganisha Ofisi na Mkonga wa Taifa. Pia, uwezo wa Shehia wa kupambana na unyanyasaji wa kijinsia umeongezwa na kuimarika katika Shehia 27 zilizochaguliwa Unguja na Pemba. Shehia zimejengewa uwezo na kupatiwa stadi zitakazowawezesha kutumia nyenzo zilizomo ndani ya Shehia zao katika kukabiliana na tatizo hilo na mengine ya kijamii.

2. Mradi wa *UNDAP* kwa ufadhili wa *UNFPA.*

Mhe. Naibu Spika, tathmini ya tatizo la unyanyasaji wa kijinsia katika maskuli imefanyika. Tume imeisadia Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA) kufanya tathmini hiyo ili hatimae kutafuta mbinu muafaka kupunguza tatizo hilo linaloweza kusababisha maambukizi ya *VVU.* Jumla ya skuli 100 za Unguja na Pemba zimehusika.
Mhe. Naibu Spika, upatikanaji wa huduma za UKIMWI kwa makundi maalum umeongezeka. Huduma za elimu ya UKIMWI, ushauri nasaha na upimaji wa VVU, usambazaji wa kondom na rufaa zimeongezeka kwa wanawake na wanaume. Watu 321 wamepima virusi vya UKIMWI, kondom 5,152 za kiume na 42 za kike zimesambazwa. Uelewa wa masuala ya kinga dhidi ya UKIMWI umeongezeka kwa kusambaza vipeperushi 442 kwa makundi maalum na kufanya mikutano ya elimu 462.
Mhe. Naibu Spika, elimu ya masuala ya afya ya uzazi imeongezeka kwa wanawake walioacha matumizi ya dawa za kulevya. Hamasa ya wanawake kuacha kutumia dawa za kulevya pia imeongezeka kwa kujiunga na nyumba za kurekebisha tabia. Wanawake 10 wamesaidiwa gharama za kujiunga na nyumba hizo.
Mhe. Naibu Spika, programu za stadi za maisha zimepanuka kwa kuwafikia vijana 95 wenye ulemavu na kusambaza vielelezo vya kujifunzia vinavyoendana na hali zao. Aidha, Makali ya athari za UKIMWI kwa watu wanaoishi na *VVU* yamepunguzwa kwa kusaidia vikundi 10 vya uzalishaji na kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa

wanawake 35 wanaoishi na *VVU* ili kunyanyua hali zao za maisha (Angalia Kiambatanisho namba 6). Vile vile, Utoaji wa elimu ya UKIMWI kupitia sanaa ya maonesho kwa jamii umefanyika katika Shehia 57 (Unguja 37 na Pemba 20) kupitia vikundi vya sanaa vya *THESODE* na UMATI ambapo watu 4667 (W/ke 2582 na W/me 2082) walifikiwa.

Mhe. Naibu Spika, Tume ya UKIMWI kwa mwaka wa fedha 2013/14 ilikadiriwa kutumia TZS 502,476,000/= kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2014, ilikwishaingiziwa TZS 211,313,500/= sawa na asilimia 42. Aidha Tume ya UKIMWI imepata jumla ya TZS 904,019,050/= kutoka kwa wahisani. (Rejea Kiambatanisho namba 1).

MUHUTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha utekelezaji cha mwaka 2013/14 OMKR ilikadiria kutumia TZS 3,020,000,000/= kwa kuendeshea kazi. Kati ya hizo TZS 1,820,400,000/= kwa matumizi mengineyo na TZS 1,199,600,000/= kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia Machi, OMKR ilikwishaingiziwa jumla ya TZS 551,999,910/= kwa matumizi mengineyo ambazo ni sawa na asilimia 30.

Kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilipanga kutumia TZS 150,000,000/= Hadi kufikia Machi 2014 ilikwishaingiziwa jumla ya TZS 120,000,000/= ambazo ni sawa na asilimia 80 ikiwa ni mchango wa Serikali. Kwa upande wa fedha za maendeleo kupitia program ya *UNDAP*, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imepokea TZS 471,966,510/= kutoka kwa mashirika ya maendeleo.

Aidha, kwa upande wa Tume ya UKIMWI katika kipindi cha utekelezaji cha 2013/14 ilitarajia kutumia TZS 768,000,000/= kwa kuendeshea kazi. Kati ya hizo TZS 502,476,000/= kwa ajili ya matumizi mengineyo na TZS 265,524,000/= kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia Machi Tume ilikwishaingiziwa jumla ya TZS 211,313,500= kwa matumizi mengineyo ambazo ni sawa na asilimia 46 Kwa upande wa fedha za washirika wa maendeleo. Tume ya UKIMWI ilipata TZS 355,283,900/= kupitia programu ya *UNDAP/UNFPA* na TZS 548,737,150/= kupitia *UNDAP/UNDP*.

VIPAUMBELE NA MALENGO YA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa Fedha 2014/15imejipangia vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kujenga uwezo kwa watendaji 20 wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais katika masuala ya utafiti.
ii. Kufanya tafiti tatu katika maeneo ya Mazingira, Watu wenye Ulemavu na Dawa za Kulevya.
iii. Kutayarisha Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.
iv. Kuandaa mpango wa utekelezaji wa Mkakati wa Mabadiliko ya Tabianchi.
v. Kutoa mafunzo ya tathmini za athari za kimazingira kwa wadau 70 kutoa taasisi mbali mbali Zanzibar.
vi. Kuendeleza operesheni 96 za mifuko ya plastiki na 96 za maliasili zisizorejesheka.
vii. Kuandaa mpango wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Watu wenye Ulemavu pamoja na kufanya mapitio ya Sheria Namba 9 ya mwaka 2006.
viii. Kujenga uwezo kwa jumuiya 10 za Watu wenye Ulemavu.
ix. Kuandaa mpango wa mawasiliano juu ya sera ya Watu wenye Ulemavu.
x. Kuanzisha programu ya Makuzi ya Awali ya Maendeleo ya Mtoto. (*Early Childhood Development).*
xi. Kuimarisha mapambano dhidi ya uingizaji wa dawa za kulevya.
xii. Kutoa kinga ya msingi kwa wanajamii ili kuwazuia kuingia katika janga la dawa za kulevya.
xiii. Kutoa tiba kwa walioathirika na dawa za kulevya ikiwemo kujenga kituo cha tiba (Detox) katika eneo la Kidimni.
xiv. Kukamilisha Mapitio ya Sheria No. 3 ya 2003 ya kuanzishwa Tume ya UKIMWI ambayo itapelekea kuanzishwa kwa mfuko wa fedha kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI (*HIV and AIDS Trust Fund*).

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa Fedha 2014/15, imepanga kutekeleza malengo yafuatayo kupitia Idara na Tume zake:

OFISI YA FARAGHA

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Faragha kwa mwaka wa fedha 2014/15 imejipangia kutekeleza malengo 2 yafuatayo:

1. Kusimamia na kuratibu shughuli zote za Makamu wa Kwanza wa Rais.
2. Kuimarisha mazingira ya kazi katika kuleta ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, ili Ofisi ya Faragha iweze kutekeleza malengo yake, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya TZS 411,150,000/=

kwa ajili ya kuendeshea kazi.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa mwaka wa fedha 2014/15 imepanga kutekeleza malengo 3 yafuatayo:

1. Kujenga uwezo wa utafiti kwa watendaji 20 na kufanya tafiti tatu katika maeneo ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais (Mazingira, Watu wenye Ulemavu na Dawa za Kulevya).
2. Kuratibu utekelezaji wa masuala mtambuka ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.
3. Kuratibu shughuli za sera, mipango na miradi ya maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya TZS 146,065,000/= kwa ajili ya kuendeshea kazi. Aidha, idara inaomba idhini ya kutumia jumla ya TZS 1,400,000,000/= kwa ajili ya kutekeleza mradi mmoja wa maendeleo wa kujenga kituo cha tiba kwa walioathirika na dawa za kulevya na TZS 577,500,000/= kwa ajili ya kutekeleza mradi wa mabadiliko ya tabianchi kupitia fedha za Washirika wa Maendeleo. Idara ya mipango pia inatarajia kupokea fedha TZS 28,000,000/= kupitia mradi wa kujenga uwezo unaoratibiwa na Tume ya Mipango. Fedha hizo zitatumika katika kuandaa Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi kwa mwaka wa fedha 2014/15 imepanga kutekeleza malengo 2 yafuatayo:

1. Kusimamia, kukuza na kuimarisha mazingira ya utendaji kazi wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na kuleta ufanisi.
2. Kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuwapatia maslahi.

Mhe. Naibu Spika, ili Idara ya Uendeshaji na Utumishi iweze kutekeleza malengo yake, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya TZS 1,610,084,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kati ya hizo TZS 320,084,000/= kwa ajili ya kuendeshea kazi na TZS 1,290,100,000/= kwa ajili ya mishahara.

IDARA YA MAZINGIRA

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mazingira kwa mwaka wa fedha 2014/2015 imejipangia kutekeleza malengo 3 yafuatayo:

1. Kuimarisha na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni za Mazingira.
2. Kusimamia uingizwaji wa masuala ya mazingira katika miradi ya maendeleo.
3. Kukuza uelewa wa elimu ya mazingira kwa jamii na wadau wengine.

Mhe. Naibu Spika, ili Idara ya Mazingira iweze kutekeleza malengo yake, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya TZS 113,284,000/= kwa ajili ya kuendeshea kazi.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara ya Mazingira imepangiwa kukusanya jumla ya TZS 10,500,000/= ambazo zinatokana na ada ya hifadhi ya mazingira ikiwa ni pamoja na vyeti vya mazingira.

IDARA YA WATU WENYE ULEMAVU

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Watu wenye Ulemavu kwa mwaka wa fedha 2014/15 imepanga kutekeleza malengo 3 yafuatayo:

1. Kuimarisha na kusimamia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo kwa Watu wenye Ulemavu.
2. Kusimamia haki, fursa sawa na ujumuishwaji wa Watu wenye Ulemavu.
3. Kuanzisha programu ya Makuzi ya Awali ya Maendeleo ya Mtoto *(Early Childhood Development)*.

Mhe. Naibu Spika, ili Idara ya Watu wenye Ulemavu iweze kutekeleza malengo yake, kwa mwaka fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya TZS 278,442,000/= kwa ajili ya kuendeshea kazi.

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Naibu Spika, Ofisi Kuu Pemba kwa mwaka wa fedha 2014/15 imepanga kutekeleza malengo 4 yafuatayo:

1. Kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuwapatia maslahi.
2. Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi.
3. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba.
4. Kukuza na kuimarisha mawasiliano ya habari.

Mhe. Naibu Spika, ili Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba iweze kutekeleza majukumu iliyopanga kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya TZS 369,575,000/= kwa matumizi

mengineyo. Kati ya hizo TZS 159,575,000/= kwa kuendeshea kazi na TZS 210,000,000/= kwa ajili ya malipo ya mishahara.

TUME YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

Mhe. Naibu Spika, Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha 2013/14 imepanga kutekeleza malengo 3 yafuatayo:

1. Kupunguza matumizi ya Dawa za Kulevya.
2. Kupunguza usafirishaji na usambazaji wa Dawa za Kulevya.
3. Kuweka mazingira bora ya kazi na kuleta ufanisi katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Mhe. Naibu Spika, ili Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya iweze kutekeleza malengo iliyopanga kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya TZS 324,000,000/= kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo TZS 220,000,000/= kwa kuendeshea kazi na TZS 144,000,000/= kwa ajili ya malipo ya mishahara.

TUME YA UKIMWI

Mhe. Naibu Spika, Tume ya UKIMWI kwa mwaka wa fedha 2014/15 imepanga kutekeleza malengo 4 yafuatayo:

1. Kuongoza, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Mkakati wa Pili wa Kitaifa wa UKIMWI kwa wadau wote.
2. Kuimarisha ubora wa taarifa zinazokusanywa pamoja na kufuatilia matumizi ya taarifa zinazotokana na ufuatiliaji, tathmini na utafiti wa programu za UKIMWI.
3. Kutoa miongozo na kuratibu masuala ya habari, utetezi na mawasiliano kuhusu UKIMWI ili kuchochea mabadiliko ya tabia katika jamii na makundi maalum.
4. Kuongoza pamoja na kuimarisha mazingira mazuri ya kazi na wafanyakazi wa Tume kwa ajili ya kuleta ufanisi katika shughuli za uratibu wa masuala ya UKIMWI.

Mhe. Naibu Spika, ili Tume ya UKIMWI iweze kutekeleza malengo iliyopanga kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya TZS 811,000,000/= kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo TZS 533,208,700/= ni kwa ajili ya kuendeshea kazi na TZS 277,791,300/= kwa ajili ya mishahara. Aidha naomba Baraza lako liidhinishe TZS 50,000,000/= kwa kazi za Maendeleo kupitia SMZ na TZS 1,369,000,000/ kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, muhutasari wa makisio ya matumizi kwa mwaka 2014/15 kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais (Angalia Kiambatanisho namba 7).

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais pia imelenga shabaha mbalimbali katika kufikia malengo yake iliyopanga kutekeleza kwa mwaka wa 2014/15. (Angalia Kiambatanisho namba 8).

SHUKURANI

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuzishukuru nchi marafiki, Mashirika ya Kimataifa, pamoja na watu binafsi ambazo zinaendelea kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais katika kutekeleza majukumu yake. Nchi hizo ni pamoja na Marekani, Finland, Norway, Uingereza, Uholanzi, Jamhuri ya Watu wa China, India, Falme za nchi za Kiarabu. Mashirika ya kimataifa yakiwemo *UNDP, UNICEF, UNFPA, UNAIDS, UNEP, UNODC, UNESCO, UNIDO, DFID, WHO, World Bank, AIHA, ICAP, Save the Children* na nchi na mashirika mengine ambayo sikuyataja, lakini kwa njia moja au nyengine yanatuunga mkono katika shughuli zetu za maendeleo. Michango yao tunaijali na kuithamini.

Mhe. Naibu Spika, napenda kutoa shukurani za dhati kwa Taasisi mbali mbali za serikali ikiwemo vyombo vya ulinzi na usalama na taasisi zisizo za kiserikali zinazojishughulisha na masuala ya UKIMWI, mapambano dhidi ya dawa za kulevya, utunzaji na uhifadhi wa mazingira na kutetea haki na fursa za watu wenye ulemavu. Nawaomba waendelee kutupa mashirikiano na hatimae kufikia lengo kuu la kukuza uchumi na kupunguza umasikini.

Aidha, napenda kuwashukuru waandishi wa habari kupitia vyombo vyao vikiwemo Televisheni, Redio na Magazeti ambavyo vimekuwa vikishirikiana nasi katika kuielimisha jamii juu ya shughuli zinazotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, napenda kutoa shukurani za pekee kwa Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, akiwa ndio kiongozi wa ofisi yetu, kwa maelekezo yake kwangu. Nawashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Dr. Omar Shajak na Naibu Katibu Mkuu Dr. Islam Salum kwa ushirikiano na ushauri wanaonipa ambao ndio ulioniwezesha kutekeleza kwa ufanisi majukumu ya ofisi yetu kwa mwaka 2013/2014.

Napenda pia kuwashukuru kwa dhati Afisa Mdhamini, wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba, Wakurugenzi Watendaji wa Tume na Wakurugenzi wa Idara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na Watendaji wote kwa kuifanya Ofisi yetu iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa na kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kuandaa mpango na bajeti hii kwa wakati.

Mhe. Naibu Spika, napenda niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwa kuwa wasikivu na wastahamilivu wakati nikiwasilisha hotuba yangu. Nawaomba waendelee kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais katika kutoa ushauri na michango mbali mbali ili kusaidia katika kuleta ufanisi.

Aidha, nakupongeza wewe binafsi Mhe. Naibu Spika, kwa busara zako katika kuliongoza Baraza hili. Ninakuombea wewe pamoja na Waheshimiwa wote kila la kheri, afya njema na mafanikio katika kazi za kila siku. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inaamini kuwa *'Kwa Pamoja Tutaweza'*, kudhibiti uharibifu wa mazingira, kupunguza uingiaji na usambazaji wa dawa za kulevya, kuzuia maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi, (*VVU*) na kukomesha unyanyasaji wa Watu wenye Ulemavu endapo kila mmoja wetu ataendelela kutimiza wajibu wake.

HITIMISHO

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima nachukua nafasi hii kuwaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waipokee, waijadili, watushauri, watuelekeze na hatimae kuidhinisha makadirio ya matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ya jumla ya Shilingi Bilioni mbili, milioni mia tisa ishirini na nane na laki saba (TZS 2,928,700,000/=). Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni moja milioni mia nne ishirini na nane na laki sita (TZS 1,428,600,000/=) kwa matumizi mengineyo, na Shilingi Bilioni moja, milioni mia tano na laki sita (TZS 1,500,600,000/=) kwa ajili ya mishahara.

Aidha, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi Bilioni moja, milioni mia nne (TZS 1,400,000,000/=) kwa kazi za maendeleo, ikiwa ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Shilingi milioni 577,500,000/= ikiwa ni mchango wa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, naliomba pia Baraza lako tukufu liidhinishie Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya matumizi ya TZS 364,000,000/= kwa kazi za kawaida, ambapo TZS 220,000,000/= kwa matumizi mengineyo na TZS 144,000,000/= kwa ajili ya mishahara.

Mhe. Naibu Spika, naliomba pia Baraza lako tukufu liidhinishie Tume ya UKIMWI matumizi ya TZS 811,000,000/= kwa kuendeshea kazi, ambapo kati ya hizo TZS 533,208,700/= kwa ajili ya matumizi mengineyo na TZS 277,791,300/= kwa ajili ya mishahara. Aidha, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya TZS 50,000,000/= kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa serikali na TZS 1,369,000,000/= ikiwa ni mchango wa Washirika wa Maendeleo.

Aidha, naliomba Baraza lako tukufu likubali mchango wa jumla ya TZS 10,500,000/= ikiwa ni mapato yaliyokadiriwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tunampongeza Mhe. Waziri kwa kutumia muda uliopangwa wa saa moja kamili, ambao hakuzidisha wala hakupunguza tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Kabla hatujaanza kumwita Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo kwamba bajeti iliyopita tuliwaacha Wajumbe wengi hawakuchangia kutokana na sababu wanachelewa kuleta maombi yao. Nashukuru sasa hivi nimepata Waheshimiwa wanne tu katika hotuba iliyosomwa sasa hivi.

Kwa hivyo, naomba yule mwenye nia ya kuchangia alete mapema ili tuweze kujipanga vizuri, tupate nafasi wengi ya kuchangia. Baada ya maelezo hayo, sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Mhe. Hamza Hassan Juma. Baada yake atafuatia Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, na Mhe. Mohammedraza Hassanali *(Makofi).*

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, kabla sijaanza kutoa shukurani zangu kwako nilikuwa nataka kidogo Mhe. Waziri naomba dakika zangu usizihisabu kwanza.

Mhe. Waziri naomba hebu jaribu kuangalia kwenye ukurasa wa 55 wa kitabu chetu hichi, lakini halafu vile vile turudi kwenye ukurasa wa 43 wa kitabu chetu hichi kikubwa cha bajeti, kwa sababu kuna tofauti kidogo katika eneo hili la kasma zetu hizi ili tuhakikishe kwamba tunapopitisha hili fungu basi liwe tumelipitisha sawa sawa.

Nilikuwa naomba katika hiki Kiambatanisho namba 7 tuangalie hii kasma 06/03 Afisi Kuu Pemba, Afisi Kuu Pemba hapa jumla imewekwa milioni 369, lakini kwenye mishahara kwenye hichi kitabu ulichokisoma Mhe. Waziri kwenye mishahara kinasoma kwamba jumla itakuwa ni milioni 210. Lakini sasa ukija kwenye kitabu cha bajeti hichi kitabu kikubwa, na naomba Waheshimiwa tufanye masahihisho ya pamoja ukiangalia ukurasa wa 43 kifungu 0301 Afisi Kuu Pemba ukija kwenye jumla ndogo hapa kimesema 211100 kinasema milioni 207.

Sasa nilikuwa najaribu kuangalia isije ikawa tumetofautisha kidogo katika maelezo lakini hili nadhani Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake bila ya shaka wananisikia tutajaribu kuliangalia kwa pamoja ili tuoanishe hii jumla ya

mishahara kwa upande wa Pemba milioni 210 na huku kuna milioni 207 kwenye kitabu kikubwa, ili tuweze kuweka sawa katika *Hansard* yetu, lakini vile vile, katika kasma zetu.

Lakini kuna jambo jengine Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa huo huo wa 55 nimejaribu kuangalia kwenye hichi kifungu cha mwisho kabisa ambacho wao wamekiandika 51/01 kinachozungumzia Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Madawa ya kulevya ambayo kuna jumla kuu 364 milioni, kwenye mishahara kuna milioni 144. Sasa nilipojaribu kufanya masahihisho kwenye kitabu chetu hichi kikubwa nilijaribu sana kuitafuta ile kasma inayohusu uratibu wa madawa ya kulevya, sasa kwenye kitabu chetu hichi kikubwa kuna 000 niliziona. Sasa unajua wakati mwengine na utu uzima unakuja na macho, na kwa sababu Waheshimiwa Makamu Mawaziri Jazira na Mshimba leo muda mrefu pale walipokaa mbele walinishughulisha kidogo, kwa hivyo inawezekana pengine nikawa sikuona vizuri. Sasa nadhani Mheshimiwa Waziri hili baadae tuje tuangalie hii kasma ya Tume ya Kuratibu ya Udhibiti wa madawa ya kulevya kwenye kitabu chetu kikubwa hichi, hii kasma yake itakuwa ipo hapa.

Sasa baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, nataka sasa uanze kunihesabia dakika zangu na niendelee moja kwa moja kwenye hoja.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu (*S.W*) kwa kutujaalia kukutana tena leo hii katika Baraza lako Tukufu kwa lengo la kujadili masuala muhimu kwa ajili ya maslahi na maendeleo ya watu wetu na nchi yetu kiujumla, ikiwemo suala hili muhimu la kujadili masuala ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Taasisi mbali mbali za Serikali; ikiwemo leo hii tunajadili bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, aidha nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kwa lengo la kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika**,** lakini vile vile nataka niungane tena na Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kumpongeza Mhe Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa mwaka wanne wa awamu yake, tukishuhudia amani na utulivu wa nchi yetu na wananchi wake inaendelea kudumishwa. Lakini pia hatua za kuimarisha hali ya maisha ya wananchi wetu zinaenendelea hatua kwa hatua na tunawaomba sisi viongozi na wananchi wetu tuendelee kumpa mashirikiano Rais wetu ili aweze kutekeleza yale yote aliyojipangia kwa faida ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, Kamati yangu inatoa shukrani kwa Makamu wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad kwa kumsaidia Rais wetu ushauri katika kuwaletea maendeleo wananchi wetu, na pia yeye mwenyewe anavyoweza kuisimamia Ofisi yake kuweza kutekeleza majukumu yao waliyojipangia siku hadi siku.

Mhe. Naibu Spika, pia niungane tena na Mhe Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kumpongeza Mhe Makamu wa Pili wa Rais, naye kwa kumsaidia Mhe Rais na kumshauri katika kuwaletea maendeleo wananchi wetu, na ameonesha uwezo mkubwa kwa kumshauri vyema na ndio maana tunashuhudia hali ya amani, upendo, maelewano na mshikamano inayoendelea hapa nchini kwetu na ninaamini wananchi wote wanafurahia hali hiyo.

Mhe. Naibu Spika, pia, uniruhusu nimpongeze Mheshimiwa makini kabisa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na watendaji wake wote, kwa mashirikiano yao ya dhati wanayoipa Kamati yangu katika kutekeleza majukumu yetu ya msingi.

Vile vile, napenda kuishukuru Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kuwasilisha mbele ya Kamati yetu pamoja na Baraza lako Tukufu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2014/2015 ya Wizara yao, ili yapate Baraka za Wajumbe wako na baadae yapitishwe kwa maslahi ya wananchi na Serikali kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia, sitosahau kwa dhati kabisa kuwashukuru kwa dhati kabisa Wajumbe wa Kamati yangu kwa mashirikiano yao makubwa wanayonipa katika kutekeleza majukumu ya kazi zetu, na naomba niwataje Waheshimiwa Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma	Mwenyekiti
2. Mhe. Saleh Nassor Juma	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Mzee Ali	Mjumbe
4. Mhe. Ashura Sharif Ali	Mjumbe
5. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Mjumbe
6. Mhe. Subeit Khamis Faki	Mjumbe
7. Mhe. Shadya Moh'd Suleiman	Mjumbe
8. Nd. Rahma Kombo Mgeni	Katibu
9. Nd. Makame Salim Ali	Katibu

Mhe. Naibu Spika, baada ya Utangulizi huo, sasa kwa niaba ya Kamati naomba uniruhusu niwasilishe maoni yetu juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 kama ifuatavyo:-

IDARA YA FARAGHA

Mhe. Naibu Spika, tunaipongeza Idara ya Faragha kwa kuendelea kutekeleza majukumu yake ya kuratibu na kutoa huduma kwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar kwa kufanikisha ziara mbali mbali za Makamu, kusaidia jumuiya na vikundi mbali mbali Unguja na Pemba pamoja na kukutana na wageni mbali mbali kutoka ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kukuza uhusianao, lakini pia na kubadilishana mawazo juu ya masuala mbali mbali kwa maendeleo ya nchi na wananchi wake kiujumla.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na idara kutekeleza majukumu yake ipasavyo lakini bado inakabiliwa na tatizo la uingizwaji mdogo wa fedha kwa matumizi ya kawaida kama Idara ya Faragha ya Mhe Makamu wa Kwanza wa Rais. Hivyo, Kamati inasisitiza kwa bajeti ya mwaka huu idara hii ya Faragha iingiziwe fedha ipasavyo ili uondoke usumbufu uliojitokeza kwa Idara nyeti kama hii ambayo haileti picha nzuri iwapo Kiongozi Mkuu wa nchi bajeti yake iwe ya kusuasua.

Mhe Naibu Spika, kamati yangu pia inaitaka Serikali kuharakisha upatikanaji wa makaazi ya viongozi wetu wakuu wa Kitaifa, pamoja na kuwapatia magari ya kutosha ili kuwawezesha kufanya kazi zao vizuri na kuwatumikia wananchi wetu vizuri, kwa ufanisi mkubwa na ambao ulikuwa unatarajiwa.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe Naibu Spika**,** Kamati inaipongeza Idara hii kwa jitihada wanazozichukua katika kuandaa na kusimamaia utekelezaji wa sera na mipango ya maendeleo kwa ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kukusanya na kutunza takwimu pamoja na kuratibu shughuli za utafiti.

Mhe Naibu Spika, Kamati yangu inapongeza kazi kubwa inayofanywa na Idara hii inayoongozwa na mwanamama hodari, shupavu na mchapakazi, kwani Idara hii ndio *engine* ya Ofisi hii, kwani katika karne ya sasa kila mradi au jambo lolote kabla ya kulifanya basi kwanza ni lazima kulifanyia utafiti ili kujua faida na hasara zake, ili unapokuja kulitekeleza basi ujue na changamoto gani zitajitokeza na kuweza kukabiliana nazo. Kamati yangu inaipongeza Idara kwa kukamilisha Rasimu ya mwanzo ya Sera ya watu wenye ulemavu, ambayo kwa hivi sasa iko kwa wadau kwa ajili ya kuweza kutolewa maoni yake.

Mhe Naibu Spika, tunaomba sana Idara hii kuendelea kufuatilia hayo maoni ya wadau ili yaweze kukamilika na baadae Sera ikamilishwe, ili kuweza kuondoa manung'uniko lakini vile vile kuweza kutoa muongozo kwa taasisi mbali mbali katika kutekeleza majukumu yao katika kushughulikia watu wenye ulemavu.

Mhe, Naibu Spika, kamati yangu vile vile inaomba kuongeza fungu kwenye Wizara hii ili idara hii iweze kupata fungu kubwa ili iweze kutekeleza majukumu yao waliyojipangia.

IDARA YA MAZINGIRA

Mhe. Naibu Spika**,** tunapongeza jitihada kubwa zinazofanywa na Idara hii siku hadi siku, mbali na jitihada zinazofanywa kupitia idara hii, lakini bado kuna changamoto kubwa ambazo zinaikabili zinazopelekea kukwamisha juhudi zinazofanywa na watendaji wa Idara kutokana na ukosefu wa sheria madhubuti itakayowasaidia kuwatia hatiani waharibifu wa mazingira na kuchukuliwa hatua zinazofaa.

Mhe. Naibu Spika, Kamati pia inashauri kufanywa jitihada za makusudi katika kutatuliwa kero za uharibifu wa mazingira zinazofanywa ndani ya manispaa ya mji wetu, ambapo husababisha kero na usumbufu kwa wakaazi lakini pia hata maradhi ya miripuko kutokana na uwepo wa taka taka. Kutokana na hali hiyo, Kamati inashauri kuwepo na ushirikiano kati ya Baraza la Manispaa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa lengo la kusaidiana katika uwekaji mji safi.

Vile vile, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua zinazofaa katika eneo liliopo jirani na Msikiti Mabluu ambalo limezingiwa mabati bila kujengwa kwa muda mrefu hivi sasa, jambo ambalo limefanya kugeuzwa kuwa sehemu ya kutupia taka, lakini pia limekua likituama maji ambayo hupelekea uchafu kuongezeka, na kusababisha kuwa ni sehemu ya mazalia makubwa ya mbu. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, tunaomba sana Baraza la Manispaa kwa kushirikiana na Idara hii ya Mazingira iweze kulishughulikia suala hili.

Mhe Naibu Spika, Kamati yangu inaitaka Idara kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuileta upya na kuifanyia marekebisho makubwa Sheria ya Mazingira ili kumpa meno Mkurugenzi kuweza kusimamia na kutoa adhabu kwa mtu au taasisi yoyote ambayo itakiuka sheria kwa kuharibu mazingira, lakini pamoja na kazi nzuri Idara hii iliyoifanya kuweza kupiga vita uingizwaji wa mifuko ya plastiki, Kamati yangu bado inaitaka Idara hii kuendeleza jitihada za kuhakikisha mifuko hiyo inatoweka kabisa. Lakini pamoja na hayo kwa kweli idara hii tunaipa pongezi kubwa kwa kupitia Mhe. Waziri kwa sababu kwa kweli hali ya mifuko ya plastiki Zanzibar, sasa hivi pamoja na kwamba ingalipo lakini ipo kwa kificho sana sio kama ilivyokuwa vile zamani.

Mhe. Naibu Spika**,** vile vile, Kamati yangu kwa mara nyengine tena inaiagiza Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano wakati wanapofanya ujenzi wa barabara wahakikishe ile 10% ya fidia ya uharibifu wa mazingira inatolewa na kupewa Idara ya mazingira kama sheria inavyotaka.
Mhe Spika, bila kusahau kama tulivyokumbushia bajeti iliyopita, Kamati inaiomba tena Serikali kuiangalia kwa jicho la huruma ofisi ya Idara ya mazingira ambayo haistahiki na wala haina hadhi ya kuwepo Mkurugenzi wa Idara hiyo; kwanza ni uchakavu na udogo wa Ofisi hiyo vile vile kutokana na majukumu yao, hivyo basi zichukuliwe jitihada za makusudi kutafutwa ofisi ambayo itakuwa na hali nzuri kimazingira na itakayowatosheleza kwa mujibu wa kazi zao tofauti na ilivyo sasa ambapo hawana nafasi wala mazingira mazuri ya kufanyia kazi.
Mhe. Naibu Spika**,** Kamati yangu inaipongeza Idara hii kwa kushirikiana na Idara ya Mipango na Sera kwa kuweza kulifikisha suala la mpango wa mkakati na wa mabadiliko ya tabia nchi katika mipango ya Maendeleo, kwani hivi sasa Dunia nzima inaungana kwa pamoja katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.
Lakini vile vile, kudhibiti athari za Mazingira, kwani hivi sasa kuna maeneo mengi hasa yaliyo pembezoni mwa Bahari kwa hapa Zanzibar ambayo mwanzoni yalikua yakilimwa mpunga na hivi sasa yamevamiwa na maji ya Bahari na hivi sasa hayawezi tena kulimwa mpunga na mazao mengine, jambo ambalo linawaongezea wananchi wetu umaskini wa kipato. Lakini vile vile, kuwaongezea umaskini wa hali ya maisha yao.

Vile vile, kazi kubwa ifanyike kwa ajili ya kutoa elimu kwa watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwani ikiweza kutoa elimu kwao, kwa sababu wao ndio wapangaji wa mipango na maendeleo. Kwa hivyo, tunaipongeza Idara hii kushirikiana na mipango na sera kwa kupeleka kwenye Baraza la Mapinduzi Mpango Mkakati wa kukabiliana na hali ya tabia nchi katika mipango yetu ya maendeleo ya huko tunakokwenda.

IDARA YA WATU WENYE ULEMAVU

Mhe.Naibu Spika, Kamati yangu inampongeza Mkurugenzi wa Idara hii mwanamama shupavu, mchapa kazi Bi Abeda kwa jitihada kubwa anazozifanya kwa kushirikiana na timu yake ya Idara ya Watu Wenye Ulemavu ikiwemo kuratibu masuala mbali mbali ya Watu Wenye Ulemavu kama Sheria Nam. 9 ya mwaka 2006 tulivyomkabidhi majukumu hayo. Mbali na jitihada hizo bado Idara inakabiliwa na changamoto kubwa sana ikiwemo uhaba wa fedha za kununulia visaidizi vya Watu Wenye Ulemavu ambapo kwa mwaka huu havikuweza kununuliwa kutokana na kutoingiziwa fedha hizo.

Hivyo, Kamati yangu inasisitza ndani ya mwaka huu wa fedha idara hii iweze kuiingiziwa zile fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivyo ambavyo kwa mwaka havikuweza kununuliwa, ili lile lengo lililokusudiwa liweze kufikiwa. Kamati yangu inaitaka Serikali kuyapa kipaumbele mahitaji ya watu wenye Ulemavu kutokana na maumbile yao, ili na wao waweze kushiriki vizuri kama wenzao katika kuiletea maendeleo nchi yetu. Kwa hiyo, tunaitaka Serikali kuwatilia pesa za kutosha ili kuweza kununulia vifaa ndugu zetu hao kwa ajili ya mahitaji yao.

Mhe. Naibu Spika, Kamati kama yangu kama nilivyoitaka Serikali kwenye hotuba yangu niliyoiwasilisha kwa Bajeti Kuu ya Serikali kupitia Tume ya Utumishi wa Umma tunaendelea kusisitiza kuangaliwa kwa suala la *scheme of Service* maalum kwa Wafanyakazi wote Wenye Ulemavu kwani imebainika kuwa wao wana mahitaji maalum ukilinganisha na wafanyakazi wengine wa kawaida. Jambo ambalo kwa mshahara wanaopewa huwa haukidhi haja kutokana na mahitaji yao ya kila siku.

Hivyo, basi tunaiomba Serikali kuliangalia suala hilo kwa ukaribu zaidi kwa watu wenye ulemavu, ili na wao waweze kujikimu kimaisha kama wenzao licha ya kuwa na maumbile tofauti na wenzao kwa kuwezeshwa au kwa kupatiwa fedha au kwa kuingiziwa fedha katika mishahara yao ambazo watazitumia kwa mahitaji yao ambapo zitawasaidia sana kuweza kujikimu.

Mhe. Naibu Spika, bado Kamati yangu inaitaka Idara hii kuharakisha na kukamilisha takwimu ya watu wenye Ulemavu yaani ile *Database* ili kuweza kuwatambua ndugu zetu hawa wenye ulemavu wapi walipo na kuweza kuwatambua na kuwapatia huduma muhimu, ili na wao waweze kufaidika na matunda ya maendeleo kwa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, Vile vile, suala la Mfuko wa Maendeleo kwa Watu Wenye Ulemavu nalo kamati inaendelea kusisitiza liharakishwe ili liweze kuwasaidia katika kutekeleza majukumu yao mbali mbali yanayowakabili. Hata hivyo, suala la *data base* kwa Watu Wenye Ulemavu nalo lifanyiwe kazi haraka nilivyoeleza hapo juu.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa katika idara hii kamati yangu inapenda kukumbushia kwa mara nyengine tena majengo yote ambayo ya serikali yaliyojengwa hapo zamani basi kwa sasa yaweze kufanyiwa tathmini kwa kuweza kuzingatiwa, ili yaweze kutumika na watu wenye ulemavu au yatengenezewe mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu ili yawe rafiki kwao na kuwekwa sheria madhubti ambayo itaweza kumbana yeyote ambaye atakiuka taratibu zisizozingatia mahitaji ya Watu Wenye Ulemavu.

TUME YA URATIBU MADAWA YA KULEVYA

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu inaipongeza na kuipa pole Tume ya Madawa ya Kulevya kwa kazi kubwa na ngumu tuliyowapa kwa kuratibu na kupambana na uingizwaji wa madawa na utumiaji wa madawa ya kulevya kwa mashirikiano na Jeshi la Polisi. Pamoja na jitihada hizo bado Tume inakabiliwa na changamoto nyingi kama zilizo Idara nyengine za Wizara hii, ambazo zinakwamisha jitihada zao ikiwemo kukwama kwa kesi na kuchukua muda mrefu bila mafanikio. Hali hii inapelekea watuhumiwa kuachiwa na kesi kufa kwa madai ushahidi haujakamilika.

Lakini pia, ukosefu wa vitendea kazi vya kutosha kwa kitengo hiki cha kuratibu madawa ya kulevya lakini hata kitengo cha Jeshi la Polisi cha kupambana na madawa ya kulevya. Tunaiomba sana serikali yetu kukiangalia kitengo cha Polisi cha Madawa ya Kulevya, kwa sababu bila ya wao kuwa na vitendea kazi vya kutosha kwa kweli Idara hii itapata tabu sana katika kuweza kupambana na madawa ya kulevya.

Mhe Naibu Spika, Kamati yangu inaiomba jamii kuamua kwa pamoja kutokomeza janga hili la matumizi ya madawa ya kulevya, kwani jamii yetu hasa vijana ambao ndio tegemeo la familia zao na Taifa letu kwa jumla. Lakini cha kusikitisha kuwa madawa haya yanauzwa mitaani kwetu na sisi tunaona, tunashuhudia, lakini kila mtu anaitupia lawama Serikali. Mimi nnawauliza wajumbe wenzangu kwani Serikali ni nani? Jawabu lakini pia, ninayo kwa sababu Serikali ni mimi, wewe na waliopewa dhamana kuiongoza nchi hii. Kwa hiyo, tushirikiane sote ili kupiga vita na kupambana na janga hili kubwa kwa taifa kwani kama hatukulifanyia kazi kwa sote suala hili kwa pamoja, basi tutaharibikiwa sote.

Hebu waheshimiwa sote tuamue kwenye majimbo yetu kwa kushirikiana na Polisi Jamii kuweka ulinzi na kuwafichua wote wanaoingiza na kuuza madawa hayo ya kulevya kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi kuwakamata je, basi hata hili linatushinda? Naamini tukiamua sote kwa pamoja basi hakutaweza kuingia wala kuuzwa madawa hayo katika nchi yetu. Zaidi ukiangalia Zanzibar ni ndogo sana na sote tunajuana. Kwa hiyo, ninaomba hebu tushirikiane sote kwa pamoja, tuone kama hata kete moja kama itaweza kuingia hapa Zanzibar.

Pamoja na hayo, lakini bado Serikali inabidi kuchukua jitihada za makusudi za kuhakikisha vitendea kazi vinapatikana kwa Idara hii ili kuweza kuendekesha vizuri kazi zao. Lakini vile vile serikali kuweza kuhakikisha kwamba uendeshaji mzuri wa kesi na ufuatiliaji wa ushahidi kuwa ni wa uhakika, ili lengo lililokusudiwa la kumaliza tatizo hili liweze kufikiwa.

Mhe. Naibu Spika**,** Kamati yangu pia inasisitiza sana juu ya suala la mashirikiano ya kila mtu katika kuhakikisha kuwa tunazuia matumizi ya madawa ya kulevya katika jamii yetu. Tunapaswa kuelewa kuwa hili ni jukumu la kila mtu na sio Jeshi la Polisi tu au Tume ya Kuratibu Madawa ya Kulevya.

Mhe Naibu Spika, Kamati yangu inaipongeza idara hii kwa kushirikiana na Idara ya Mipango na Sera na Utafiti ya Afisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kufanikiwa kupata kiwanja huko Kidimni kwa ajili ya kujenga kituo cha kurekebisha tabia *(Rehabilitation Centre).* Ili kuweza kuwapatia huduma wale vijana wetu ambao wameathirika kwa kutumia madawa ya kulevya.

Kwa hiyo, pamoja na kwamba mradi huu ni mkubwa lakini hadi sasa hakuna muhisani yeyote ambae amejitokeza kuweza kusaidia ujenzi huu mkubwa. Tunaiomba Serikali kwenye bajeti inayokuja mwakani basi mradi huu uweze kutengewa fedha kwa ajili ya ujenzi japo kwa awamu, au kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kuweza kujenga kituo hiki na Serikali kuweza kuwarejeshea pesa zao kidogo kidogo, ili kuweza kulimaliza jengo hili kwa wakati na kuweza kuwarejeshea hali zao vijana wetu walioathirika na madawa ya kulevya, ili baadae warudi kuungana na familia zao kwa ajili ya kuijenga nchi yetu.

TUME YA UKIMWI

Mhe. Naibu Spika, Kamati inapongeza jitihada zinazochukuliwa na Tume ya Ukimwi katika kupambana na maambukizi mapya kwa jamii kwa kutoa elimu na mafunzo mbali mbali kwa jamii, ili waweze kujikinga na kuepukana na uhatarishi wa ugonjwa huu hatari wa Ukimwi ambao unaathiri kwa kiasi kikubwa maendeleo ya nchi yetu na kupoteza nguvu kazi yetu siku hadi siku.

Mhe. Naibu Spika, bado Kamati kwa mara nyengine tena inasisitiza kwamba Tume ya Ukimwi kuwa karibu sana na ZAPHA+, Serikali pamoja na *NGOs* nyengine zenye kusaidia kupiga vita masuala ya ukimwi kwa kukaa pamoja na kuwa na mashirikiano kwa hali na mali katika kupunguza changamoto zinazoikabili jamii yetu, ambazo hutokana na athari za ugonjwa huu wa ukimwi.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu vile vile inaiomba jamii yetu kuacha unyanyapaa kwani bado Zanzibar ina kiwango kikubwa cha unyanyapaa na ndio maana watu wengi wanaogopa kwenda kupima kwa hiari, kwa kuogopa kutengwa na jamii iwapo atagundulika na maambukizi ya virusi vya ukimwi. Jambo ambalo linarejesha nyuma jitihada za mapambano dhidi ya maradhi haya thakili ya ukimwi.

Mhe. Naibu Spika, Hata hivyo bado Kamati yangu inaendelea kuiomba Serikali kufanya jitihada za makusudi kwa kutenga fedha za kutosha na fedha maalum kwa ajili ya mapambano ya maambukizi dhidi ya Ukimwi, kutokana na wahisani kuanza kusitisha misaada yao na kupelekea kusuasua kwa jitihada zinazofanywa na Tume dhidi ya mapambano dhidi ya maradhi ya Ukimwi. Kwani waswahili wana msemo usemao, “mtegemea cha ndugu hufa masikini”. Kwa hiyo basi tuanze kupanga mikakati ili kuweza kujitegemea wenyewe kwa kutenga fedha ndani ya serikali kwa ajili ya mapambano dhidi ya ukimwi, ili hii hatua tuliyofikia isije ikarudi ikawa mbaya kama hapo mwanzo.

HITIMISHO

Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue tena fursa hii kwa mara nyengine tena kukushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa mbele ya Baraza lako Tukufu. Pia naomba niwashukuru wajumbe wenzangu wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuweza kunivumilia na kunisikiliza kuwasilisha ripoti hii ya Kamati. Lakini vile vile kabla sijamalizia kabisa kabisa hotuba yangu Mhe. Naibu Spika, nitaomba unigaie japo dakika 5 alau na mimi niweze kusema yale niliyotumwa na wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kabla sijahitimisha hotuba yangu hii nilikuwa ninamuomba sana Mhe. Waziri pamoja na ufinyu wa bajeti ambao tuliokuwa nao na kwa kweli kama tulivyokueleza tulipokuwa kwenye Kamati. Tunasikitika sana na jinsi ya fedha za uendeshaji wa kazi zonavyokuwa haba na ukiangalia vile vile bajeti ya mwaka huu, Tume ya Mipango kwa kushirikiana na Waziri wa Fedha kama walivyosema wamejaribu kukata fedha, ili kuendana na hali halisi ya mapato ya nchi.

Sasa suala hili kwa kweli hii ni mipango ambayo tumeipanga sisi lakini kwa watendaji wetu kwa kweli bado tunawaacha katika wakati mgumu sana. Kwa hivyo kitu ambacho ninachokiomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwamba hivi sasa tunapitisha bajeti ya serikali na madhumuni ya kupitisha bajeti ya serikali sio kupitisha tu mafungu yaliyoletwa na kuyaachia serikali waende wakatumie. Lakini kazi yetu nyengine ambayo ni kubwa zaidi kuweza kuishauri ipasavyo serikali, kuweza kuibua vianzio vipya vya mapato.

Vile vile, suala la kuibua vianzio vipya vya mapato Mhe. Naibu Spika, sio kuachia tu serikali, hata na sisi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kujaribu kuangalia zile fursa ambazo tulizokuwa nazo ndani ya Zanzibar. Lakini vile vile, kuangalia na rasilimali alizotujaalia Mwenyezi Mungu ambazo zilizokuwepo nchini kwetu au fursa ambazo zipo katika nchi yetu bado hatujaweza kuzitumia vizuri.

Mhe. Naibu Spika, ingawa swahibu wangu, rafiki yangu kipenzi changu Mhe. Hija leo alituomba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuondoe fungu la safari za nje kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa kweli nadhani Mhe. Hija leo alipitikiwa sana na kwa sababu safari hizi za nje tunapokwenda tukirudi kwa kweli tunapata kujifunza mambo mengi na kwa kweli huwa tunaishauri ipasavyo serikali.

Kwa kiasi fulani naamini ndani ya mipango ya maendeleo ambayo hii tunayoipanga basi hata ule ushauri mbali mbali unaoletwa na wajumbe wa kamati au wajumbe mbali mbali wa Baraza, kwa kweli unasaidia sana katika

kuongeza mapato yetu kwa serikali, lakini vile vile kuweza kuleta ufanisi mzuri katika kazi zetu. Sasa haya yote yataweza kufanyika kwa vipi? Mimi nadhani kama leo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alipokuwa akihitimisha hotuba yake ya bajeti, alitueleza kwamba tuendeleze mshikamano na mashirikiano lakini vile vile kuweza kulinda amani yetu katika nchi yetu. Mhe. Naibu Spika, hata na mimi naungana na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kweli hali tunayoendelea nayo sasa si nzuri sana kwa jamii yetu.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wetu walikwisha kujenga matumaini makubwa baada ya kuanzishwa Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa. Walikuwa wanatuona tulivyokuwa tunafanya kazi kwa pamoja, tunashirikiana kwenye tatizo hatujali limetokezea kwa nani au upande gani. Tulikuwa tunashirikiana kwa pamoja, tunajenga hoja kwa pamoja na tunapoamua kuikamata serikali tunaikamata kwa pamoja. Na hata pale tunapoamua kuiachia serikali tunaiachia kwa pamoja. Lakini kwa malumbano ambayo yalioanza kwa kweli hali hii nadhani hatutowatendea haki wananchi wetu.

Sasa mimi nilikuwa naomba kwa sababu wanaoleta amani zaidi katika nchi ni wanasiasa na wanaovunja amani vile vile katika nchi ni wanasiasa. Sasa mimi nadhani sisi tusiwe wa mwanzo katika kuvuruga hii amani. Kwa hivyo naungana na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, hebu tujaribu kuji-*control.* Sasa hivi hasa tunapokuwa katika majukwaa yetu tuondoe jazba, tuzungumze zaidi mambo ya maendeleo ya nchi yetu. Naamini wananchi wetu ndio watakapotuamini zaidi, kuliko tukianza kulumbana, kuanza kusema huyu anatoka wapi, huyu kazaliwa lini, huyu kazaliwa tarehe ngapi, huyu mfupi, huyu mrefu.

Kwa kweli hii haitoweza kutusaidia. Wananchi wetu hawataki huyu kazaliwa wapi, wananchi wanataka fedha zijae katika mifuko yao. Wananchi wetu wanataka matumbo yao yajae, wananchi wetu wanataka watoto wao wasome, wapate elimu kubwa.

Kwa hivyo, mimi nadhani, tukiondoka katika msatari wa kuzungumzia maslahi ya nchi tukaanza kujadiliana mtu mmoja mmoja, nadhani tutaanza kupoteza muelekeo na kwa kweli tutamyumbisha hata Rais wetu kuweza kupanga mipango yake vizuri. Kwa sababu leo cheche moja ikianza, matokeo yake ndio chanzo cha kuripua moto mkubwa. Kwa hivyo, hili tu nilikuwa ninaliomba waheshimiwa wenzangu ule mzimu wa Bunge la Katiba hebu tuufute tuumalize, turudi katika Baraza la Wawakilishi tushirikiane, tuishauri vizuri serikali yetu na ninaamini serikali yetu pamoja na kwamba mengi hayajatekelezwa, lakini haya yaliyotokelezwa ni kwa ushauri wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa kweli tunashukuru.

Hata nidhamu sasa hivi ndani ya serikali Mhe. Naibu Spika, iko nzuri sasa hivi ndani ya serikali yetu, tofauti na pale mwanzo. Kwa kweli watendaji unawahisi hasa ukienda katika kamati ukitaka taarifa yoyote unaletewa na ukiwaambia sijaridhika na hili kaleteni wanakwenda, kwa kweli tulifika pahala pazuri sana. Lakini sisi tukianza kuondoka katika mstari huo basi na wao watajipweteka, kwa sababu anajua hata bajeti nikiipeleka kule sina wasiwasi, wakifika kule waheshimiwa badala ya kujadili bajeti wataanza kuchambuana wenyewe kwa wenyewe kama karanga, wao wenzetu wanapiga suti. Kwa hivyo, mimi nadhani turejeshe msimamo wetu wa utulivu na amani katika nchi yetu, hatua iliyokuwepo mbele yetu ni kubwa sana tunahitaji mashirikiano.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho kabisa namuomba Mhe. Waziri, nilipojaribu kuangalia hiki kitabu amejitahidi sana kusomesha, nimejaribu kuangalia katika viambatanisho hivi katika ile sehemu aliyoonesha ni maeneo gani ambayo ameamua kusomesha au wafanyakazi wao wameamua kuomba nafasi za masomo. Ukiangalia ukurasa wa 47 kwa kweli amejitahidi sana kusomesha vijana wetu, lakini sasa nilikuwa naomba vile vile kwamba kuna hawa madereva hasa wa mawaziri.

Mhe. Naibu Spika, katika nchi za wenzetu mfano Uganda au Rwanda waziri haendeshewi na dereva hivi hivi tu yeyote, lazima mtu ambaye ana cheo fulani katika jeshi la nchi ile. Kwa sababu waziri ni mtu mkubwa sana, waziri sio mtu wa kupata watu wababaishaji, kwa sababu waziri yule ndiye *engine* ya utendaji ndani ya wizara kwa ndani ya serikali. Sasa tulikuwa tunahitaji hawa madereva wetu hasa wa mawaziri wapatiwe zile nafasi.

Wenzetu Tanzania Bara sasa hivi kiko chuo kule cha *VETA* wanasomesha sana madereva. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri sisemi kama dereva wake hajamsomesha, lakini naomba hawa madereva aweze kuwasomesha.

Vile vile, kutokana na umakini wetu sasa hivi vikao vya Baraza la Mapinduzi wakati mwengine vinafika mpaka saa 8 za usiku, samahani kwa kutaja muda pengine sio, nazungumza ikianzia kufika saa 5 na kuendelea, basi hawa madereva wetu wanaporudi nyumbani wanakuwa na hali ngumu sana ya kurudi majumbani kwao. Kwa sababu gari

ya waziri dereva anatakiwa aiache kwa waziri na yeye arudi nyumbani. Sasa wanapokuwa na wao hawana usafiri kwa kweli ni hatari kwa maisha yao, lakini vile vile ukiangalia kipindi kama hiki cha mvua inakuwa hali sio nzuri sana.

Kwa hivyo, madereva hawa wasomeshwe lakini vile vile wapatiwe na usafiri wao ili wakishaweka yale magari ya Waheshimiwa Mawaziri waweze kupanda vyombo vyao vya moto. Na si vizuri dereva wa waziri kupanda baskeli. Leo dereva wa waziri akapandie baskeli, hili sio jambo zuri, angalau basi awe na vespa. Kwa hiyo, hili nadhani hata Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ingawa alikuwa kule katika Ofisi yake najua alinisikia, naamini madereva hawa wa mawaziri watapewa mafunzo na vile vile watapewa na usafiri.

Mhe. Naibu Spika, kabla hujaniambia niondoke nakushukuru sana kunipa nafasi hii, lakini vile vile nawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura kwa kuendelea kuniamini na ninaamini nawawakilisha vizuri, akiwemo dereva wa Mhe. Waziri. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, mimi sikuhizi nikichangia nimejipangia *special* kwenye bajeti hii niwe na *style* yangu ya kuchangia.

Mhe. Naibu Spika, juzi nilipokuwa nikichangia katika Bajeti ya Serikali nilisema kuwa kuna mawaziri wengine na makatibu huwa mizigo kwenye serikali, pamoja na wakurugenzi. Nasema hayo na nitaendelea kusema na nitakapofika pahali nitasema sasa mizigo yenyewe ni hawa ambao hawawatekelezei wananchi.

Leo nimpongeze sana Mhe. Waziri ambaye si mzigo kwenye serikali, nimpongeze sana Katibu wa wizara hii si mzigo kwenye serikali pamoja na wakurugenzi wake. Nina sababu zangu kwa nini nikasema hivyo. Mhe. Waziri ukimpigia simu saa yoyote anaipokea na saa yoyote ukimwambia jambo la ushauri anakubali, anakusikiliza na kutoa njia ya ushauri. Katibu yuko nje wewe mpelekee simu usione tabu kuliwa pesa yako tu, mnasikilizana na anakubali kutelekeza, hiyo inakuwa si mizigo na hivyo ndivyo inavyotakiwa. Lakini kuna wengine watafika idara yao nitakwambieni sasa huyu waziri mzigo wala sitoona tabu kumwambia. Kwa sababu lengo ni kuwasaidia wananchi na ndio maana tumeletwa hapa tuwasaidie wananchi katika shughuli zao za kimaendeleo.

Mhe. Naibu Spika, jambo la kumsifu waziri wangu kusimamia jambo la walemavu ni kitu cha sifa kubwa sana na katibu wake, si kitu cha masihara niseme ukweli. Kwa sababu hawa wenzetu ni watu ambao kusema kweli bado hatujafikia *level* ya kuwasaidia katika maisha yao. Hili niseme ukweli Mheshimiwa. Nilikuwa nikiwakera sana Mhe. Waziri na katibu lakini *Wallahi* hawakunipuuza hata dakika moja kwa sababu wanajua suala la mchango wa walemavu ni suala kubwa na ni nyeti, hili lazima tuliseme. Tuna mapungufu makubwa sana kwa ndugu zetu hawa kutowatendea haki, hili lazima tuseme, tuna mambo mengi tu.

Nikiuliza hata wenzetu maana na wao wana michezo yao, lakini nikikuuliza kiwanja kiko wapi cha michezo yao hatuna, tunawatendea haki hapo? Tuna mambo ya biashara hata siku moja hatujasema kuwa tutenge eneo maalum la kuwasaidia hawa ndugu zetu kwa kufanya biashara na kutafuta rizki zao. Kama tunavyojua upungufu wao kwenye viungo hakuna hata kimoja tulichotenda, hatukuwatendea haki.

Halikadhalika hatujawatafutia mabenki ambayo yatawawezesha wao kutokana na ujasiriamali wao, kutokana na hali zao hatujawatafutia hili suala. Sasa mimi naomba sana Mhe. Waziri wangu weka sifa na hili, katibu weka sifa, ukiondoka ofisi hii ukienda ofisi nyengine Mwenyezi Mungu akujaalie basi huku unaondoka na jina zuri na ndivyo tunavyotaka mawaziri wawe na sifa za aina hiyo, sio wachaguliwe kuwa mawaziri tu au makatibu na wakurugenzi tu. Waweke sifa kwenye mawizara yao nini walichokifanya walipoondoka pale, hivi ndivyo tunavyotaka Mheshimiwa, lakini mpaka leo bado.

Mhe. Waziri naomba niipambe hii bajeti yako, hawa watu ukija unambie kwamba tayari nimeshazungumza na benki ya *PBZ*, nimezungumza na *NMB*, tuwatafutie nyezo hawa ndugu zetu. Ni asilimia ndogo sana utawakuta wafanyabiashara hawa wanaopata Mfuko na wako wengi sana, hata tukienda kwenye kazi tupige hesabu tuone wangapi wamepata kazi, anahangaika masikini Mkurugenzi wao yule mama shujaa, shupavu na ndio maana nikasema wakurugenzi wengine si mizigo kwenye serikali mmoja ni yule si mzigo. Ni mwanamama jasiri. Lakini bado kutokana na hali yake hatujamtendea haki. Naomba sana Mhe. Waziri tuweke *plan* ya kuwawezesha.

Tumetembea nje ya nchi tunaona wenzetu jinsi gani wanavyoenziwa, nchi za wenzetu wanaenziwa vizuri hata katika majumba wanatengenezewa majumba ambayo yanaridhisha kwa kupanda kiurahisi, lakini sisi tunajenga majumba ya kisasa hatuwatengenezei njia ya kupita wao kirahisi tunakusudia nini?

Mimi sidhani leo yule Mkurugenzi wangu kama yupo hapo juu na yeye anataka kuja kusikiliza bajeti yake, lakini sidhani kama kafika, hamna *lift* jumba hili la Baraza la Wawakilishi, hamna njia ya kupita kiti kile, humu ndani pengine masikini ya Mungu kakaa nje anasikiliza kwenye spika, mazuri hayo? Tunakuwa hatuwatendei haki, kwa kweli haridhiki lakini lisilo budi hufanyika.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana Serikali Kuu akiwemo mwenyewe Makamu wa Pili wa Rais, naomba sana na yeye aingie majonzi kabisa na wenzetu hawa walemavu, awe *serious* na yeye kwa sababu ni jukumu kubwa hata kwa Mwenyezi Mungu sio kwenye serikali tu, ni jukumu kubwa sana wale wenzetu kuwatupa, kutokuwashughulikia.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba sana ahakikishe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hawa watu wanapata maeneo na wao wakajidai na michezo yao. Kwa sababu wanakwenda nje wanarudi na medali lakini medali zao hatuzifanyi zikatambulika sijui kwa nini, hata hawafanyiwi sherehe na *Alhamdulillah* ukija kwenye mpira wanacheza vizuri. Hamjaenda nyinyi kutizama mipira yao, wanakwenda kwenye riadha wanacheza vizuri lakini basi tu, hatujawatafutia kiwanja.

Mhe. Naibu Spika, naomba katibu wangu anisikilize ni mzuri, kamanda mzuri na waziri ni mama jasiri, cheo alichopewa kimefika pahali pake. Kwa hivyo, namuomba sana akubali hili suala tuone jinsi gani bajeti inayokuja anieleze kwa upeo na kwa mbwembwe kabisa kuwa wamekamilisha katika *item* hizo nilizotoa mimi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuzungumzia ndugu zangu hawa na kuwatetea kwa nguvu zote na sitosita hata siku moja kuwatetea. Hii nimeamua kama hatukufanya hivyo basi kila siku tutakuwa tunawarudisha nyuma kimaendeleo na wanajisikia unyonge masikini ya Mungu. Kuna watoto wazuri wanasoma mpaka vyuo vikuu sasa hivi. Kuna mtoto kule Kwahani anaitwa Rashid ni mlemavu wa mguu mmoja, lakini anacheza mpira vizuri na ni msomi mzuri tu bado anachukua vitu huko. Sasa nataka nihakikishe na yule naye sasa hivi anatia suti anafanya kazi kama tunavyofanya kazi sisi. Naomba sana hilo uweze kufikisha.

Mhe. Naibu Spika, nije katika Tume ya Madawa ya Kulevya. Kamanda wangu hapa Mhe. Hamza Hassan Juma aligusia, mimi siku moja nilisema hapa pengine sisi Wawakilishi tunashiriki masuala ya madawa ya kulevya tusikatae inawezekana. Nilisema kuwa tushirikiane lakini hatujawa tayari sisi kushiriki hilo suala. Kwa sababu pengine ndio *activities* zetu, sisi Waeheshimiwa kwa nini tusiseme na kama kweli tunakuwa hatushiriki suala hili kwa nini lisiishe. Kamanda Hamza Hassan Juma kasema hapa kinchi kidogo tu ukikifanya hivi umekitia mkononi hata masaa hayatimii. Vijana wanakufa, vijana wanateketea, vijana wanaingia katika dimbwi la wizi, vijana tunawakosa katika nguvu kazi kutokana na masuala haya na nitakupeni ushahidi.

Narudia tena suala la Uwanja wa Ndege wala sitolionea haya kulisema, nimejitolea kabisa nimeshika msahafu hapa, katibu wangu aliniapisha kuwa niseme kila nitakaloliona na nilindwe kwa mujibu wa Sheria na Katiba na haya sasa ndio ninayasema.

Mhe. Naibu Spika, tukijiuliza kamera kwa nini siku ile ikawa mbovu? Inakuwaje Mheshimiwa kamera ya *International Airport* Zanzibar kwa siku ile iwe mbovu, *why*? Hebu tujichunguze ndio yale aliyosema Kamanda Hamza Hassan Juma kama hakuna wakubwa waliohusika hapa. Lakini mizigo ile amepewa mfanyakazi wa mle mle wa shirika lile la Mamlaka ya Uwanja wa Ndege ndiye aliyebeba mizigo ule. Itafika katika wizara sasa nikifika tu namtoa paka kwenye gunia namtaja huyo, humu narashia rashia tu kwa kuwa hii tume naipenda, naipa nguvu ione na sisi jinsi gani tunasaidia. Ni mfanyakazi bwana aliyebeba mabegi yale asikwambie mtu, akenda akayaweka pahali anangoja muda ule ufike ili aweze kuupitisha.

Mhe. Naibu Spika, Mwenyezi Mungu bwana si Mzee Athumani ile kuzubaa zubaa sasa watu wa *ZAT* ndio wamekuwa wao ndo kafara, ile kusema jamani mizigo ya nani ile, vile vidole vinaonekana kuonesha hivi kumbe imekuwa kafara wao sasa, wamenyang'anywa vitambulisho wameambiwa wasifanye kazi mle ndani sababu gani, hatujiulizi? Kitu kinaonesha wazi hicho wale *ZAT* inahusiana wapi na wapi na masuala ya mabegi, kwenye uwanja wa ndege muna *screens* zile ambazo zinapitishiwa mizigo, ina maana siku ile ilikuwa mbovu? Nauliza Mhe. Naibu Spika?

Sasa nataka niwaambie mama yangu yule mhusika wa tume asikudanganye mtu na askari wanahusika na wao hakuna kuficha. Askari wetu na wao wanahusika, namuomba sana Kamishna asilegee sana, wasininunie askari lakini nasema na wao wanahusika kuirahisisha kazi ya uuzaji wa madawa ya kulevya, hiyo tuseme ukweli tusifiche. Mtaunda tume zaidi ya 50 na mtatoa pesa tele za wavuja jasho wetu, wana kazi huko mitaani. Lakini mianya hii kama hatukuiziba na tukaikamata kisawasawa hatufiki pahali watateketea tu watoto wetu, watakufa kutokana na hii mianya mibaya.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana Serikali Kuu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wale vijana naomba wakarejeshewe vitambulisho vyao wasinyanyaswe kwa kuwa wametoa siri ya kuwa mabegi yale pale mnayaacha, warejeshewe Mheshimiwa tusiwahukumu bure, imekuwa tabu jamani. Ndio maana tukasema Wakurugenzi wengine mnakuwa mizigo katika utendaji wa kazi hiyo lazima tuseme, hiyo ndio mizigo yenyewe unafikiria vipi. Unakwenda kutesa watu waliokuwa siwo na waliokuwa ndiwo mnawadhibiti.

Kuna watu mle ambao kazi yao wao wakikunyang'anya kitambulisho tu umekwenda na maji, kuna watu kama watano hivi wamekuwa kama ziraili wakikutoa roho ndio basi hairudi hiyo. Hawa watu watano wapo wanaringa katika maeneo ya Uwanja wa Ndege kwenye mamlaka, unakwenda na maji ikiwa ndilo, ikiwa silo unanyang'anywa, lakini twende kwa mujibu wa sheria, mtu kwanza ukimnyang'anya kitambulisho mpe onyo, basi tunabena tu sheria.

Mhe. Naibu Spika, naomba hawa watu watano leo sikuwataja nitawataja hiyo siku ya wizara yao, nitamwambia mwenyewe waziri watu wako hawa hapa sioni tabu kumwambia mtu ukweli ulivyo, wakati umefika wa ukweli na uwazi.

Mhe. Naibu Spika, leo sitokuwa na mchango mkubwa sana, kwa sababu wizara hii haina ubaya na mimi, sikufichi. Naendelea kwanza dakika zangu bado.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa una dakika tano.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Haya nakubaliana na wewe. Niende katika kitengo changu ambacho nakipenda sana cha Mazingira. Kama tulivyosema tayari zinakuja sheria hizo na kanuni zake za kumuwezesha Mkurugenzi wangu sasa hivi awe na meno na yeye. Kwa kweli tuliliona na nilikuwa nalipigia debe sana, ninashukuru.

Mimi nashukuru kuwa ninayoyasema kumbe baadhi ya viongozi, mawaziri ndio maana nikakwambia sio mzigo wanakuwa wanakubali. Suala hili nilisema sana, sheria za mazingira zibadilishwe zimepitwa na wakati. Leo chuma hicho hapo kiko njiani kinaletwa si mzigo hawa wanatufahamu, wananifahamu lugha yangu, si mkali lakini nasema ukweli, mambo mengi nimesema. Nimedai Wizara ile ya Vikosi Maalum imepatikana, sikupewa mimi kapewa mwenzangu Mhe. Haji Omar Kheir lakini ndio inavyotakiwa. Mimi kazi yangu kupiga debe wapewe watu wengine lakini mimi sina tatizo na Makamu wa Pili huyo hapo ananiona, wala hanigaii hata siku moja. Sasa hiyo ndio hali halisi, nafikiri nimalizie.

Mhe. Naibu Spika, leo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, alisema jamani amani tuitunze. Mimi nataka kuwaambia ndugu zangu huyu Ndugu yetu Mhe. Tundu A. Lissu aliyepita akasema, akafufua maiti waliokufa, si vizuri. Kwa sababu wale wenzetu wanakuwa na vijukuu, watoto wao, si vizuri kuwanadi kwenye viriri, sijui nani kauliwa, nani kauliwa, kwa kweli hii haihalisi.

Mwambieni Mhe. Tundu A. Lissu kama hana kazi akafanye kazi nyengine asitugombanishe. Mimi sisemi mambo hayo sipendi sana kwa sababu nina akili yangu, lakini na yeye asipite kwenye viriri akatuendeleza kutugombanisha, ndio sasa anafika Mnadhimu wangu anasema kuwa analeta hoja , inamjia jazba mtu kutokana na hali halisi ilivyo.
Mhe. Naibu Spika, naomba sana iwe ndio mwanzo, ndio mwisho kusikia, kama akisema kama niko karibu, mimi nitamrukia kichwa kwa sababu hatutaki kudhalilishiwaa maiti waliokuwa wameshapita kwa mujibu wa sheria. Huwezi ukadhalilisha, akaseme Singida uko sio hawa awataje wale watu wengine mbona hawataji....

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa Malizia.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Namalizia Mhe. Naibu Spika, ama zake ama zangu nikimsikia siku ya pili kwenye kiriri mimi nitamtia vichwa, anatuudhi si vizuri kama yeye kashindwa sheria basi akatie vitabu mkononi. Sio afanye mambo ya kitoto haifai bwana. Kama wameshakufa tuwapigie *fat-ha* tuwarehemu.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono asilimia mia kwa mia na wananchi wangu wa jimbo la Kitope shukrani. (*Makofi*)

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu katika Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, mimi naanza kwa kusema kwamba siungu mkono hotuba ya Bajeti hii kwa sababu nitamtaka Mhe. Waziri aje kwanza anifahamishe kwa kina juu ya suala la mradi wa Tabia Nchi ambao upo katika eneo letu la Jimbo la Kikwajuni, tunaanzia. Lakini pia linaelekea na limepakana na ndugu yangu Jimbo la Mji Mkongwe. Mradi ule ulisimamiwa na Mbunge wangu wa Jimbo la Kikwajuni na baadae ukapata mitihani ambapo katika kipindi cha miaka mitatu mpaka minne sasa hivi tumekuwa tukilizungumzia suala lile na halijapatiwa ufumbuzi.

Kitu cha kushitusha zaidi ni pale niliposikia baadhi ya viongozi na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakizungumzia juu ya suala zima la fedha zile za mradi kwamba zimeingizwa kwa upande wa Zanzibar na wakatamka kwamba pesa hizi zimepelekwa kwenye mradi wa Jimbo la Kikwajuni. Sasa mimi naomba leo nipate taarifa zitakazonitosheleza juu ya suala hili ili hatimae niweze kupitisha bajeti hii.

Baada ya hatua hii na *Reference* tu ukitaka Mhe. Waziri kikao cha Bunge tarehe 12 ndio kilifanyika kikao hicho na magazeti tulikuja kuyasoma ya tarehe 13 hususan gazeti letu la *Daily News*, taarifa hizi zimo kwa vizuri zaidi. Nimejaribu kutafuta *Hansard*, lakini mpaka dakika hii naambiwa kuwa inakuja inakuja sijaipata na nimejaribu kuangalia kwenye mitandano mote sijaiona, kwa sababu bado hawajatia ule mpango mzima wa shughuli zao za kibunge kwa kipindi hiki kinachoendelea.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaendelea mbele zaidi nachukuwa nafasi kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais kwa hotuba yake mwanana na murua aliyokuja kuitoa leo wakati anafanya majumuisho katika Wizara yake, na kuomba kwamba hali ya amani na utulivu iendelee katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mimi napenda kumuahidi tu penye nia pana njia na *inshaallah* tukiamua tunaweza, Mwenyezi Mungu atuwezeshe amani na utulivu katika nchi hii uendelee, umoja na mshikamano uzidi ili mambo yetu yaweze kwenda vizuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo sasa nakwenda katika ukurasa wa 21 wa kitabu ambacho Mhe. Waziri alikuwa amekisoma. Mhe. Waziri hapa amezungumzia katika kifungu cha 56 suala zima la Tume ya Kuratibu na Kudhibiti Madawa ya Kulevya na hapa vile vile pale nilipunguza shilingi mia kule kwenye fungu la kwanza. Lakini hapa sasa nitakuja kupunguza shilingi moja ili ziwe shilingi 101 ambazo nitazipunguza katika Wizara yako Mhe. Waziri, mpaka unipe maelekezo ya kina juu ya suala zima la Udhibiti wa Madawa ya Kulevya ndani ya visiwa vyetu vya Zanzibar.

Mhe. Waziri katika kifungu cha 107 umeomba hapa tukuidhinishie fedha ambazo zitasaidia kuhakikisha kwamba utaendeleza mapambano zidi ya biashara na matumizi ya uingizaji na usafirishaji wa Madawa ya Kulevya Zanzibar. Lakini kinachonisikitisha kuona kwamba baada ya Serikali Kuu kwisha kufanya juhudi za kutafuta angalau Chuo kile cha kuweza Kudhibiti haya Madawa ya kulevya. Lakini sijasikia utaratibu na kuona kwamba Chuo kile kinafanya kazi vipi, pamoja na kunusuru zile fedha nyingi ambazo tulikuwa tumezitoa pale na kuona kwamba tunasaidiana, ili shughuli ziweze kwenda vizuri na Madawa ya Kulevya haya yaweze kudhibitiwa.

Nikiondoka hapo sasa Mhe. Naibu Spika, nakwenda katika ukurasa wa 32 wa kitabu cha Mhe. Waziri ambacho amekisoma katika namba tisa ya kirumi (ix) hapa juu, kuna neno linasema kwamba kuandaa mpango wa mawasiliano juu ya sera ya watu wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, kwa uono wangu mimi tulisema kwamba taratibu za magari haya ya daladala na mambo mengine tuyaondoe pale Darajani kutokana na mazingira, lakini zaidi ilikuwa waliangaliwa wanafunzi ambao wamekuwa wanapata mtihani pale katika kukaa maeneo yale.

Sasa ninachoshangaa mimi Mhe. Naibu Spika, kama kuna wanafunzi ambao wanataka uangalifu wa hali ya juu, kama kuna wanafunzi wanataka kuangaliwa kwa maslahi yao na hali zao walizonazo basi ni wanafunzi ambao wanasoma Skuli ya Kisiwandui ambapo kuna wanafunzi wana maumbile maalum.

Kutokana na mazingira ambayo yako pale kwa sasa imekuwa ni pahala ambapo pana fujo, pana bughudha, pana kila aina ya vitu ambavyo vinaweza kuhatarisha maisha yao wale watu ambao wana matatizo kama yale ambayo Mwenyezi Mungu amewajaalia nayo. Sasa nataka kuona Mhe. Waziri atakapokuja hapa anakuja kunifahamisha kwa kina ni namna gani wametayarisha mipango yao kuhakikisha kwamba wale watu ambao wana maumbile maalum wananusurika vipi na kadhia pamoja na matatizo ambayo yanaendelea kujitokeza, likiwemo suala la watoto wa Skuli pale kugongwa na magari kila mara kutokana na msongomano ambao uko katika Skuli ya Kisiwandui.

Nikiondoka hapo Mhe. Naibu Spika, ninakwenda katika kitabu kikubwa. Katika buku letu kubwa hili kuna maeneo ambayo nilihisi kidogo Mhe. Waziri atakapokuja hapa anisaidie ufafanuzi. Katika buku kubwa hili, katika kifungu cha 0401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti katika *bullet* 263100 kifungu kidogo ukurasa wa 47, 263166 kumeombwa pesa hapa ruzuku ya shilingi sabini na sita milioni mia sita na arubaini na tano. Fedha hizi hazikuombwa mwaka 2011/12, 2012/13, 2013/14 lakini zimeombwa kwa mwaka 2013/14 sijui kuna utafiti wa namna gani ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie kutueleza, ni utafiti gani ambao utafanyika katika kipindi hichi.

Kama hiyo haitoshi ukurasa wa 48 fungu 0501 Uendeshaji wa Utumishi kifungu kidogo 220107 kuna fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa kanda za Santuri. Mhe. Waziri sijui Santuri mpaka leo tungali nazo, lakini santuri hizi hazikununuliwa katika kipindi cha nyuma kutoka mwaka 2011/2014 isipokuwa mwaka 2014/15, zimeombwa shilingi milioni mia moja na ishirini na tatu kwa kazi hii. Ningeomba kupata ufafanuzi ili niweze kuruhusu fedha hizi ziweze kutumika au zisite.

Pia, kuna ongezeko kubwa vile vile katika ukurasa wa 49 kwa kifungu namba 220200 viburudishaji. Mwaka jana ziliombwa milioni 8039,000/= lakini mwaka huu kumeombwa kumi na mbili milioni na thamanini na tano elfu. Je, hawa wageni wameongezeka zaidi? Naomba kupata ufafanuzi vile vile.

Eneo jengine ni lile Mhe. Hamza Hassan Juma alilizungumza kwa hiyo sitolirejea tena, lakini zaidi tukija katika ukurasa wa 54 kifungu 0901 Idara ya Mazingira *bullet* namba 211116 Posho la Vikao vya Kamati. Mwaka 2012/13 ziliombwa laki nne na ishirini elfu. Lakini 2013/14 hapakuombwa kitu, cha kushitusha zaidi 2014/15 zimeombwa milioni 27, 360,000/= ukiangalia hili ongezeko ni kubwa mno kuhusiana na shughuli ambayo mwanzo huku kwa namna ilivyokuwa imeanzia, ningeomba kupata ufafanuzi zaidi.

Tukiondoka hapo tukienda kwenye ukurasa namba 57 kwenye kifungu namba 2101 Idara ya Watu wenye Ulemavu napo vile vile kwenye vinywaji hapa na viburudisho kifungu kidogo 220201 mwaka 2011/12 ziliombwa 2012/13 ziliombwa 779,000/= 2013/14 ziliombwa shilingi laki nane. Lakini mwaka 2014/15 zimeombwa 7,775,000/=. Hili ni ongezeko kubwa sana ningeliomba kupewa ufafanuzi wake.

Kama hiyo haitoshi kuna maeneo haya mengine ambayo bora tuyawache lakini nayo kuna ongezeko kubwa vile vile katika ada ya ushauri wa kitaalamu chini kabisa huku kabla hujaingia *bullet* 220600. Kuna miaka ya mwazo yote hakuna ada ya ushauri wa kitaalamu. Lakini mwaka huu zimeombwa milioni 20 kwa ada ya ushauri wa kitaalamu na vile vile Sera ya Sheria kumeombwa milioni 9. Katika miaka ya nyuma huku hakuna labda 2011 zimeombwa pesa kidogo.

Tukiondoka hapo sasa tunakwenda katika hili eneo nililoona lina uzito zaidi ukurasa wa 59 katika kifungu 220105 Gharama za Vifaa vya Uchapishaji mwaka jana 2013/14 ziliombwa 1,800,000. Lakini mwaka huu kuna ongezeko kubwa sana 2014/15 kumeombwa milioni 25,900,000/=. Ukiangalia hili ongezeko ni kubwa sana.

Kwa hiyo, haya mengine naomba bora nimwachie Mhe. Waziri ili kwanza aweze kutujibu kule na baadae tuweze kupata ufafanuzi wa maswala haya tuweze kwenda vizuri na tuweze kumpitishia bajeti yake endapo atatupa majibu ambayo yatakuwa yanatosheleza.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelekezo hayo, narejea tena kwamba sitounga mkono bajeti hii mpaka nipate maelekezo ya kina juu ya suala linalohusu Jimbo la Kikwajuni. Baada ya maelezo hayo nashukuru sana.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukuwa nafasi hii kukushukuru kwa dhati kabisa kwa kupata nafasi hii ya kutoa mchango wangu kwa Makadiro ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais iliyosomwa na dada yangu Mhe. Fatma A. Fereji.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunipa pumzi na kuweza kuwepo jioni hii katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Naibu Spika, nichukuwe nafasi hii vile vile kumpongeza Mhe. Waziri kwa bajeti ambayo aliyosoma pamoja na Mwenyekiti wa Wenyeviti Mhe. Hamza Hassan Juma kwa bajeti ambayo imeleta ufasaha mzuri, maelezo ambayo yanafahamika na nimshukuru vile vile Mhe. Waziri na watendaji wake katika kazi ambayo waliojiamini na kutuletea mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa ningependa kumshauri dada yangu tena namuheshimu sana pamoja na watendaji wake, Katibu Mkuu pamoja na viongozi wake. Ningependa kumshauri pamoja na wenzake hili ni Baraza tumekuja hapa kwa ajili ya wananchi ndio waliotuleta mbele ya Baraza lako. Kwa hivyo, ningelimshauri Mhe. Waziri atakapokuja awe na hekima na busara. Ningemlimshauri kuwa mbunifu na sio kama wengine wanakuwepo mara nyengine kutupa tupa tu maneno, naamini yeye si kawaida yake naamini ni mtu mwenye hekima na naamini kwa sababu mwaka jana tu Mwenyezi Mungu kamjaalia ametokea katika nafasi nzuri ambayo na sisi tunaomba mwakani tuelekee huko huko Makka. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ningelipenda kuingia kwenye *page* 21 mpaka 27 halafu nitakuja kwenye *page* ya 37. Nafikiri lazima sisi Zanzibar tujiulize hasa suala la haya Madawa ya Kulevya, Tume ya Kuratibu, Udhibiti ya Madawa ya Kulevya.

Mhe. Naibu Spika, kazi hii ni yetu sisi sote na kazi hii sehemu nyingi ambazo zinakataza katika suala zima la Madawa ya Kulevya. Lakini nataka niseme kwamba hii Wizara ina kazi kubwa sana na hii Wizara hata ikiwa tutakuja kuwaambia tu Madawa ya Kulevya hawa sio wakamataji na uzuri wa jambo hili la Wizara hii ni kupewa mashirikiano. Sasa ningemshauri Mhe. Waziri vitu ambavyo havijui au vitu ambavyo hapati mashirikiano vinamzonga pamoja na watendaji wake.

Mhe. Naibu Spika, ningelimuomba kwa uwezo wa Mwenyezi asilibebe yeye kama Waziri kuja humu ndani ni bora akasema limeliwa kivuli, sikupewa mashirikiano watendaji hawakunipa mashirikiano na akataja hizo taasisi zinazohusika. Kuliko Mhe. Waziri kuja kubeba jambo ambalo la kuwambia watendaji, watu ambao si waaminifu, watu ambao hawako kwenye wizara yake. Kila anapotaka msaada kwenye Wizara zinazohusika kwa sababu Wizara hii si peke yake inayofanyakazi hiyo na Wizara hii ina Wizara nyingi ambazo zimeguswa na mambo kama haya.

Sasa kama asipopewa mashirikiano yeye si mkamataji wala yeye si mtu anaekwenda kuhukumu. Kwa hivyo, ninachoomba Mhe. Naibu Spika, Madawa ya Kulevya lazima tuwe wakweli, tuwe wakweli kwamba hili suala lipo linafahamika Serikali zote zilikuwa zikikemea, hata dini zote zinakemea mambo kama haya.

Lakini Mhe. Naibu Spika, lazima sisi tuwe waaminifu, tuwe wakweli. Nitatoa mfano uliokuwa hai na ushahidi ninao. Aliyekuwa Mhe. Waziri Kiongozi awamu iliyopita Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, aliita watendaji asubuhi saa 5:00 kwenye Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi lile la zamani. Basi unafanywa utaratibu wa zile dawa za kulevya kukamatwa Uwanja wa Ndege, pale pale mle ndani jamaa wanatuma *message* "Bwana kuna hili Waziri Kiongozi katuita ngoma ipo tayari imesharipuka". Mle mle ndani kwa watendaji. Tena akija muulizeni Mhe. Shamsi Vuai Nahodha. Mimi baada ya nusu saa nikawasiliana nae Mhe. Shamsi, nikamwambia Mhe. Waziri Kiongozi Kamati uliyoiita wewe Barazani kama nusu saa iliyopita ngoma tayari huko imeshachezwa, watu wameshatawanyika yale madawa hayapo tena. Nikamwambia alikuwepo mtu fulani moja, mbili, watatu, wanne, watano.

Sasa Mhe. Naibu Spika, tusiingie kwenda kutafuta *Sober House*, tutajenga *Sober House* nyingi sana kama hatukuwa wakweli. Mimi nashangaa Serikali hii ishindwe kutekeleza mambo kama haya. Maana yake pakitokea jambo Mawaziri wote hukusanyika, jeshi zima hukusanyika kwenye sehemu ile, lakini baadae panakuwa hakuchukuliwi hatua yoyote. Tunasema sijui ushahidi, sijui nini, kitu kipo wazi.

Mhe. Naibu Spika, nikwambie basi ile mizigo iliyokuwepo *Airport* iliyokamilika ambayo ilikuwa isafirishwe haijasafirishwa ni jambo moja tu. Kwa bahati nzuri Mhe. Naibu Spika, siku ile *IGP* alikuwa anakuja Zanzibar na *helicopter* yake, sasa ile *mission* walipoona *helicopter* imekuja wale jamaa walifikiria tayari ile *information* imeshatoka ndio wakaacha ile kutokana na kunusuru *IGP* kutua pale.

Unajua mambo yetu ya Zanzibar, akija *IGP* basi askari wote wapo *Airport*. Basi ile ndio iliyotunusuru sisi watu wakaacha mizigo wakakimbia. Ule ndio ukweli ulivyo Mhe. Naibu Spika, na laiti isingekuwa *helicopter* ya *IGP*, ile ngoma ilikuwa tayari.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Kiongozi alisema na ninayo humu ushahidi wake, akasema madawa ya kulevya yanapitishwa Uwanja wa Ndege *VIP*. Huyo hapo yuhai kaka yangu, namheshimu sana. Kasema ndani ya Serikali madawa ya kulevya yanapitishwa *VIP*, tunakuja hapa tukisema kwamba hili jambo letu basi liwe letu. Kwa hiyo, mimi ninachosema kwamba hatukuwa *serious.*

Leo nasikitika kwamba mwaka uliopita katika sehemu ya Madawa ya Kulevya wenzetu waliomba milioni 160, *they got only 25%.* Yale makadirio ya kuuondosha ubadhirifu katika nchi hii, wenzetu kwa nia nzuri wameomba milioni 160 walichopata ni milioni 40. *Are we serious?* Halafu Mhe. Naibu Spika, hili suala ni la vitendea kazi. Hili suala la kushirikiana. Kwa hiyo Mhe. Naibu Spika, mimi naona tuzungumzeni ukweli kwamba vitu kama hivi na hasa Mhe. Waziri sasa hivi katika tatizo tulilonalo, akienda pale ataambiwa CUF huyu. Huyu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, hapa alikuja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Lakini akiwaendea hapati mashirikiano huyu dada yangu, hakika hiyo. Yeye anaonekana kama ni mtu ambaye sie.

Sasa mimi nafikiri lazima sisi watendaji na viongozi tuwe *serious*. Walikwenda Mawaziri pale, vitu vyote vipo, hakuna mmoja aliyepelekwa kwenye vyombo vya sheria, wanasema uchunguzi bado unafanywa. Sasa mimi ninachoomba hili suala hapa naona sasa Wizara inakuja inatafuta bilioni 1.4 eti kujenga kwa kuwahifadhi hawa walioathirika na madawa ya kulevya. Tutakuja kujenga majengo 10 kama hatujatafuta mzizi. Kwa sababu tuna *problem* hiyo tufanye *solution,* na baada ya *solution, what is next?* Ina maana sasa hivi tunalea *Sober houses!* Vijana wetu wataharibika kwa sababu hawa mapapa hatujawafanyia kazi kubwa.

Mhe. Naibu Spika, unakwenda kumkamata mtu Miembeni na peremende moja anakwenda hivi, huyu sie.

Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi ninachotaka kuuliza Serikali lazima itizame, sioni choyo kila mmoja kajaaliwa, lakini mtu ghafla tu kaibuka na rasilimali ya mabilioni. Ukitizama leseni hana, *income tax* hana, kitu cha kushangaza, hana hata *tin number*, ana majumba ya mabilioni. Serikali inakaa kimya tu! Ina maana huyu anakuwa *supported*, ana watu anawalinda/wanamlinda. Ndio kama alivyotwambia Waziri Kiongozi, anaita *message* pale pale yumo ndani inatumwa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma aliposema *VIP* hakubahatisha. Sasa mimi naona kwamba haya mambo tusikimbilie tu katika vitu vya kufanya, tutafute kwa kweli tuwe na hali ya udhibiti. Lakini hali ya udhibiti tunahitajia vitendea kazi.

Mhe. Naibu Spika, mimi navipongeza vyombo vyote vya dola kwa kazi nzuri, lakini hizi kazi zinahitajika vitendea kazi. Sasa kama leo kuna Mkurugenzi wa Dawa za Kulevya hata hiyo gari hana, ana baiskeli. Mhe. Naibu Spika, lazima tuwe wakweli tuwe na mambo ambayo tunaweza tukaona njia gani, kunatokea *mission* mafuta hana lita 40 anacheleweshwa. Sasa mimi nafikiri lazima kuwepo na kamati ya mashirikiano.

Kwa hiyo, Mhe. Waziri nakuheshimu sana, ninachokuomba ukija hapa sisi ni wenzako tutakusaidia, mimi sina tatizo na bajeti hii kabisa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini. Nina asilimia 110 mimi kwa bajeti hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Lakini Mhe. Waziri nakuomba usiwalinde, kwa sababu ya kuwalinda hupati mashirikiano, sema humu ndani kwamba bwana naliwa kivuli, nikiambiwa naambiwa sie, sema tutakusaidia sisi. Kuliko Mawaziri mnabeba watendaji inakuwa mzigo halafu tunakuwa hapa tunalaumiana. Ndio mimi nimempongeza sana leo kwa historia yangu katika familia yangu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar amekuwa mkweli.

Siku moja kulikuwa na jeshi la Bibi Aisha, upande wa pili kulikuwa na jeshi la Sayyidna Ally. Sasa wafuasi wakamuuliza Sayyidna Ally tuelekee wapi, huku kuna jeshi la Bibi Aisha, hapa kuna jeshi la Sayyidna Ally tuelekee

wapi. Sayyidna Ally akajibu hivi, elekeeni palipokuwa na haki ya kweli. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini, ahsanteni sana.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Naibu Spika, na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia jioni hii kuwepo hapa katika kutekeleza majukumu yetu. Pia, nakushukuru wewe kunipa nafasi ya mwisho kwa jioni hii ya leo ili na mimi niweze kutoa mchango wangu mfupi katika hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niendelee kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na watendaji wake wa Wizara kuandaa kitabu hiki kizuri ambacho pia nae alikiwasilisha kwa ufasaha wa hali ya juu kabisa, na mwenyewe umempongeza kwa kuutumia muda vizuri.

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu wa kwanza uende katika mchango wa jumla wa uingizwaji wa fedha katika Idara mbali mbali za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, kwa haraka haraka inaonekana kwamba ofisi hii uingizwaji wa fedha ni mdogo sana; ni mdogo kiasi ambacho kutokana na mambo mbali mbali ambayo yanahusika na utekelezaji wa majukumu ya ofisi hii, basi ofisi hii inaweza kushindwa kutekeleza majukumu yake kiufanisi.

Mhe. Naibu Spika, nikenda na mfano wa Ofisi ya Faragha. Ofisi ya Faragha hadi Machi 2014 imeingiziwa fedha kwa asilimia 26 tu. Ofisi ambayo ina majukumu mbali mbali yanayohusiana na ofisi hii ya Makamu wa Kwanza.

Mhe. Naibu Spika, nikienda katika Idara ya Mipango, Sera na Utafiti hadi Machi 2014 imeingiziwa fedha asilimia 27 tu kati ya fedha ambazo zimehitajika kuingizwa katika Idara hii. Muingio huu wa pesa ni mdogo kiasi ambacho watendaji wanaweza kushindwa kutekeleza majukumu yao kama inavyotakiwa.

Mhe. Naibu Spika, nikienda katika Idara ya Mazingira; hii kidogo imeingiziwa asilimia 44, niseme kwamba kiasi fulani labda inakuwa haijambo.

Mhe. Naibu Spika, nikiachilia mbali uingizwaji wa fedha ambao ni mdogo, ningeiomba Serikali iliangalie suala hili la uingizwaji wa fedha katika ofisi hii ili iweze kufanya shughuli zake kwa ufanisi na kwa uzuri kama inavyotakiwa.

Mhe. Naibu Spika, niingie katika kitabu moja kwa moja ukurasa wa 3.5 "Kuimarisha Usimamizi wa Mazingira na Matumizi Endelevu ya Maliasili". Kwa kweli hivi sasa miongoni mwa mambo ambayo wananchi wetu wanashiriki ni uchafuzi wa mazingira katika ukataji wa miti, uchimbaji wa mchanga, uchimbaji wa mawe, uharibifu wa mazingira na mengineyo.

Nataka hapa nizungumzie kuhusu habari ya ukataji wa miti ovyo. Ukataji wa miti, una ulazima mkubwa katika mazingira yetu kwa sababu tunatumia miti ama kwa kujengea, au/na kuni. Ningependa kumuuliza Mhe. Waziri ana mipango gani ya kushirikiana na Wizara nyengine zinazohusika ili kuweka kuni mbadala au matumizi ya kupikia mbadala, na matumizi mbadala ya majengo kabla ya kutumia hii miti ambayo kwa asilimia kubwa hivi sasa ndio tunayoitumia.

Mhe. Naibu Spika, baadhi ya nchi hivi sasa wamepunguza matumizi makubwa kabisa ya miti kwa kujengea, na katika milango labda na madirisha wanatumia vifaa vyengine, *glasses* na mengineyo. Je, Mhe. Waziri, ana mpango gani wa kushirikiana na vyombo husika na Wizara husika nyenginezo, ili kuondoa tatizo zima hili la ukataji wa miti ovyo.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 12 *paragraph* ya 28 hapa inatajwa ziara za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ndani na nje ya nchi. Kwa ufupi tu naomba Mhe. Waziri atufahamishe ni tija gani iliyopatikana katika safari 7 za nje za Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea niende katika ukurasa wa 18 *paragraph* ya 45, mchango wangu naomba ninukuu. Mhe. Waziri amesema hapa"kama inavyoeleweka kwamba kila mwaka tarehe 3 Disemba huwa ni siku ya kimataifa ya watu wenye ulemavu duniani. Kwa upande wa Zanzibar maadhimisho ya siku hiyo yalifanyika Dole, Wilaya ya

Magharibi Unguja ambapo ujumbe wa mwaka 2013 ni Ondoa Vikwazo Weka Fursa ili Kuwa na Jamii Jumuishi kwa Wote".

Mhe. Naibu Spika, watu wenye ulemavu kwa kweli ni wanadamu kama mwanadamu mwengine. Hawa wanahitaji upendo, ushirikiano, uhusiano wa hali ya juu ili wajisikie kwamba wao ni wanadamu kama wanadamu wenzao.

Mhe. Naibu Spika, juzi Mhe. Waziri alikuwa anajibu swali la watu wenye ulemavu ambao Zanzibar wamepata elimu pamoja na ajira. Nampongeza sana kwa sababu vijana wengi wenye ulemavu *Alhamdulillah* miongoni mwao wamepata ajira, na wapo ambao ni maafisa wa ngazi mbali mbali.

Sasa katika maeneo ya vijijini na mjini kuna skuli mbali mbali zinatoa elimu mjumuisho. Elimu mjumuisho ina maana kwamba wamekusanywa wanafunzi wenye mahitaji maalum pamoja na wanafunzi ambao wapo sahihi katika viungo vyao. Namuomba Mhe. Waziri anipe maelezo hapa, ana utaratibu gani na mpango gani wa kuwasaidia wanafunzi walio na mazingira magumu katika skuli za elimu mjumuisho hasa vijijini. Nazungumza hasa vijijini kwa sababu misaada mingi sana inayotoka huwa inazingatiwa mjini kuliko vijijini. Kwa hiyo namuomba Mhe. Waziri atueleze ni mpango gani ambao anashirikiana nao na walimu na wanafunzi hawa wa madarasa ya elimu mjumuisho.

Mhe. Naibu Spika, niendelee na mchango wangu katika ukurasa wa 24 wa kitabu hiki kuhusiana na suala zima la Tume ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya. Mhe. Naibu Spika, Tume hii ina kazi ngumu. Madawa ya kulevya ni janga la taifa, janga ambalo linapoteza nguvu kazi ya vijana wetu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali alizungumza kwa urefu sana kuhusiana na suala hili la madawa ya kulevya. Mimi sitaki nieleze kwa urefu isipokuwa naomba tu nimuulize Mhe. Waziri kwa mwaka huu ambao tunamaliza nao ni watu wangapi ambao wamekamatwa na dawa za kulevya na hatua gani ambazo zimechukuliwa dhidi yao.

Mhe. Naibu Spika, nataka niendelee na mchango wangu katika ukurasa wa 18, narudi nyuma kidogo kuhusiana na suala zima la hii *paragraph* ya 76. Naomba kunukuu inasema kwamba "Upatikanaji wa huduma za ukimwi kwa makundi maalum umeongezeka. Huduma za elimu ya ukimwi, ushauri nasaha na upimaji wa virusi vya ukimwi, usambazaji wa kondom na rufaa zimeongezeka kwa wanawake na wanaume".

Mhe. Naibu Spika, ukimwi ni tatizo na pia unawaangamiza vijana wetu. Naomba Mhe. Waziri awaeleze wananchi wetu juu ya usambazaji wa kondom unasaidia vipi kupunguza ukimwi.

Mimi nahisi kwamba usambazaji wa kondom bila ya utaalam haupunguzi ukimwi bali unawaruhusu watu kuendelea na mazoezi ya kusambaza ukimwi. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri aielimishe jamii usambazaji wa kondom unasaidia vipi katika kusaidia suala zima la kupunguza maambukizo ya ukimwi.

Mhe. Naibu Spika, mwisho wa mchango wangu niende katika uhifadhi wa mazingira. Uhifadhi wa mazingira ni jambo muhimu na kwa kweli kutokana na hali ilivyo hivi sasa kuna maeneo mbali mbali yanachimbwa mchanga ovyo. Namuomba Mhe. Waziri atoe taaluma ya kutosha kupitia Idara yake inayohusiana na mazingira.

Kwa mfano, pale katika jimbo langu kuna eneo maarufu sana linachimbwa mchanga na nafikiri katika Wilaya au Mkoa wa Kusini Pemba majumba mengi ambayo yanajengwa basi yanatumia mchanga kutoka eneo lile. Eneo lile Mhe. Mohammed Haji Khalid ananiuliza linaitwaje, ni maarufu Gining'i. Eneo hili linachimbwa mchanga wananchi wa pale wanahitaji vile vile kupewa maelekezo ya kutosha, ili ule uharibifu wa mazingira uweze kudhibitika kitaalam.

Mhe. Naibu Spika, kwa mchango huo naunga mkono hoja hii kwa asilimia tisini, baada ya kupata majibu ya masuala yangu nitaweza kuiunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwashukuru kwa ushirikiano wenu mlionipa kwa jioni hii ya leo. Na hapa tunaahirisha kikao chetu mpaka siku ya Jumatatu tarehe 26/05/2014 saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1:41 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 26/05/2014 saa 3:00 asubuhi)